# BUNGE LA TANZANIA

# MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA TATU

## Kikao cha Nne – Tarehe 3 Novemba, 2023

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Mwenyekiti (Mhe. Daniel B. Sillo) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa maswali; tunaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI Mheshimiwa Rehema Juma Migilla, Mbunge wa Ulyankulu sasa aulize swali lake.

Na. 45

### Uchaguzi wa Serikali za Mitaa – Ulyankulu

**MHE. REHEMA J. MIGILLA** aliuliza: -

Je, kuna mpango gani kuruhusu Kata za Kanindo, Igombemkulu na Milambo kufanya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Udiwani?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rehema Juma Migilla, Mbunge wa Jimbo la Ulyankulu kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua uwepo wa Kata za Kanindo, Igombemkulu na Milambo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua. Hata hivyo, maeneo hayo bado yana mwingiliano wa makazi ya wakimbizi na raia, hali ambayo huathiri utekelezaji wa shughuli za uchaguzi ndani ya maeneo hayo. Serikali inaendelea kushughulikia suala hili chini ya Ofisi ya Rais TAMISEMI na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ili kuhakikisha wananchi wa Kata hizo wanapata haki ya kushiriki kwenye shughuli za uchaguzi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rehema swali la nyongeza.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru; nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nipende kusema majibu ya Serikali kiukweli sijaridhika nayo kutokana na sababu zifuatazo. Serikali inatambua kwamba hizi kata zipo na ni maeneo yao kiutawala na huko nyuma hizi kata zilikuwa zinafanya uchaguzi wa kumchagua diwani na Wenyeviti wa Serikali za Mitaa na kwa kuwa kwenye majibu ya Serikali imesema kwamba kuna mwingiliano wa makazi ya wakimbizi na raia lakini wakati huo huo kuna uchaguzi unafanyika kumchagua Rais lakini pia kuna uchaguzi wa kumchagua Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa swali langu ni; je, ni sifa zipi ambazo hawa raia au hawa wakazi wa eneo hili wanazo ambazo zinawafanya waweze kumchagua Rais na kuweza kumchagua Mbunge? Lakini ni sifa zipi ambazo hawa raia wanazikosa kuweza kumchagua Diwani na Wenyeviti wao wa Serikali za Mitaa na Vitongoji na Vijiji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; tunajua kabisa katika maeneo ya kata kiongozi wa kushughulikia shughuli za maendeleo katika Kata husika huwa ni Diwani; sasa kata hizi hazina madiwani. Je, ni nani msimamizi wa shughuli za maendeleo katika hizi kata au ni kuniongezea mimi Mbunge majukumu ambayo yangefanywa na madiwani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naomba nianze kwa kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inatambua umuhimu wa wananchi hawa na vijiji hivi na kata hizi kuwa na viongozi wanaochaguliwa. Kwa sababu za kiusalama; maeneo yale yana mchanganyiko wa raia na mchanganyiko wa wakimbizi lakini na wale wakimbizi ambao wamepewa uraia hivi karibuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa sababu za kiusalama kuna kazi ya ziada inatakiwa kufanyika ili kujiridhisha na usalama wa wale ambao watakuja kushiriki katika shughuli za uchaguzi ili chaguzi hizo ziweze kwenda kwa mujibu wa taratibu lakini kwa kuzingatia usalama wa nchi yetu. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba suala hilo linahitaji umakini mkubwa ili twende katika njia ambayo ni salama zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala la kwamba wanachagua viongozi wa Kitaifa kwa maana ya Mheshimiwa Rais lakini pia Mheshimiwa Mbunge; ni sawa lakini ikumbukwe kwamba Mwenyekiti wa Kijiji atatoka ndani ya Kijiji kile, utajiridhishaje *beyond reasonable doubt* kwamba yule Mwenyekiti siyo mkimbizi au ni raia ambaye bado hajapata uraia rasmi? Kwa hiyo, ndiyo maana taratibu zinaendelea na nikuhakikishie tu kwamba Serikali inaendelea na mchakato huo kuhakikisha kwamba tunakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji na kata hizi zina maafisa wanaoitwa Wakuu wa Makazi ya Wakimbizi ambao wale

wanawajibika kutoa taarifa mbalimbali za Kiserikali kwenda ngazi ya halmashauri, wilaya na ngazi nyingine. Kwa hiyo, pamoja na kwamba hakuna madiwani na wenyeviti lakini kuna uwakilishi wa Wakuu wa Makazi ya Wakimbizi katika maeneo yale, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante; Mheshimiwa Boniphace Getere swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Naomba tu nijazilize hapo alipoongelea Mbunge aliyemaliza kuongea. Mtu mwenye sifa za kupiga kura za Urais ni raia wa Tanzania mwenye uraia wa Tanzania mwenye sifa za kupiga kura, maana yake ni raia amejiandikisha, ana umri wa miaka 18, ni raia wa Tanzania; sasa kama hao wana sifa za kupiga kura za Rais wametambulika kwamba ni Watanzania, kwa nini hawachagui Diwani? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge hizo ni sehemu ya sifa za mpiga kura lakini kama nilivyotangulia kusema, kuchagua viongozi ngazi ya vijiji vile na ngazi ya kata zile ambazo zina mchanganyiko mkubwa wa wakimbizi na watu ambao siyo raia kunahitaji umakini mkubwa ili kulinda usalama wa nchi na Serikali inaendelea kuchukua hatua ambazo zitawawezesha sasa kwenda kufanya uchaguzi huo baada ya kujiridhisha na mazingira ya kufanya chaguzi katika maeneo hayo, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Florence George Samizi, Mbunge wa Muhambwe sasa aulize swali lake.

Na. 46

**Ukarabati wa Kituo cha Afya cha Kifura – Muhambwe**

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itakarabati Kituo cha Afya cha Kifura – Muhambwe?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Florence George Samizi, Mbunge wa Jimbo la Muhambwe kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Afya Kifura kilichopo Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo ni moja ya vituo vya afya 199 chakavu ambavyo Ofisi ya Rais TAMISEMI imeviainisha. Serikali inaendelea kutenga bajeti kwa ajili ya ukarabati na kuongeza majengo kwenye vituo vya afya chakavu vyote nchini kikiwemo Kituo hiki cha Afya cha Kifura, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Samizi swali la nyongeza.

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi niweze kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Kituo cha Afya cha Kifura ambacho Serikali imekiri kwamba ni chakavu sana kinapokea wagonjwa wa nje 110 hadi 150 kwa siku lakini kinazalisha kinamama 120 mpaka 150 kwa mwezi. Je, kutokana na mzigo wa wagonjwa wengi ulioko katika Kituo hiki chakavu, Serikali haioni sasa iko sababu ya kuharakisha mchakato wa kuleta pesa za ukarabati wa Kituo hiki cha Afya cha Kifura? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; Serikali iliahidi kumalizia ujenzi wa Kituo cha Afya cha Nyaruyoba kupitia ziara ya Mheshimiwa Makamu wa Rais mwaka 2021. Kituo hiki cha Afya cha Nyaruyoba kinahudumia takribani kata tatu ikiwemo Mkabule, Rusohoko na Kigaga iliyoko Kata ya Rugongwe. Je, Serikali haioni iko sababu ya kuharakisha kuleta pesa za kumalizia Kituo hiki cha Afya ambacho kinahudumia takribani kata nne katika Jimbo la Muhambwe? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba nianze tu kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa namna ambavyo amefuatilia ahadi hizi za Serikali kuhakikisha kwamba zinakarabati Kituo cha Afya cha Kifura na ni kweli kituo hiki ni chakavu, kina upungufu wa miundombinu na kinahudumia wananchi wengi. Nimhakikishie kwamba katika mpango wa Benki ya Dunia hivi karibuni, hiki ni miongoni mwa vituo ambavyo vimeingizwa na tunaamini fedha zitakwenda kwa ajili ya kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili ni kweli kwamba Kituo cha Afya cha Nyaruyoba ni ahadi ya Mheshimiwa Makamu wa Rais nimhakikishie kwamba tayari Serikali inaendelea kutafuta fedha na mapema iwezekanavyo fedha ikipatikana itapelekwa kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Kituo hiki cha Afya, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa swali la nyongeza.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwenye Jimbo la Ndanda tuna vituo kwenye Kata ya Ndanda, Kijiji cha Chiroro, Lukuledi, Ngalole, Chikundi pamoja na Namajani. Vituo hivi vimeshakamilika ujenzi wake zaidi ya miaka miwili sasa hivi lakini hata hivyo havijafunguliwa na kuanza kutoa huduma kwa wananchi kwa sababu ya mapungufu madogo madogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimuulize Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba; je, yuko tayari kutoa maelekezo kwa Halmashauri yetu ya *Masasi DC* ili vituo hivi vikamilishwe na kuanza kutoa huduma kwa wananchi kwani zile shilingi milioni 50 zilizoletwa na Serikali hivi sasa majengo haya yameanza kuchakaa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Cecil Mwambe, Mbunge wa Jimbo la Ndanda kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kuwapongeza Wananchi wa Jimbo la Ndanda kwa kujenga kutumia nguvu zao lakini Serikali iliwaunga mkono kuwapelekea shilingi milioni 50 kwa ajili ya ukamilishaji wa zahanati hizi na vituo hivi na vimekamilika vitoe huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nitumie fursa hii ya Bunge lako tukufu kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kuwaelekeza Wakurugenzi wote wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuzingatia maelekezo ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwamba vituo vikikamilika vinabaki hatua ndogo ndogo za ukamilishaji, vifaatiba kwa ajili ya kuanza kutoa huduma. Ni lazima watoe kipaumbele kuhakikisha vinakamilika mapema na vinaanza kuwahudumia wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kwa Wakurugenzi wote nchi nzima, lakini mahususi nitoe maelekezo kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi kuhakikisha vituo hivi ambavyo vimetajwa na Mheshimiwa Mbunge wa Ndanda mapema iwezekanavyo ndani ya miezi mitatu tuhakikishe vituo hivi vimekamilishwa na vinaanza kutoa huduma kwa wananchi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mbunge wa Namtumbo sasa aulize swali lake.

Na. 47

**Hitaji la walimu Namtumbo**

**MHE. VITA R. KAWAWA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itapeleka Walimu kukidhi mahitaji katika Shule za Sekondari na Msingi Wilayani Namtumbo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mbunge wa Jimbo la Namtumbo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikiajiri walimu wa Shule za Msingi na Sekondari kwa awamu kwa kuzingatia upatikanaji wa fedha. Katika mwaka wa fedha 2022/2023 na 2021/2022, Serikali iliajiri walimu 22,930 ambapo walimu 111 walipangiwa katika shule zilizopo kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kupeleka walimu kwenye Shule za Msingi na Sekondari zikiwemo zilizopo katika Wilaya ya Namtumbo kulingana na uhitaji lakini pia kulingana na upatikanaji wa fedha, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa swali la nyongeza.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa fursa hii kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa uwiano wa idadi ya walimu tuliopata katika shule za msingi na sekondari haulingani na walimu waliofariki, waliostaafu na waliohama kwa vibali vya TAMISEMI hivyo kufanya uhaba mkubwa kuendelea kuwepo.

Je, Serikali inaweza kutupa kipaumbele wilaya za pembezoni ikiwemo Namtumbo kutuongezea idadi ya walimu wakati inagawa walimu hao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa shule za msingi za Namtumbo tuna walimu 867 na tuna upungufu wa walimu 418; je Serikali inaweza kutuletea walimu kupunguza upungufu huo kwa sasa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwanza katika utaratibu wa ajira za walimu lakini pia watumishi wa Sekta ya Afya kuanzia mwaka wa fedha 2021/2022 walimu na watumishi wa afya wanaomba kwa njia ya kielektroniki lakini wanapangiwa kwa uwiano na idadi kubwa kwenda kwenye halmashauri za pembezoni zenye upungufu mkubwa zaidi wa watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali tayari imeshaanza kulifanyia kazi jambo hilo na ajira zote ambazo zitaendelea kuja zitakuwa zinakwenda kupeleka watumishi wengi zaidi maeneo ya vijijini na maeneo yenye upungufu mkubwa zaidi na Ofisi ya Rais, TAMISEMI tayari ina *data base* ya maeneo yote yenye changamoto kubwa zaidi ya walimu kama ilivyo Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie kwamba eneo hili la walimu tutaendelea kutoa kipaumbele katika Halmashauri hii ya Namtumbo na halmashauri nyingine zote za pembezoni likiwemo suala la upungufu wa walimu 418 ambalo kadiri ya ajira tutahakikisha kwamba tunatoa kipaumbele kupunguza *gap* ya watumishi katika Halmashauri ya Namtumbo, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru; kutokana na upungufu wa walimu kuna walimu ambao wameendelea kujitolea katika shule za msingi na shule za sekondari kwa kulipwa na wananchi. Sasa ni kwa nini Serikali walau isiwape mkataba wa muda ili kuwapa motisha waendelee kufundisha wakati wakisubiri kuajiri walimu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, Serikali ilikwishatoa kwanza maelekezo kwa Wakuu wa Shule lakini kwa maana ya Wakurugenzi katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwamba wanaweza wakaajiri walimu wa kujitolea kwa muda wakati Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuwaingiza kwenye utaratibu wa ajira za kudumu; kwa hiyo, jambo hilo linaendelea kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namna ya kuweka mikataba, Serikali imeandaa mwongozo mahususi ambao utapelekea kuandaa mfumo ambao utawezesha walimu wanaojitolea kutambuliwa rasmi kwenye mfumo kuepuka udanganyifu wa baadhi ya Wakuu wa Shule wasiowaaminifu ambao mara nyingi wamekuwa wanaleta majina kwa mfano wakati wa ajira walimu ambao wanajitolea lakini wanaleta pia walimu ambao hawajitolei. Kwa hiyo, tunataka tuwe na mfumo mahususi ambao walimu wenyewe watajisajili na Ofisi ya Rais, TAMISEMI itakwenda kuhakiki na kujiridhisha ili ajira zinapotokea waweze kupata kipaumbele cha kuajiriwa katika ajira za kudumu, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Midimu swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Shule za Sekondari na Msingi Mkoa wa Simiyu zina upungufu mkubwa wa walimu. Je, ni lini Serikali itapeleka walimu wa kutosha katika shule za msingi na sekondari Mkoa wa Simiyu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, Serikali imeendelea kupeleka walimu wa Shule za Msingi na Sekondari katika Halmashauri zote za Mkoa wa Simiyu kuanzia ajira za 2021/2022, 2022/2023 lakini pia katika ajira za mwaka huu wa fedha 2023/2024 tutatoa kipaumbele

kuhakikisha kwamba walimu zaidi wanaendelea kupelekwa katika shule za Mkoa wa Simiyu, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda swali la nyongeza.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa swali la nyongeza. Mheshimiwa Waziri katika Bunge la Bajeti tulikuuliza swali la mfumo kuwakataa walimu wanaojitolea. Unaweza ukatoa ni lini Serikali itafanya haraka ili mfumo huo uweze kuwaelewa walimu wanaojitolea na waweze kupata ajira na kuachwa wakati muda mrefu wanajitolea?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge kwamba wapo walimu ambao wamekuwa wakijitolea lakini mfumo wetu wa kuwatambua rasmi na kuthibitisha kwamba wanajitolea ili wapate kipaumbele cha ajira ulikuwa haujaandaliwa. Kwa hiyo, hivi sasa Serikali iko kwenye hatua za mwisho za kukamilisha mfumo ambao utawatambua na kuhakikisha kwamba wanaajiriwa kwa kipaumbele kila fursa zinapojitokeza, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge, tunakushukuru sana. Tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji, Mbunge wa Mwera sasa aulize swali lake.

Na. 48

**Changamoto za Muungano**

**MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI** aliuliza:-

Je, Serikali ipo tayari kuleta marekebisho ya Sheria baada ya Serikali kukubaliana kuondoa baadhi ya changamoto za Muungano?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira Mheshimiwa Khamis majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji, Mbunge na mtumishi wa Wananchi wa Jimbo la Mwera kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Changamoto zote za Muungano zimekuwa zikitatuliwa na kupatiwa ufumbuzi kwa njia ya Majadiliano na Maridhiano utaratibu ambao umekuwa na mafanikio makubwa. Aidha, katika utatuzi wa Changamoto hizo umeandaliwa utaratibu wa vikao vya Kamati ya Pamoja ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ajili ya kushughulikia Masuala hayo ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu huu umetumika kwa mafanikio makubwa na kuhakikisha changamoto nyingi za Muungano zinatatuliwa. Hata hivyo, ushauri wa Mheshimiwa Mbunge ni mzuri na Serikali inaangalia uwezekano wa kufanya vikao vya pamoja baina ya SJMT na SMZ ili changamoto zilizotatuliwa kupewa na nguvu ya kisheria, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zahor swali la nyongeza.

**MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi. Sasa naomba Mheshimiwa Waziri anipe majibu; je, ni lini Serikali italeta Muswada wa Mabadiliko ya Sheria ili mambo yote ambayo yameondolewa kwenye changamoto za Mambo ya Muungano yaonekane kwenye Sheria? Nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue fursa hii

nimpongeze sana Mheshimiwa Zahor kwa kazi nzuri anayoifanya Jimboni lakini pia kazi anayoifanya katika kutaka wananchi wajue na wapate taaluma juu ya masuala yanayogusa mnasaba wa Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kikao chetu cha tarehe 6 Disemba, 2022, miongoni mwa ajenda ambayo iliibuka katika kikao kile ni namna gani changamoto zilizokuwa zimeshatatuliwa tukaziweka katika *legal document*. Miongoni mwa kazi ambayo tuliwapa tulitoa maelekezo kwa wanasheria wetu wa pande zote mbili za muungano waende wakakae wakaone namna ya kuweza kuanza mchakato huu ili lengo na madhumuni tuweze kuyaingiza katika *legal document*. Hii itasaidia kizazi kijacho kuyatambua haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimuombe Mheshimiwa Mbunge awe na subira kidogo, kazi inafanyika, wanasheria tumeshawapa kazi na watakuja kutuletea majibu na hili jambo la kuifanya ikawa kwenye *document* ya kisheria inakwenda kufanyika, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu hayo. tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa George Ranwell Mwenisongole Mbunge wa Mbozi sasa aulize swali lake.

Na. 49

**Wakulima wa Kahawa Mbozi kukatwa shilingi 200 kwa kilo**

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE** aliuliza: -

Je, kwa nini wakulima wa kahawa Mbozi wanakatwa shilingi 200 kwa kilo licha ya tamko la kusitisha tozo hiyo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo naomba kujibu swali la Mheshimiwa George Ranwell Mwenisongole, Mbunge wa Jimbo la Mbozi kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatekeleza Mkakati wa Maendeleo ya Tasnia ya Kahawa unaolenga kuongeza uzalishaji wa kahawa kutoka wastani wa tani 68,147 kwa mwaka wa fedha 2018/2019 hadi kufikia wastani wa tani 300,000 kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Wadau wa kahawa walikubaliana kukusanya shilingi 200 kwa kilo ya kahawa safi ili kugharamia shughuli mbalimbali za maendeleo ya zao la kahawa kama zilivyoainishwa kwenye mkakati huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizo zinazokusanywa na Bodi ya Kahawa Tanzania zinatumika kutekeleza shughuli za maendeleo ya zao hilo zikiwemo uzalishaji wa miche bora, kuboresha shughuli za utafiti wa kahawa, upatikanaji wa pembejeo na kuimarisha masoko ya kahawa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa George swali la nyongeza.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza kabisa, Mheshimiwa Waziri wakati akihitimisha bajeti hapa alisema kwamba hiyo tozo atakuwa analipa mnunuzi, na kwa hiyo wakulima wa arabica nchini hawatalazimika kulipa shilingi 200.

(a) Je, kwa nini bodi bado inaendelea kuwatoza?

(b) Je, kwa nini basi mnunuzi asiambiwe rasmi kwamba awe analipa hiyo, na ijulikane kwenye *Hansard*?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana naomba nimjibu Mheshimiwa Mbunge kwamba ni kweli Mheshimiwa Waziri alipokuwa anazungumza hapa wakati wa Bunge alilitolea ufafanuzi, na ndiyo maana hii bei ya shilingi 200 ikawa inawekwa katika bei ile ya jumla ya soko, kwa maana

mnunuzi analipa moja kwa moja na katika ile sehemu mkulima anakatwa. Hata hivyo, mapendekezo yake sisi tunayapokea na tutayapitia upya ili tuone namna bora ambayo mkulima ataona athari za moja kwa mojo za makato hayo ya shilingi 200. Ahsante sana.

**MWENNYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana. Tunaendelea na swali linalofuata. Mheshimiwa Jonas William Mbunda Mbunge wa Mbinga mjini sasa aulize swali lake.

Na. 50

**Hitaji la Skimu ya Umwagiliaji Kata ya Kihungu, Mbinga**

**MHE. JONAS W. MBUNDA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itajenga Skimu ya Umwagiliaji Kata ya Kihungu, Mbinga?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na kwa niaba ya Waziri wa Kilimo naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jonas William Mbunda, Mbunge wa Jimbo la Mbinga Mjini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inaendelea na usanifu na ujenzi wa skimu mbalimbali nchini kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ikiwemo skimu za Sanga Lugalagala, Sanga Mabuni, Mkungwe na Kimbande zilizopo Wilaya ya Mbinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inaendelea na utambuzi wa maeneo mengine yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji kwa ajili ya kufanyiwa usanifu na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Kati ya maeneo yatakayofikiwa na wataalamu ni pamoja na Kata ya Kihungu iliyopo Wilaya ya Mbinga.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jonas Mbunda swali la nyongeza.

**MHE. JONAS W. MBUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza, naomba niishukuru Serikali kwa kuweka mpango wa kufanya usanifu pamoja na kujenga miundombinu katika skimu ya umwagiliaji kwenye eneo la Kata ya Kihungu kwa Mwaka 2024/2025. Nina swali moja la nyongeza. Katika Kata ya Mpepai eneo la Mtuwa na Ruvuma Chini nayo ni maeneo ambayo yanafaa kwa ajili ya kujenga za umwagiliaji;

Je, Serikali inampango gani wa kuhakikisha kwamba maeneo hayo yanajengewa skimu za umwagiliaji?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Moja, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba malengo ya Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ni kuhakikisha kwamba kilimo tunachokipeleka sasa ni kile ambacho kitakuwa kinategemea maji badala ya mvua. Yaani tunataka Mtanzania alime katika misimu yote, yaani kwa maana kipindi cha kiangazi awe na shughuli ya kufanya ya kilimo lakini na kipindi cha msimu wa mvua afanye hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo haya maeneo ambayo ameyaainisha Mheshimiwa Mbunge ni maeneo yote ambayo Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inayapitia ili kuhakikisha kwamba yote tunayatafutia fedha na yanaingia katika mpango ili yaweze kutekelezeka, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rashid Shangazi swali la nyongeza.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule katika Jimbo la Mlalo Tarafa ya Umba kwa maana ya Kata ya Mng'aro, Lunguza, Mnazi lakini

na Kijiji cha Kivingo tumeshatenga maeneo kwa ajili ya skimu hizi za umwagiliaji;

Je, lini miradi hii itaanza?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana naomba nimjibu Mheshimiwa Rashid Shangazi Mbunge wa Jimbo la Mlalo kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua kwamba haya maeneo yote ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyataja ya Mng'aro, Lunguza, Mnazi na Kivingo wameshayaandaa kwa ajili ya shughuli hiyo. Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inayafanyia kazi; na tukishamaliza kazi hiyo basi miradi hiyo itatekelezeka. Kikubwa ambacho niwaondoe shaka Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Rais ameweka *commitment* kubwa kwenye miradi yote ya umwagiliaji na fedha ipo kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hii. Kwa hiyo, tutafikia takriban miradi yote nchini, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ishengoma swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni lini Serikali itajenga skimu za umwagiliaji kwenye Kata za Minepa, Mazimba na Lupiro Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kama nilivyojibu swali la msingi, lakini vilevile swali la nyongeza la Mheshimiwa Rashid Shangazi, nimjibu tu Mheshimiwa Christine Ishengoma kwamba maeneo yote haya ambayo yanafaa kwa ajili ya umwagiliaji tumeiagiza Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kuyapitia yote nchini kuyaweka katika mpango makakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mpaka sasa hivi tumeshafikia takriban asilimia 70 ya maeneo yote ambayo yanafaa kwa kilimo.

Kwa hiyo, hata haya nayo mengine yamefikiwa mengine tunaendelea na utekelezaji wake. Kwa hiyo nimuondoe shaka kazi hiyo inafanyika. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Skimu za mifereji ni skimu ambazo zilikuwepo na kule kwetu Vunjo zimekuwa zinaweza zikaleta matokeo chanya kwenye kuongeza tija kwenye kilimo. Kwa kuwa Tume ya Umwagiliaji imeshafika kutafiti na kuziangalia skimu hizi, je, Waziri anaweza akanihakikishia kwamba wataenda haraka na kuanza kukarabati mifereji ile?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge wa Vunjo Dkt. Charles Kimei kwamba hiyo kazi tutaifanya kwa haraka iwezekanavyo kwa sababu tumepewa rasilimali zote kutekeleza jambo hili; kwa hiyo, liko ndani ya uwezo wetu. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ndaisaba swali la nyongeza.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Serikali kupitia Tume ya Umwagiliaji ya Taifa ilifika Ngara ikaanza kujenga Skimu ya Umwagiliaji ya Vigondo ila ikaitelekeza kwa miaka saba iliyopita. Naomba *commitment* ya Serikali;

Je, ni lini Serikali itafika Vigondo, Rulenge na Ngara kuja kukamilisha mradi wa Skimu ya umwagiliaji ya Vigondo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana nimjibu Mheshimiwa Ndaisaba Mbunge wa Jimbo la Ngara kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri jambo lake tumelizungumza jana na tumeshalifikisha kwa Mkurugenzi wa Tume; kwamba miradi yote ya nyuma ambayo ilikuwa imesimama tunaipa kipaumbele itekelezeke na ikamilike kwa wakati, na miradi mipya ambayo tunataka isaidie wakulima wote nchini nayo itakamilika. Ndiyo maana nimesema kwamba bahati nzuri Mheshimiwa Rais kama ni fedha ametupa kwa ajili ya kutekeleza miradi hii na sisi tutaitekeleza kama maelekezo ya Mheshimiwa Rais na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ally Kassinge, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi ya swali la nyongeza. Ni muda mrefu sasa tangu serikali itoe ahadi ya kupeleka wataalam ili wakafanye upembuzi na usanifu kwa ajili ya Skimu ya Umwagiliaji ya Makangaga Kata ya Kiranjeranje katika Jimbo la Kilwa Kusini kazi hiyo bado haijafanyika mpaka sasa; je, ni lini sasa Serikali itatekeleza ahadi yake ya kwenda kufanya usanifu huo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante Mradi wa Makangaga uko katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 kwa ajili ya kufanyiwa usanifu, kwa hiyo unatekelezeka katika mwaka huu wa fedha. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu kwa Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Mheshimiwa Edward Olelekaita Kisau Mbunge wa Kiteto sasa aulize swali lake.

Na. 51

**Hitaji la Mnara wa TBC Radio, Kiteto**

**MHE. EDWARD O. KISAU** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga Mnara wa TBC – Kiteto?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Mawasiliano Mheshimiwa Mhandisi Andrew Kundo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari napenda kujibu swali la Mheshimiwa Edward Kisau Olelekaita, Mbunge wa Kiteto kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imepanga kujenga mnara wa redio Wilayani Kiteto katika mwaka huu wa fedha 2023/2024 na ujenzi huo unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Februari, 2024, ahsante.

**MWENEKITI:** Mheshimiwa Edward Olelekaita swali la nyongeza.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru, na nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri mafupi yenye *time frame,* kwa kweli wananchi wa Kiteto wamesikia na tangu uhuru hawakuwahi kusikia Redio Tanzania. Lakini pamoja na hayo nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiteto ni kubwa sana, nataka kujua; Je, mnara huu wa Redio mnaojenga uta-*cover* eneo kubwa kiasi gani? Swali la pili; mwaka wa fedha 2023/2024 kuna vijiji takriba 20 na zaidi mlikuwa mmepanga kwamba mtajenga minara ya simu kwenye Kata za Dosidosi, Laiseri, Loolera, Magungu, Namelock, Ndirgishi, Njoro, Olboloti, Partimbo na Songambele. Nataka mniambie lini hasa miradi hii itaanza ili wananchi wa kiteto wapate mitandao ya simu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Olelekaita kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa mtambo huu utakapokamilika utaweza kuhakikisha kwamba huduma hii inapatikana katika Wilaya nzima ya Kiteto na kwa bahati nzuri Mheshimiwa Mwenyekiti tunamtambo mwingine upo pale Kilindi, ule mtambo utaweza kusaidiana vizuri kabisa na mtambo ambao tutaukamilisha pale Kiteto, na Wilaya nzima ya Kiteto haitokuwa na changamoto yoyote ya mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili ametaja Kata za Dosidosi, Laiseri, Lengatei nafikiri majina kama hayo lakini katika kata zote 12 kata moja ndiyo inaenda kuhudumiwa na Halotel, kata saba zinaenda kuhudumiwa na Airtel, kata tatu zinaenda kuhudumiwa na Tigo na kata moja ambayo ni ya Songambele inaenda kuhudumiwa na Vodacom.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mradi huu uko katika hatua nzuri kabisa kwa sababu nafikiri mmeshaanza kuona wanapita huko kwa ajili ya kutafuta maeneo kwa ajili ya kuingia mikataba ili ujenzi uanze rasmi. Nakuhakikishia Mheshimwa Mbunge tuendelee kushirikiana ili maendeleo kutokana na mawasiliano yaweze kupatikana. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Profesa Ndakidemi, swali la nyongeza.

**MHE. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa fursa.

Je, wakandarasi waliopewa kazi ya kujenga minara katika Kata za Uru Shimbwe, Kibosho Kati na Mabogini wako katika hatua gani? Kwani wananchi wanashauku kubwa kuona minara hii ikijengwa na ikianza kufanya kazi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Profesa Ndakidemi Patrick Mbunge wa Moshi vijijini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mradi wetu wa Tanzania ya Kidijitali Mheshimiwa Ndakidemi alipata kata tatu ambayo ni Uru Shimbwe ambapo mtoa huduma Tigo anaenda kuweka huduma ya mawasiliano. Pia na Kibosho Kati ni Tigo vilevile, na Mabogini tutakuwa na Vodacom.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimejibu katika swali la nyongeza la Mheshimiwa Olelekaita, watoa huduma wako katika hatua mbalimbali; nafikiri Waheshimiwa wengi tayari wameshanipa mrejesho kwamba wameanza kuwaona wanapita kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wanapata maeneo kwa ajili ya kuingia mikataba ya ujenzi wa minara yetu ya mawasiliano. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Condester, swali la nyongeza.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi. Mheshimiwa Waziri nakuja kwako tena leo kwa mara ya saba, naomba *commitment* yako. Je, ni lini utatuboreshea mawasiliano kwenye Kata ya Mkomba, Kata ya Kapele na Ming'ong'o Chitete na maeneo mengine yote ambaypo kuna changamoto ya mawasiliano ndani ya Jimbo la Momba?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Condester Sichalwe kwa niaba ya wananchi wake wa Jimbo la Momba kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa Mheshimiwa Mbunge amekuwa mstari wa mbele kuhakikisha kwamba anawatetea wananchi wake wa Jimbo la Momba; lakini kwa bahati mbaya katika Mradi wetu wa Tanzania Kidijitali haikuweza kuchukua kata zote kwa sababu tunaelewa kwamba changamoto ya mawasiliano bado ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini habari njema sasa ni kwamba Mheshimiwa Rais ameshapata fedha na tayari Wizara

yetu iko katika mchakato wa kukamilisha mambo ya mikataba ili tupate fedha kwa ajili ya kwenda kujenga minara mingine Zaidi. Ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kata ambazo amezitaja tutahakikisha kwamba zinakuwa sehemu ya utekelezaji wa mradi huo, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kajege swali la nyongeza.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Je, ni lini Serikali itajenga minara ya kutosha kwa ajili ya Jimbo la Mwibara?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Charles Kajege Mbunge wa Mwibara kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kajege tayari ameshanijulisha changamoto ya mawasiliano katika jimbo lake na tayari maeneo yake nimeshayachukua tutawatuma wataalamu wetu wakafanye tathmini ili tujiridhishe na ukubwa wa tatizo ili tupeleke ufumbuzi wa tatizo kulingana na changamoto iliyoko kule, ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu kwa Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Atupele Fredy Mwakibete Mbunge wa Busekelo sasa aulize swali lake.

Na. 52

**Mkataba wa ujenzi wa Barabara ya Katumba – Mbambo hadi Tukuyu**

**MHE. ATUPELE F. MWAKIBE** aliuliza: -

Je, lini Mkataba wa Ujenzi wa Barabara ya Katumba – Mbambo hadi Tukuyu utasainiwa kwa kuwa Mkandarasi alishapatikana?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Niabu Waziri wa Ujenzi ,Mheshimiwa Godfrey Kasekenya, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Atupele Fredy Mwakibete, Mbunge wa Busokelo kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, taratibu za manunuzi ya mkandarasi kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya Barabara ya Katumba Lupaso (km 35.3) na Kibanja Tukuyu (km 20.7) zimekamilika, hatua inayofuata ni kumkabidhi mkandarasi eneo la kazi *(signing),* ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Fredy swali la nyongeza.

**MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina swali moja la nyongeza. Kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa ujenzi wa barabara hii kwa kilomita 27 na sasa bado kilomita 56. Je, ni lini hizi kilomita zilizobaki zinakwenda kusainiwa ukizingatia kwamba Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi kaka yangu Innocent Bashungwa pamoja na Mheshimiwa Waziri wa Fedha walitembelea Jimbo la Busokelo tarehe Mosi Oktoba na walifanya mkutano mzuri sana. Tunawashukuru sana kwa kuja, ninyi ni mashuhuda wazuri kwamba barabara hii inahitaji kujengwa kwa kiwango cha lami. Je, ni lini itasainiwa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu. Naona amesimama Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Waziri karibu.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri pia nampongeza Mheshimiwa Mwakibete kwa kuupiga mwingi kwa ajili ya wananchi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara anayoitaja Mheshimiwa Mwakibete ni moja ya barabara 15 ambazo tunasubiri kusaini. Nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote wa barabara hizi, Mheshimiwa Rais ameshatoa kibali kama Mheshimiwa Naibu Waziri alivyosema. Tumeona tuandae siku ambayo tutasaini mikataba hii kwa siku moja halafu baada ya hapo mimi pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri tutaambatana na Waheshimiwa Wabunge kwenda kuwakabidhi wakandarasi kwenye Majimbo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba Waheshimiwa Wabunge, tuko mbioni katika kuandaa tukio hili ambalo tutaomba Kiongozi Mkuu wa Kitaifa aweze kushuhudia utiaji saini huu. Nawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaenda kufanya kazi na miradi hii 15 ina thamani ya shilingi 1,034,000,000. Natumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais na Waheshimiwa Wabunge wamefanya kazi kubwa ya ufuatiliaji. Tumefika hatua nzuri na Serikali ya Awamu ya Sita hakika katika kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi imejipanga vizuri, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Wizara hiyo hiyo, Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 53

**Matumizi ya teknolojia ya kisasa katika kusafisha barabara**

**MHE. ESTHER N. MATIKO** aliuliza:-

Je, kwa nini Serikali isitumie teknolojia na vifaa vya kisasa kusafisha barabara za *TANROADS*?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imelichukua wazo la Mheshimiwa Mbunge na itaona ni namna gari nzuri ya kujumuisha teknolojia na vifaa vya kisasa katika kufanya usafi wa barabara pasipo kuathiri ajira za vikundi maalum ambavyo vimesajiliwa na Halmashauri za Miji, Wilaya, Mikoa, Manispaa na Majiji kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2011 na Kanuni zake za mwaka 2016, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza niseme tu nasikitika na majibu kwa sababu nilielekeza swali langu *TANROADS* kwa maana ya *highways,* lakini hapo anajibu vikundi vilivyosajiliwa na Halmashauri, Manispaa na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutumia teknolojia ya kisasa kwa maana ya magari yangeweza kuwa yanasafisha hizi *highway* usiku ambapo kuna msongamono mdogo sana wa magari. Nataka kujua, Serikali imeshafanya *cost benefit analysis* kuweza kujua matumizi ya vifaa vya kisasa *vis a vis* wanavyosafisha kwa mikono ina faida gani kwenye uchumi wa Kitaifa? Kwa maana vifaa vya kisasa vinapunguza msongamano wa magari, ajali na madhara mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; Serikali imeshafanya tafiti kuweza kujua madhara wanayopata wananchi wanaofanya usafi kwa mikono kusafisha barabara na mitaro? Wameshafanya tafiti za kiafya kujua madhara wanayopata wananchi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kama nilivyosema kwenye jibu la msingi, wazo la Mheshimiwa Mbunge Serikali imelichukua, hilo la kwanza.

Suala la pili, ni kwamba *TANROADS* pia ina barabara ambazo ziko katika Majiji, Miji, Manispaa na hata katika Halmashauri za Wilaya. Hayo maeneo ndiyo hasa ambayo yameonekana yanakuwa na uchafu mwingi ambayo yanahitaji kufanyiwa usafi. Hata hivyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba kazi ya kufanya usafi wa barabara huwa tunatoa kwa wakandarasi na hawajalazimishwa kwamba ni lazima watumie watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana kwa sasa pale Dar es Salaam tayari tuna wakandarasi wawili ambao wameshaanza kutumia teknolojia hii ya kutumia magari kusafisha barabara zetu. Pia, namkumbusha Mheshimiwa Mbunge kwamba tuna Sheria inayotutaka katika kila mwaka vikundi vingapi, watu wangapi ambao wamepewa kazi hizi za kufanya usafi, kwa hiyo ni takwa pia la kisheria ambalo ni lazima tulitimize.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesema tutakapokuwa tumejiridhisha, kwamba kuna haja sasa pengine ya kubadilisha sheria kwamba tuelekeze zaidi kwenye matumizi ya vifaa vya kisasa, hilo litafanyika na ndiyo maana tumesema wazo hilo tumelichukua. Hili ni pamoja na kuangalia kama kuna madhara kiasi gani ambayo wanaofanya usafi kwa njia ya mikono ambavyo ni vikundi vya watu maalum hasa vikundi vya akinamama na vijana ambavyo mara nyingi ndiyo vitakuwa vinafanya kazi. Tutafanya hizo tafiti kwa kuwa hilo wazo tumelichukua na tutalifanyia kazi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Wizara hiyo hiyo, Mheshimiwa Ally Juma Makoa, Mbunge wa Kondoa Mjini sasa aulize swali lake.

Na. 54

**Hitaji la mbadala wa Shule ya Msingi Unkuku iliyopitiwa na barabara**

**MHE. ALLY J. MAKOA** aliuliza:-

Je, ni lini *TANROADS* watalipa fidia kwa kujenga shule mbadala baada ya shule ya Msingi Unkuku kupitiwa na Barabara ya Dodoma – Arusha?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ally Juma Makoa, Mbunge wa Kondoa Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)*, Mkoa wa Dodoma ilikwishalipa fidia kwa jengo la Shule ya Msingi Unkuku, miti pamoja na sehemu ya eneo la shule ambavyo viliathiriwa na ujenzi wa barabara ya Dodoma – Babati ambapo mnamo tarehe 10 Septemba, 2014 kiasi cha shilingi 8,370,221.00 kililipwa kwa Mkurugenzi wa Halmasauri ya Wilaya ya Kondoa, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ally Juma Makoa, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY J. MAKOA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa fidia aliyoitaja Mheshimiwa Naibu Waziri ililipwa mwaka 2014 wakati barabara ilikuwa na upana wa mita 22. Mwaka 2017 walipokamilisha ujenzi wa barabara ile waliongeza mita nane kufika 30 na yenyewe ikachukua madarasa na nyumba ya malimu, na kwa kuwa Mheshimiwa Waziri Mbarawa alifika akaiona ile hali na akatoa maelekezo kwa Mkurugenzi wa Halmashauri kutoa michoro pamoja na gharama na Mkurugenzi akafanya hivyo.

Napenda kujua sasa ni lini Serikali itatekeleza kupitia *TANROADS* ujenzi wa ile Shule ya Msingi Unkuku kwa sababu imeliwa sana na barabara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari niambatane naye pamoja na wataalam wake tukaione hii Shule ya Msingi Unkuku ilivyo katika mazingira hatarishi kwa watoto?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza kwa pamoja. Ni kweli kwamba Serikali ililipa fidia wakati huo barabara ikiwa na upana wa mita 22.5. Kama alivyosema kwa sababu mimi mwenyewe sijaenda, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Kondoa na Dodoma ni karibu, nataka nimuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaongozana, tutafute siku mimi pamoja na wataalam ili twende eneo la shule tukaangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, umetolewa mwongozo kwamba pale ambapo miundombinu ya shule, zahanati ama hospitali zinakuwa zimepitiwa na barabara kwa maana ya kuifuata, hatutakuwa tunatoa fidia badala yake tutakuwa tunajenga ile miundombinu yote iliyoathirika. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutakwenda na haya yote yatajibiwa ikiwa ni pamoja na kuona uwezekano kama kuna haja ya Serikali kujenga hiyo shule upya ama kutoa fidia, basi tutafanya hivyo baada ya kufika *site*, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante, tunaendelea.

Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mbunge wa Nsimbo, sasa aulize swali lake, kwa niaba yake Mheshimiwa Flatei Massay.

Na. 55

**Ujenzi wa barabara ya Kawajense – Ugalla – Kahama**

**MHE. FLATEI G. MASSAY K.n.y MHE. ANNA R. LUPEMBE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga barabara ya lami kutoka Kawajense – Ugalla hadi Kahama?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mbunge wa Nsimbo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeanza maandalizi kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa Barabara ya Kawajense ambapo ni Mpanda – Ugalla – Kaliua – Ulyankulu – Kahama yenye urefu wa kilomita 456 ambapo kazi ya upembuzi yakinifu imekamilika na kazi itakayofuata ni kufanya usanifu wa kina. Aidha, usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa Daraja la Ugalla pamoja na madaraja saidizi sita yaani *relief culverts* umekamilika na kazi ya ujenzi wa madaraja hayo imeanza na inatarajia kukamilika mwaka 2024. Kwa sasa Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Flatei Massay, swali la nyongeza.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili. Swali la kwanza; je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kuweka fedha kwenye bajeti ijayo ili Barabara hii ya Ugalla - Kahama ikawa kwenye bajeti kwa uhakika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; Barabara ya Dareda - Dongobesh aliiweka kwenye mpango wa kujengwa kwa kilomita

tisa na mpaka leo haijaanza kujengwa. Je, ni lini ujenzi wa barabara hiyo utaanza?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, barabara hiyo inanigusa, kwa hiyo naomba majibu. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara niliyoitaja kuna baadhi ya maeneo ambayo yalikuwa hayajafunguliwa, kwa hiyo kitu cha kwanza ni kuifungua yote na kuikamilisha. Pia tuliona kwanza tufanye usanifu uliokamilika kwenye Daraja kubwa la Mto Ugalla, lakini kabla ya kufika kwenye Daraja la Mto Ugalla kuna madaraja madogo sita ambayo tumeanza kuyajenga ili kulifikia hilo daraja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tutakapokamilisha ujenzi wa hayo ma-*culvert,* hatua ya pili itakuwa ni kujenga hilo daraja ili kuifungua barabara yote ambayo inaunganisha Mkoa wa Katavi – Tabora na Mkoa wa Shinyanga kwa upande wa Kahama. Kwa hiyo, tutakapokuwa tumekamilisha hii kazi sasa Serikali itaweka kwenye bajeti kuijenga barabara yote, lakini cha muhimu kwanza ni kukamilisha hayo madaraja ili kwanza tuifungue hiyo barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye swali lake la pili la Barabara ya Dareda – Dongobesh, ni kweli tulikuwa tumepata mkandarasi, lakini ikatokea tatizo la kimkataba ambalo sasa limeshatatuliwa na tunategemea kukamilisha manunuzi ya hiyo barabara. Baada ya hapo naamini barabara hiyo inaenda kujengwa kwa kiwango cha lami, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Mheshimiwa Rose Cyprian Tweve, swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Husna Sekiboko.

Na. 56

**Kubadili Mitaala ya Elimu**

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO K.n.y. MHE. ROSE C. TWEVE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itabadili Mitaala ya Elimu ili kwenda na wakati?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Mheshimiwa Kipanga, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rose Cyprian Tweve, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekamilisha uandaaji na uidhinishaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, Toleo la mwaka 2023 na Mitaala katika ngazi ya Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Mafunzo ya Ualimu kwa lengo la kufanya elimu yetu iende na wakati. Mitaala iliyoboreshwa imezingatia mahitaji ya sasa ikiwa ni pamoja na kuweka msisitizo katika stadi za karne ya 21 ili kumjengea mhitimu stadi za Kuwasiliana, Kushirikiana, Ubunifu na fikra tunduizi. Aidha, ratiba ya utekelezaji wake inatarajiwa kuanza rasmi Mwezi Januari, 2024 na kukamilika mwaka 2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Elimu ya Kati na Elimu ya Juu, mapitio ya programu mbalimbali pia yanaendelea kwa lengo la kuifanya iende na wakati, vipaumbele vya nchi na mahitaji ya soko la ajira. Kwa mfano, kwa upande wa Elimu ya Juu kupitia Mradi wa *Higher Education for Economic Transformation (HEET)* programu zaidi ya 300 zitahuishwa au kuanzishwa, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Husna Sekiboko, swali la nyongeza.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kauli ya Serikali iliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu hapa Bungeni jana, suala hili limeeleweka vizuri na sina swali la nyongeza, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Wizara hiyo hiyo, Mheshimiwa *Engineer* Stella Martin Manyanya, Mbunge wa Nyasa, sasa aulize swali lake.

Na 57

**Ukosefu wa vipooza joto katika Ukumbi wa *VETA* - Nyasa**

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA** aliuliza:-

Je, kwa nini ukumbi wa *VETA* Nyasa haujawekwa vipooza joto?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa *Engineer* Stella Martin Manyanya, Mbunge wa Nyasa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeshafanya makadirio ya gharama za kufunga vipooza joto katika Chuo cha *VETA* cha Wilaya ya Nyasa ambapo katika Mwaka huu wa Fedha 2023/2024, Serikali imetenga kiasi cha shilingi milioni 20 kwa majengo yote. Kati ya fedha hizo shilingi milioni 7.5 zimetengwa kwa ajili ya kuwezesha kununua vifaa vitakavyofungwa katika ukumbi huo ili kuondoa changamoto ya joto kali, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mhandisi Stella, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Naibu

Waziri kwa majibu yenye matumaini makubwa, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa chuo cha *VETA,* Nyasa wakati huo kilikuwa na changamoto kubwa ya ulipaji wa fidia na kwa sababu kipo maeneo ambayo ni ya kimkakati, kwa hiyo eneo lake ni dogo kiasi kwamba uendelezaji wa chuo hicho unakuwa mgumu kwa hatua zinazofuata. Hakuna kiwanja cha mpira, lakini pia kwa fani nyingine kama za utalii ni ngumu kuendeleza hapo. Je, serikali ina mpango gani wa kuweza kuongeza eneo la chuo hicho?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; naomba kwa kuwa Wizara ni hiyo hiyo moja kupitia mradi wa *EP4R,* Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilijenga jengo la utawala na maktaba ya ghorofa katika Shule ya Sekondari Mbamba Bay ambayo kila siku nalisemea hilo jengo.

Je, ni lini jengo hili litaweza kukamilika na ikibidi Mheshimiwa Waziri sasa ifikie mahali wakatembelee wakaone hali halisi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Manyanya, Mbunge wa Nyasa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na suala la eneo la chuo chetu cha *VETA* kuwa dogo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge mimi pamoja na timu yangu ya wataalam wa *VETA* tutafanya ziara katika chuo hicho ili kujiridhisha na ukubwa wa hilo eneo. Kama kutakuwa na uhitaji wa kuongeza eneo, nimwondoe hofu, tulishalifanya jambo hilo katika Chuo chetu cha Kipawa ambacho kilikuwa na eneo dogo, tumeweza kuongeza eneo, basi na hapa katika Chuo chetu hiki cha *VETA* tutafanya ziara lakini vilevile tutahakikisha kwamba kama kutakuwa na eneo linahitajika kuongeza, Serikali itaweza kuongeza eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali la pili katika shule hiyo aliyoitaja ya Sekondari ya Mbambabay kwamba Serikali ilishapeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu. Pia, kuna hili jengo la utawala ambalo halijakamilika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Wizara yangu kwa kushirikiana na wenzetu wa TAMISEMI, tutafanya ziara katika eneo hilo. Vilevile, tumuagize Mkurugenzi wa Halmashauri ya Nyasa kuweza kufanya tathmini ya jengo hilo, kuona ni kiasi gani cha fedha kinahitajika ili basi Serikali iweze kupata tathmini hiyo na kuweza kuifanyia kazi ili jengo hili liweze kukamilika, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Uchukuzi. Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha Ng'anzi Ulenge, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 58

**Mkakati wa kufanya Bandari ya Tanga kuwa ya ufanisi**

**MHE. *ENG*. MWANAISHA N. ULENGA** aliuliza:-

Je, nini Mkakati wa Serikali wa kuifanya Bandari ya Tanga iwe na ufanisi zaidi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa David Kihenzile, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwanaisha Ng'anzi Ulenge, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu sasa Bandari ya Tanga ilikuwa haihudumii meli na shehena ya kutosha kutokana na changamoto ya kasi ndogo ya huduma za meli na shehena hizo ambazo zilipaswa kuhudumiwa nangani umbali wa kilomita 1.7 kutoka gatini. Hali hii ilipunguza kwa kiasi kikubwa uwezo wa Bandari ya Tanga na ushindani wa bandari hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Serikali kupitia *TPA,* inaendelea na maboresho ya bandari hiyo katika maeneo ya miundombinu, mitambo na vifaa ili kuvutia meli na shehena nyingi zaidi kama mkakati mahsusi wa kuifanya bandari hiyo ifanye kazi kwa ushindani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada hizo *TPA* ina mkakati mahsusi wa kimasoko kwa ajili ya Bandari ya Tanga ambao lengo lake ni kuteka soko la kaskazini mwa Tanzania na nchi jirani za Rwanda, Burundi, Uganda na *DRC*. Mikakati hiyo ni pamoja na kuwashawishi wateja wakubwa kutumia bandari hiyo kwa kutoa punguzo la tozo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanaisha, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bandari ya Tanga ilifanya vizuri sana miaka ya 1980 na sababu kubwa ilikuliwa ni uwepo wa viwanda vingi ambavyo asilimia 90 sasa vimeshakufa. Kwa kuwa, meli kubwa na nyingi haziwezi kwenda mahali ambako zitapeleka tu mzigo bila kuchukua, yaani ile *exchange of containers* hakuna meli kubwa ambayo itakwenda bila kukutana na hali hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, tunamini kabisa bandari ndiyo uti wa mgongo wa Taifa hili; Je, Wizara hii ya Uchukuzi haioni haja ya kushirikiana kwa karibu na Wizara zingine kuhakikisha kwamba meli kubwa zinakuja kwa kufufua viwanda ambavyo Tanga vimekufa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, Bandari ya Mwambani ilipangwa kuendeshwa kwa ubia lakini kikwazo ilikuwa ni Sheria ya Ubia ambayo sasa imekwishafanyiwa marekebisho. Sasa Serikali itueleze wazi, mpaka sasa imeshachukua hatua gani kuhakikisha mpango ule wa kuendesha Bandari ya Mwambani kwa ubia unatekelezeka?

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Eng. Mwanaisha kwa kazi yake kubwa anayofanya ya kufuatilia mchakato wa miundombinu katika Mkoa wa Tanga. Serikali imeshaanza kufanya mambo mengi katika eneo hilo, mojawapo ni ukarabati wa hiyo Bandari ya Tanga lakini pia uwepo wa fursa kama bomba la mafuta ni hatua muhimu kwenye kuelekea Tanga kuwa eneo muhimu sana la kiuwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ameuliza kama je, tuko tayari kushirikiana na Wizara nyingine, ni kweli, tuko tayari kushirikiana na sekta nyingine ikiwemo Wizara ya Viwanda na Biashara kuhakikisha kwamba viwanda vilivyokuwa vimefungwa na vimefanya vizuri miaka ya 1990 na huko nyuma vinafufuliwa ili angalau bandari hiyo iweze kupata mizigo. Mojawapo ya mambo ambayo tunayafanya ni pamoja na kufufua pia uwanja wa ndege wa Tanga ili ndege kubwa na za kati ziweze pengine kuanza kutumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili ameuliza kuhusu Bandari ya Mwambani, kwenye mpango wetu mkakati wa mwaka 2045 hiyo ni moja kati ya maeneo ambayo tunatazama kwa jicho la karibu zaidi. Kwa sasa hivi, moja tumeshakamilisha mabadiliko ya sheria ya *PPP* na hivyo tunakaribisha mtu yeyote anayetaka kuja kushirikiana nasi katika kuendeleza bandari hiyo ili kwa pamoja tuweze kuhakikisha kwamba Bandari ya Mwambani inafanya vizuri zaidi. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Asante. Mheshimiwa Prof. Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi, Mbunge wa Kilosa, sasa aulize swali lake.

Na. 59

**Kukarabati na kufufua reli kutoka Kilosa – Kidatu**

**MHE. PROF. PALAMAGAMBA J. A. M. KABUDI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itakarabati na kufufua reli kutoka Kilosa hadi Kidatu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Prof. Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi, Mbunge wa Kilosa, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa vipindi tofauti imeendelea kuimarisha huduma za usafiri na usafirishaji katika maeneo mbalimbali nchini. Kuhusu ufufuaji wa reli kutoka Kilosa hadi Kidatu, Serikali kupitia *TRC* katika bajeti ya mwaka wa fedha 2023/2024 imetenga jumla ya shilingi bilioni 3.4 kwa ajili ya kuanza kazi za awali za marekebisho na ufufuaji wa njia katika kipande hiki chenye urefu wa kilomita 108 ambayo imefungwa kwa muda mrefu zaidi. Reli hii inaunganisha Reli ya Kati na *TAZARA* eneo la Kidatu. Aidha, kwa sasa *TRC* imekamilisha tathmini ya kihandisi ikiwemo makadirio ya gharama ya mradi *(Engineering estimates)* na inaendelea na ukamilishaji wa nyaraka za zabuni kwa ajili ya kumwajiri Mkandarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutumia fursa hii kumuomba Mheshimwa Prof. Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi - Mbunge, pamoja na wananchi wa Kilosa kuwa na subira wakati Serikali inaendelea na juhudi ya urejeshwaji wa njia hii ambayo ni muhimu kwa ajili ya usafirishaji wa mizigo na abiria. Lengo la Serikali ni kuendelea kufanya maboresho katika maeneo yenye mahitaji ili wananchi waweze kuendelea kupata huduma za usafiri na usafirishaji.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Profesa Palamagamba, swali la nyongeza.

**MHE. PROF. PALAMAGAMBA J. A. M. KABUDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ambayo yanatia moyo wa

kuanza kufufuliwa kwa reli hii muhimu kwa uchumi wa Tanzania. Nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Moja, ningependa kujua ni lini hasa mchakato wote huu utakamilika *(time-frame)* ili wananchi wa Kilosa lakini Wananchi wa Mikumi na wananchi wa Kilombero wajue ni lini reli hii itaanza kukarabatiwa?

Swali langu la Pili la nyongeza; kwa kuzingatia kwamba Mji wa Kilosa sasa utaunganisha reli tatu, yaani reli ya sasa ya *MGR*, reli ya *SGR* na kwa sababu kutoka Kilosa mpaka Kidatu inaanza reli ya *TAZARA* Kidatu mpaka Mlimba. Maana yake sasa Mji wa Kilosa utaunganisha reli tatu.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuifanya sasa Kilosa kuwa ndiyo *logistic hub* kubwa katika nchi yetu inayounganisha reli hizi tatu, ukichukua reli ya *TAZARA* ina uwezo mpaka wa kufika Zimbabwe, Zambia, Afrika ya Kusini na Namibia ili mizigo katika reli hizi iweze kuhamishwa na makontena kwa urahisi katika Mji wa Kilosa ambao sasa una stesheni kubwa mbili ya *MGR* na *SGR* na uwezo wa kuungana na reli ya *TAZARA*. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Profesa kwa sababu swali lake linagusa sehemu kubwa sana ya maeneo ya Mashariki na Kati mwa Tanzania. Kwa kuwa reli hii ilikuwa ni muhimu sana miaka ya nyuma kwa nchi za *SADC* kuanzia nchi za *South Africa* mpaka Uganda, Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Jemedari Dkt. Samia Suluhu Hassan inao mkakati madhubuti wa kufanyia kazi jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ameuliza ni lini, jibu ni Mwaka huu wa Fedha 2023/2024, tumekwishaanza mchakato wa kimanunuzi na pengine ifikapo mwezi Februari tayari tutakuwa kwenye hatua kubwa zaidi.

Swali la pili anauliza ni upi mkakati wa Serikali wa kuifanya Kilosa kuwa *logistic hub*, kwa sababu tayari reli ya *MGR*, *SGR* na

*TAZARA* zinaungana, kwanza nataka kumhakikishie kupitia *SGR* na *MGR*, tutajenga kituo kikubwa cha mizigo katika eneo hilo la Kilosa na tayari tumeshaanza upembuzi yakinifu katika kuhakikisha tunatimiza jambo hilo na hivyo kuifanya Kilosa kuwa ni *Logistic hub* kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge ameuliza hapo awali kwenye swali lake la nyongeza.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge.

Tuendelee Wizara ya Mendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum. Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda, Mbunge wa Newala Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 60

**Utoaji wa huduma za afya kwa wazee bila malipo**

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA** aliuliza: -

Je, kuna mkakati gani wa kuhakikisha wazee zaidi ya miaka 60 wanaostahili kupata huduma za afya bila malipo wanapata huduma hizo?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda, Mbunge Newala Vijijini, kuhusu za afya bila malipo kwa wazee wa miaka 60 na kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi cha Julai, 2022 mpaka Juni, 2023, jumla ya watu milioni 2.2 wakiwemo wanaume milioni 1.3 na wanawake 735,169 wametambuliwa kuwa ni wazee wa miaka 60 na kuendelea katika Mikoa yote 26 ya Tanzania Bara. Kati ya hao, Wazee 585,672 sawa na asilimia 27.65 walithibitishwa kutokuwa na uwezo wa kugharamia huduma za matibabu hivyo Serikali imewapatiwa vitambulisho vya bima ya afya iliyoboreshwa *(ICHF)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kufanya utambuzi wa Wazee wasio na uwezo katika Halmashauri zote nchini ili kuhakikisha wanapata huduma za matibabu zilizolipiwa gharama na Serikali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maimuna, swali la nyongeza.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza naipongeza Serikali kwa kufanya zoezi la kuhakiki na kubaini wazee hao ambao hawana uwezo. Pia, pamoja na kuwabaini, Serikali ikawapatia vitambulisho vya *ICHF* kwa ajili ya kupata matibabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto iliyopo ni kwamba pamoja na kupewa hivyo vitambulisho, wakienda kwenye maeneo ya kupata huduma za afya wanaishia kutangatanga kwa sababu hawapati dawa.

Je, Serikali imejipangaje kuhakikisha kwamba wazee hawa sasa watapata dawa bila matatizo?

Swali la pili; huko nyuma kulikuwa na *slogan* ilikuwa inasema" Mpishe Mzee Kwanza" sasa hivi *slogan* hiyo imeanza kupotea, wazee wanahangaika, wakienda kupata huduma sehemu nyingine hata hospitali na maeneo mengine, hakuna anayejali.

Ni upi mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba tunarudi kwenye mkakati ule wa mwanzo wa kuhakikisha wazee wanapishwa ili kupata huduma kwanza ili wakaendelee na mambo yao mengine? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hawa wazee kwenda kwenye vituo vya huduma za afya pamoja na vitambulisho vyao wanakuwa hawapati huduma, tutafanya ufuatiliaji kwa sababu huenda wako watu ambao hawawathamini wazee hawa waliotambuliwa kuwa hawana uwezo kwa mujibu wa mwongozo uliowekwa na Wizara Mama ya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, tutashirikiana na Mabaraza ya Wazee yaliyopo nchini kote ili kufuatilia na kupata maoni ya wazee hawa wasiopata hizo huduma ni kwenye maeneo gani hasa, kwa sababu vipo vituo vya afya vingine vinafanya vizuri sana. Huenda ni baadhi ya maeneo ambayo tutayafuatilia tuyaibue na tushirikiane na Mheshimiwa Waziri wa Afya kuchukua hatua stahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala hili la kampeni ya "Mpishe Mzee, Mzee ni Tunu Apate Huduma", kama kuna mahala pameanza kusinzia pia tutafanya ufuatiliaji maana kampeni hii ni endelevu na tuliianzisha mwaka 2021 na imeendelea vizuri mwaka 2022. Sasa kama kuna mahala panalegalega, napeleka tu salamu kwa wale wanaotakiwa kufanya kazi hiyo wakiwemo Maafisa Ustawi wa Jamii wakishirikiana na Wakuu wa Vituo kupitia Waziri mwenye dhamana ya afya, tutafanya ufuatiliaji ili kuiinua tena kampeni hiyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea Wizara ya Afya, Mheshimiwa Martha Nehemia Gwau, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake. Mheshimiwa Massare, kwa niaba yake.

Na. 61

**Watoto wachanga kutumia Bima za Afya za mama zao**

**MHE. YAHAYA O. MASSARE K.n.y. MHE. MARTHA N. GWAU** aliuliza: -

Je, Serikali haioni kuna haja ya watoto wachanga kutumia Bima za Afya za Mama zao?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Martha Nehemia Gwau, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kumekuwa kukitokea changamoto kwa wazazi wenye bima wanaojifungua watoto wao kushindwa kupata huduma hasa kwenye vituo vya huduma za afya vya sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Afya alishatoa maelekezo kwa Mtendaji Mkuu wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kuhakikisha watoto wachanga wenye uhitaji wa huduma wanapata huduma za afya bila kikwazo chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutumia fursa hii kuelekeza Watendaji wa Mfuko wa Bima ya Afya na vituo vyote vya huduma za afya nchini kuhakikisha watoto wanapata huduma kwani Mama yupo na kadi yake inayoonesha ushahidi wote kuhusu mtoto husika na ni mtoto wa ngapi kwenye familia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaasa wazazi na viongozi wa hospitali husika kukomesha kabisa matukio ya kughushi nyaraka ambayo pia ndiyo yanapelekea kuwepo na usumbufu wakati mwingine. Naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yahaya Massare, swali la nyongeza.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni juzi tu tumepitia Sheria ya Bima ya Afya, je, katika sheria hii, ita-*consider* mtoto ambaye anazaliwa kwa kadi ya mama yake kutumia angalau kwa miezi mitatu

wakati wazazi wanajipanga kumtengenezea bima huyu mtoto aliyezaliwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili; Serikali ilishawahi kutoa tamko kama hili kwamba imeelekeza hospitali, wazazi wanapojifungua watumie bima za mama zao lakini hili halifanyiki. Nini kauli nyingine ya Serikali kwa sababu jambo hili linajirudia, Serikali inasemaje katika hili?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba kujibu maswali mawili mazuri ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Moja; anasema je, sheria iliyopo sasa ambayo tulipitisha juzi kwamba inaenda ku-*accommodate*, labda nisisitize tu, kwamba siyo tu sheria tuliyoipitisha juzi kuanzia sasa ni kwamba, watoto wanaozaliwa hospitali ambao wazazi wao wana kadi zao za bima, watibiwe na wapate huduma kwa sababu ambazo nimezielezea hapa inawezekana ku-*track* vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, akaseme je, tunafanya nini kuhusu ambao sasa wanakwenda kwenye vituo vyetu na tayari tulitoa tamko lakini bado hayo matatizo yanaendelea. Waheshimiwa Wabunge wenzangu ninawaomba pia nawaasa Watanzania wenzangu na ninawaasa Watumishi wa Mfuko wa Bima ya Afya na hospitali zote Tanzania kwamba sasa hivi tukisikia hilo na likitokea na Mheshimiwa Mbunge ukikutana na kitu kama hicho naomba utuletee na mtu huyo ambae amesababisha hayo atachukuliwa hatua mara moja palepale. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu.

Tunaendelea Wizara ya Maji. Mheshimiwa Vincent Paul Mbogo, Mbunge wa Nkasi Kusini, sasa aulize swali lake.

Na. 62

**Mradi wa maji Kata za Nkasi Kusini**

**MHE. VINCENT P. MBOGO** aliuliza: -

Je, lini Serikali itapeleka mradi wa maji katika Kata za Kizumbi na Wampembe – Nkasi Kusini ?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Mhandisi Maryprisca Mahundi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri ya Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Vincent Paul Mbogo, Mbunge wa Jimbo la Nkasi Kusini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali katika mwaka wa fedha 2022/2023, imekamilisha usanifu wa Mradi wa Maji Wampembe utakaohudumia Kata mbili za Kizumbi na Wampembe. Utekelezaji wa mradi huo unatarajiwa kuanza mwezi Januari, 2024 na kukamilika mwezi Desemba, 2024 ambapo utanufaisha wananchi wapatao 15,089 waishio kwenye vijiji sita vya Wampembe, Mwinzana, Kizumbi, Lyapinda, Ng'anga na Katenge.

Mheshimwa Mwenyekiti, mradi huo unatarajiwa kutekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na Shirika lisilo la Kiserikali la *USAID* kupitia Mradi wa Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira (MUM), ambapo baadhi ya miundombinu inayotarajiwa kujengwa ni pamoja na matenki Manne (4) ya kuhifadhia maji yenye jumla ya lita 405,000, ujenzi wa vituo 39 vya kutolea huduma kwa wananchi sambamba na mtandao wa bomba kuu na mabomba ya usambazaji umbali wa Kilometa 41.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Vincent Mbogo, swali la nyongeza.

**MHE. VINCENT P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi kuweza kuuliza swali nyonyeza, nina maswali mawili.

Makao Makuu ya Wilaya ya Nkasi yana changamoto kubwa sana ya maji, ni nini mpango wa kutoa maji Ziwa Tanganyika ambao unaanzia Kata ya Wampembe kupeleka maji Wilayani Nkasi ?

Swali la Pili, Vijiji vya Mwinza, Diela, Katenge, Lupata, Lyapinda, Kasanga Ndogo, Katenge, Msamba, wananchi wanaliwa na Mamba wanapofuata huduma ya maji. Je, ni lini kama Wizara mtakaa na Wizara ya Maliasili ili muainishe maeneno yale ambayo wananchi wanapata huduma ya maji muwawekee wavu ili wananchi wasiliendelee kuliwa na mamba? Kwani ndani ya mwaka mmoja wameliwa watu Kumi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya Ziwa Tanganyika kupeleka maji Makao Makuu ya Wilaya. Kwanza nampongeza Mheshimiwa Mbunge, umefuatilia sana na tayari Wizara tunaendelea na taratibu za kuona kwamba Ziwa Tanganyika tunaweza kuleta maji pale na maji yawe ya uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la wananchi kuliwa na mamba. Mheshimiwa Mbunge nakupa pole sana kwa wananchi kupata hii kadhia, tutalichukulia kwa umakini mkubwa kuhakikisha kwamba tunakutana na wenzetu wa Maliasili basi tuje tuweke hiyo mipaka ya kuhakikisha wananchi wanachota maji maeneo yenye usalama. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, nakushukuru sana kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea, Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Jacqueline Kainja Andrea, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Venant Daud Protas.

Na. 63

**Marekebisho ya Mahakama ya Wilaya ya Urambo**

**MHE. VENANT D. PROTAS K.n.y. MHE. JACQUELINE K. ANDREA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati Mahakama ya Wilaya ya Urambo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri Katiba na Sheria, Mheshimiwa Pauline Gekul, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jacqueline Kainja Andrea, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama ya Tanzania inaendelea kutekeleza mpango wa kuboresha majengo katika ngazi mbalimbali kwa kujenga majengo mapya na kukarabati baadhi ya majengo ya zamani. Aidha, katika mpango huu, jengo la Mahakama ya Wilaya ya Urambo limepangwa kufanyiwa ukarabati mkubwa mwaka wa fedha 2024/2025. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Venant, swali la nyongeza.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya kuendelea kuboresha mahakama zetu hapa nchini na hii itatusaidia hata ukienda kuhukumiwa kule uende vizuri vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina swali moja tu la nyongeza. Kwa kuwa Serikali ina mpango wa kujenga mahakama ikiwemo hiyo ya Urambo aliyojibu, lakini Halmashauri ya Wilaya ya Uyui

mpaka leo tunatumia majengo ya Mkuu wa Wilaya: Je, ni lini Halmashauri ya Wilaya ya Uyui nayo itajengewa Mahakama ya Wilaya? Nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Venant Daud, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mheshimiwa Venant Daud, Mbunge wa Uyui pamoja na Mheshimiwa Almas Maige, wamekuwa wakifatilia ujenzi wa mahakama katika Wilaya yao ya Uyui. Pia nampongeza Mheshimiwa *DC* kwa kutupatia ofisi yake na majengo ili kazi za mahakama ziendelee. Nimjulishe Mheshimiwa Venant kwamba tunajenga Mahakama ya Uyui mwaka huu wa fedha, na tayari utaratibu unaendelea kumpata mkandarasi.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge. Tuendelee na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Cosato David Chumi, Mbunge wa Mafinga Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 64

**Manufaa ya Taifa katika Ulinzi wa Amani**

**MHE. COSATO D. CHUMI** aliuliza:-

Je, Taifa linanufaika kiasi gani katika uuzaji wa bidhaa na huduma katika maeneo ambayo Jeshi letu linafanya ulinzi wa amani?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cosato David Chumi, Mbunge wa Mafinga Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania imekuwa mstari wa mbele kushiriki katika jitihada mbalimbali za kutafuta amani kama ilivyoainishwa katika Sera ya Mambo ya Nje ya mwaka 2001. Hivyo, ushiriki wa Tanzania katika Misheni za Ulinzi wa Amani umekuwa na manufaa mbalimbali ikiwemo walinda amani wetu kufaidika na mafunzo ya ziada ambayo yanawajenga na kuwaimarisha; pia ajira za kiraia kwa Watanzania na kudumisha utamaduni wetu kupitia kukua kwa lugha ya Kiswahili, kwani katika maeneo mengi ya *DRC*, Lebanon na Darfur, kumekuwa na ongezeko la matumizi ya Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na manufaa yaliyoainishwa, zipo fursa za kiuchumi zinazopatikana katika shughuli za ulinzi wa amani, ikiwa ni pamoja na biashara ya bidhaa zinazoweza kutumika katika vikosi vilivyopo katika misheni hizo, kama vile chakula, mavazi, vinywaji, vifaa tiba na madawa. Fursa nyingine ni usafirishaji wa mizigo, ujenzi wa majengo yanayohamishika, vifaa, huduma za TEHAMA na nyinginezo. Aidha, Tanzania inaweza pia kuuza teknolojia ya kutumia panya katika kubaini na kutegua mabomu ambayo yametegwa ardhini kama fursa za kiuchumi, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cosato, swali la nyongeza.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi na kwa majibu mazuri ya Serikali. Nitakuwa na swali moja la nyongeza. Kabla ya swali hilo napenda kutumia nafasi hii kuipongeza nchi yetu ya Tanzania kwa kuendelea kuwa kinara katika masuala ya ulinzi wa amani kama ambavyo tulikuwa kinara katika ukombozi wa Kusini Barani Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu ni moja; kwa sababu kuna hizo fursa, je, Wizara ipo tayari kuwa Wizara kiongozi kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara ili kuendelea

kung'amua fursa hizo kwa kushirikiana labda na *NBC* pamoja na *TPSF* kufanya kongamano ambalo linaweza likawasaidia wafanyabiashara wa Tanzania kung'amua hizo fursa na hivyo kunufaika kiuchumi kama Taifa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Serikali inatambua umuhimu wa kuwania fursa ambazo zinapatikana katika uendeshaji wa operesheni za ulinzi wa amani. Kwa kutambua hilo, mwezi Januari mwaka huu, 2023, Serikali iliandaa semina mahususi kwa wafanyabiashara kuhusiana na fursa zilizopo katika maeneo ya operesheni hizo. Lengo hasa la semina hiyo ilikuwa ni kuwapa elimu na kuwahamasisha wafanyabiashara wa Tanzania juu ya fursa mbalimbali ambazo zipo katika Operesheni za Ulinzi wa Amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba matunda ya semina hiyo tayari yameanza kuonekana, kwani hivi sasa wafanyabiashara wengi wa Tanzania wanachangamkia fursa hizo ambazo zipo katika Pperesheni za Ulinzi wa Amani katika sehemu mbalimbali, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu.

Tunaendelea na Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege Mbunge wa Kalambo, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Joseph Kakunda.

Na. 65

**Mkoa wa Rukwa kuunganishwa na Gridi ya Taifa ya Umeme**

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA K.n.y. MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE** aliuliza:-

Je, lini Mkoa wa Rukwa utaunganishwa na Gridi ya Taifa ya umeme?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Judith Kapinga majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati napenda kujibu swali la Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mbunge wa Kalambo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuunganisha Mkoa wa Rukwa na Gridi ya Taifa, Serikali inatekeleza Mradi wa Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovolt 400 kutoka Iringa hadi Sumbawanga kupitia Mbeya na Tunduma kwa Mradi wa *TAZA*, umbali wa kilomita 620. Mradi huu pia unahusisha ujenzi wa vituo vya kupooza umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa, Wakandarasi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wameshapatikana na Wakandarasi wa ujenzi wa vituo vya kupooza umeme wapo katika hatua za majadiliano. Mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi huu wa Novemba, 2023 na kukamilika mwezi Desemba, 2025, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Joseph Kakunda, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru sana Serikali kwa majibu mazuri, nami nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza: Je, ni mikoa mingapi hapa nchini hadi sasa haijaunganishwa na Gridi ya Taifa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili: Nafahamu kwamba Kigoma nayo ipo katika mpango wa kuunganishwa kwenye Gridi ya Taifa kupitia vituo vya Urambo na Ipole Sikonge. Sasa swali ni kwamba wananchi watalipwa lini fidia kwenye ile njia ya kutoka Tabora kwenda Ipole?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kakunda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na mikoa ambayo haijaunganishwa kwenye Gridi ya Taifa, mikoa miwili ya Katavi na Rukwa ndiyo ambayo haijaunganishwa kabisa kwenye Gridi ya Taifa. Mikoa ya Mtwara, Lindi, Kigoma na Kagera imeunganishwa kidogo kwa Msongo wa kilovolt 33, lakini miradi inaendelea ili tuiunganishe kwa Msongo Mkubwa wa Kilovolt 220 na Kilovolt 400. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na fidia ambayo ameuliza Mheshimiwa Mbunge, tayari tumeshafanyia kazi na tunategemea ifikapo tarehe 30 mwezi huu wa Novemba, 2023 wananchi wataanza kulipwa, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu hayo mazuri.

Waheshimiwa Wabunge, naomba tupunguze sauti kidogo ili tuweze kusikia majibu yetu toka Serikalini. Tunaendelea na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga, Mbunge wa Kilolo, sasa aulize swali lake.

Na. 66

**Ahadi ya JWTZ kujenga daraja la dharura**

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA** aliuliza:-

Je, lini Jeshi la Wananchi litatimiza ahadi yake ya kujenga daraja la dharura katika Mto Mtitu Kata ya Ihimbo?

**MWENYEKITI:** Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Mhandisi Masauni, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI K.n.y. WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga, Mbunge wa Kilolo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu ya kuendeleza na kusimamia barabara za vijijini na mijini ambayo awali yalikuwa yakitekelezwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa yamekabidhiwa kwa Wakala wa Barabara za Vijijini Tanzania *(TARURA)*. Hata hivyo, mwezi Julai, 2022 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ilipokea maombi ya kujengewa daraja la dharura katika Mto Mtitu, Kata ya Ihimbo kutoka Ofisi ya Mbunge wa Jimbo la Kilolo Mkoani Iringa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Jeshi la Wananchi wa Tanzania ilipeleka kikundi cha Wahandisi wa Medani ambacho kilifanya uchambuzi wa madaraja ya chuma yaliyopo na kubaini kuwa lipo daraja la JWTZ la *Bailey Bridge* lililopo yadi za *TARURA* mkoani Mbeya ambalo lingefaa kujengwa katika eneo husika. Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo inashauriwa kukamilisha ujenzi wa barabara ya vumbi yenye uwezo wa kupitisha magari ya tani 20 pamoja na uimarishaji wa eneo jipya la ujenzi wa daraja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutatua changamoto ya kukosekana kwa mawasiliano baina ya wananchi wa Kata ya Ihimbo na maeneo mengine, Wizara inapendekeza kukutana na Mheshimiwa Mbunge pamoja na Ofisi ya *TARURA* Wilaya ya Kilolo ili kutatua changamoto hiyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lazaro, swali la nyongeza.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali. Sasa nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, kwa kuwa tayari daraja lipo kule Mbeya; na kwa kuwa Wizara tayari ilishabaini mahitaji kwamba kuna mahitaji ya daraja hilo.

Je, ni lini tutafanya hicho kikao na Wizara ya Ulinzi kwa sababu sisi Kilolo tuko tayari ili utekelezaji uanze kufanyika? Hilo ni swali la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; je, Serikali haioni umuhimu wa kufanya haraka kwa sababu kipindi cha msimu wa mvua ambacho ndiyo huwa kina matatizo makubwa kimekaribia na ikiwa tutachelewa, madhara makubwa yanaweza kutokea, kwa sababu kila mwaka tunapoteza watu kama hatutaweza kujenga hilo daraja?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI K.n.y. WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Nyamoga, Mbunge wa Kilolo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge juu ya umuhimu na uharaka wa ujenzi wa daraja hili, lakini nampongeza pia kwa utayari wake. Kama nilivyomjibu katika swali la msingi kwamba Wizara iko tayari kukutana naye pamoja na *TARURA*, hivyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge baada ya kikao hiki niweze kukutananaye na pale ambapo atakuja Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, nimfikishie ujumbe huu waweze kufanya kikao hicho kwa haraka na suala hilo liweze kupatiwa ufumbuzi.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, tunakushukuru kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Justina Arcadius Rahhi, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 67

**Utambuzi wa mifugo nchini**

**MHE. YUSTINA A. RAHHI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa utambuzi wa mifugo baada ya kusitisha zoezi la utambuzi kwa kutumia hereni za mifugo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mheshimiwa Alexander Mnyeti majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi Novemba, 2022 Serikali ilisitisha kwa muda zoezi la utambuzi wa mifugo kwa njia ya hereni ili kurekebisha kasoro zilizojitokeza ambazo ni pamoja na wafugaji kulalamika juu ya bei ya kuvisha hereni na baadhi ya wafugaji kukosa elimu sahihi ya utambuzi wa mifugo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imekamilisha kufanya marekebisho ya kasoro la zoezi hilo la utambuzi zilizojitokeza ambapo bei ya kuvika hereni imeshuka kutoka 1,750 hadi shilingi 1,550 kwa ng'ombe na kutoka shilingi 1,000 kwa mbuzi na kondoo hadi shilingi 900. Pia, Wizara imekamilisha kuandaa mkakati wa utoaji elimu kwa wafugaji kuhusu umuhimu wa utambuzi wa mifugo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara kwa kushirikiana na wadau wa mifugo, inategemea kuanza awamu ya pili ya utambuzi wa mifugo kwa kuanza na mashamba makubwa ya mifugo ya Serikali, mashirika, watu binafsi, wawekezaji kwenye vitalu vya *NARCO*, vituo vya unenepeshaji ng'ombe wa maziwa, wafugaji wakubwa na wafugaji watakaokuwa tayari wakati wa zoezi hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yustina, swali la nyongeza.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza. Kwanza ni kweli Serikali ilisitisha zoezi hili la utambuzi wa mifugo kwa kutumia hereni za kieletroniki mwaka jana 2022, Novemba tarehe kama hii, ili kuipa Wizara kufanya tathmini ya

upungufu. Kutokana na umuhimu wa zoezi la utambuzi wa mifugo ambacho ndicho kinachoweza kuondoa migogoro kati ya wafugaji, na kusababisha mifugo kuhamahama na kuingiliana pamoja na wizi wa mifugo; changamoto ambayo iko kwa wafugaji wadogo zaidi kuliko wa mashamba makubwa, ambapo ufugaji kule uko salama na idadi yake inafahamika: Ni lini sasa Serikali itafanya zoezi hili kwa wafugaji wa kawaida na wadogo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, kuna changamoto ya takwimu ya uhakika ya mifugo. Ni lini Serikali itafanya sensa ya mifugo ili tuwe na takwimu halisi ya mifugo katika nchi yetu? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, kwanza nianze na hili la hereni kwamba ni kweli Serikali ilisitisha na sasa mwaka mmoja umepita. Serikali imesitisha baada ya zoezi hili kulalamikiwa sana na wadau, hasa wafugaji wadogo wadogo. Sasa Serikali ilichokifanya ni kuainisha changamoto zile ambazo wafugaji wanazilalamikia na kutafuta majawabu sahihi. Baada ya kupata hayo majawabu sahihi, na kwa kuwa zoezi hili lilizuiliwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu, tulichokifanya Wizara ni kumwandikia Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba sasa tunashughulikia changamoto zote ambazo wafugaji wameziainisha, kwamba majibu yake sasa tayari tunayo na Mheshimiwa Waziri Mkuu tayari amesharuhusu tuendelee na zoezi hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nikuhakikishie kwamba zoezi hili litaanza mara moja, hivi punde kadiri ambavyo maelekezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu yalivyotolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili amelisema hapa kuhusu sensa. Ni kweli kwamba sensa hii huwa inafanyika kila baada ya miaka mwili. Sensa ya mwisho ilifanyika mwaka wa fedha 1920 na mwaka huu sasa tutafanya sensa 2023 kwa ajili ya kubaini idadi halisi ya mifugo tuliyonayo katika Taifa letu. Sensa hii tunashirikiana na watu wa *NBS*, wanaoshughulika na masuala ya

takwimu kuhakikisha kwamba takwimu tunazozipata zinalenga kwenye kuleta tija katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Emmanuel Lekshon Shangai, Mbunge wa Ngorongoro, sasa aulize swali lake.

Na. 68

**Kutoza faini mifugo iingiapo hifadhini**

**MHE. EMANNUEL L. SHANGAI** aliuliza:-

Je ni sheria ipi inawaruhusu Watumishi wa *TANAPA*, *TAWA* na *NCAA* kutoza mifugo shilingi 100,000 pindi iingiapo hifadhini?

**MWENYEKITI:** Naibu Waziri Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Luka Kitandula, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Emannuel Lekshon Shangai, Mbunge wa Jimbo la Ngorongoro, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi za Uhifadhi za *TANAPA*, *NCAA* na *TAWA* zinaongozwa na Sheria mahususi za kusimamia rasilimali za wanyamapori. Mathalan, Sheria ya *TANAPA* Sura 282 Kifungu cha 28(1)(a) kama kilivyorekebishwa na Sheria ya Marekebisho Mbalimbali (Na. 11) ya mwaka 2003 ambayo imeongeza kifungu 20A cha Sheria hiyo kwa kuwapa mamlaka watumishi wa *TANAPA* kutoza faini isiyozidi shilingi 100,000 kwa kila kosa pale mkosaji anapokiri na kukubali kwa maandishi kulipa faini kwa kosa husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 116 cha Sheria ya Uhifadhi Wanyamapori, Sura ya 283 hutumika katika kutoza faini

pindi mifugo inapoingizwa kinyume cha sheria, ndani ya mapori ya akiba. Kifungu hiki kimebainisha utaratibu wa kulipa faini ambapo mkosaji atalipa faini mara baada ya kukubali na kukiri kosa. Aidha, sheria imeelekeza kuwa kiwango cha faini hakitapungua shilingi 200,000 na hakitazidi shilingi 10,000,000. Mkosaji hukiri kosa kwa maandishi na kulipa faini hiyo, na endapo hatakuwa tayari kulipa faini, hufikishwa Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Wananchi kwa ujumla kuwa Serikali itaendelea kuhifadhi na kusimamia rasilimali za wanyamapori kwa kushirikiana na jamii. Hivyo, tunawaomba wote watoe ushirikiano katika kufanikisha jukumu hilo na kuwasihi wazingatie sheria ili kuepusha migongano isiyo ya lazima baina yao na Wahifadhi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Emmanuel Lekshon Shangai, swali la nyongeza.

**MHE. EMANNUEL L. SHANGAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Nashukuru kwamba, ameshindwa kuthibitisha kwamba mifugo inatakiwa kutozwa shilingi 100,000 kwa kichwa cha ng’ombe wanapoingia hifadhini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wafugaji wengi Tanzania wamekuwa wakitozwa shilingi laki moja kwa kichwa cha ng’ombe wanapoingia hifadhini na kuna wananchi wametozwa mpaka shilingi milioni sabini kwa wakati mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali langu la kwanza nini kauli ya Serikali kwa Watumishi wa *TANAPA, TAWA* pamoja na *NCAA* ambao wamekuwa wakitoza shilingi laki moja kwa kichwa cha ng’ombe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili je, Serikali ipo tayari kurejesha fedha za wananchi ambazo wametozwa zaidi ya shilingi milioni kumi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Shangai kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jibu langu la msingi nimeonyesha sheria inataka nini? Lakini sambamba na eneo hilo niseme tu kwamba, kosa la kuingiza mifugo kwa mujibu wa Sheria ya Hifadhi ya Taifa lipo pia katika Kanuni Na. 7(1) ya Kanuni za Hifadhi ya Taifa *GN* Na. 255 ya mwaka 1970 kama ilivyorekebishwa ambavyo Kifungu kinazuia kuingiza mifugo Hifadhini na adhabu ya kosa kuingiza mifugo ni kwa kila mfugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nchi yetu, Serikali yetu ina heshimu Utawala wa Sheria na chombo ambacho kimekasimiwa kutafsiri sheria pale ambapo kuna changamoto ni Mahakama zetu. Nitoe rai kwamba wale wote wanaoona kwamba imepita hukumu ambayo wanaona haikuwatendea haki basi twende kwenye mfumo wa kisheria ili sheria iweze kutoa haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hili la kurejesha bado narudi pale pale yeyote anayehisi kwamba hakutendewa haki tuzitumie Mahakama zetu ili haki iweze kutendeka. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge, tunakushukuru sana.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali na majibu, ninayo matangazo hapa. Tangazo la kwanza ni wageni waliopo Bungeni asubuhi hii.

Kwanza ni wageni waliokaa Jukwaa la Spika, wageni wawili wa Mheshimiwa Naibu Spika ambao ni Balozi Dkt. Ramadhani Kitwana Dau ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya Utalii Tanzania *(TTB)* ambaye ameambatana na Ndugu Ghifari Al Moukhar kutoka Malaysia, ahsante sana karibu. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Jerry Silaa, Mbunge ambaye ni Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kutoka Dar es salaam Ndugu Omary Kimbau na Ndugu Rahim Dossa, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wa Waheshimiwa Wabunge, tuna wageni 36 wa Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda, Mbunge ambaye ni Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Wajumbe wa Kata ya Mahida, Mamsera na Chala na viongozi kutoka Ofisi ya Mbunge kutoka Jimbo la Rombo, Mkoani Kilimanjaro, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa ambaye Naibu Waziri wa Madini kutoka Chama cha Ma-*broker* Tanzania (CHAMMATA), karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 21 wa Mheshimiwa Hamis Mwinjuma, Mbunge na Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo ambao ni *Muheza Jogging and Sports Club* kutoka Muheza Mkoa wa Tanga, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 59 wa Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, Mbunge ambao ni wanafunzi wenzake waliosoma *SAUT* mwaka 2010 kutoka sehemu mbalimbali hapa nchini, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Muharami Mkenge ambao ni viongozi kutoka Kata ya Nianjema Bagamoyo, Mkoa wa Pwani, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni 32 wa Mheshimiwa Japhet Hasunga, Mbunge ambao ni Wanakwaya ya Moravian kutoka Vwawa, Mkoa wa Songwe wakiongozwa na Mchungaji Mkondya na Hellen Mwashiuya, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni watano wa Mheshimiwa Maimuna Pathan, Mbunge ambao ni watoto na wajukuu zake kutoka Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, Mbunge ambaye ni mpiga kura wake kutoka Nyang’hwale, Mkoa wa Geita, Ndugu Juma Ntambi, ahsante na karibu sana. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Vedastus Manyinyi, Mbunge ambao ni wapiga kura wake kutoka Mkoa wa Mara, ahsante karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Ravia Idarus Faina, Mbunge ambao ni viongozi wa Wadi ya Kiongoni kutoka Makunduchi Kusini, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; wapo wageni 20 kutoka *Kimara Wazazi SACCOS,* ahsante karibuni. *(Makofi)*

Wapo wanafunzi 29 kutoka *Dodoma Institute of Development and Entrepreneurships Studies,* karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wanafunzi watano wa Chuo cha Habari *(Dodoma Media)* kutoka Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, lipo tangazo kutoka kwa Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club* anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kuwa kesho siku ya Jumamosi tarehe 4 Novemba, 2023 kuanzia saa kumi jioni kutakuwa na mchezo wa kirafiki wa mpira wa miguu kati ya timu ya *Mati Super Brands Limited* kutoka Karatu na timu ya Waheshimiwa Wabunge. Mchezo huo utachezwa katika Uwanja wa Kilimani, Wabunge wote mnakaribishwa kuhudhuria katika mchezo huo muhimu.

Waheshimiwa Wabunge, lipo tangazo kutoka kwa Katibu wa Bunge; Katibu wa Bunge anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kuwa Ofisi ya Bunge imepata msiba wa mtumishi wake Ndugu Ramadhani Katabazi Shabani ambaye ni Afisa Ugavi Mwandamizi wa Kitengo cha Menejimenti ya Ununuzi na Ugavi, aliyefariki dunia tarehe 2 Novemba, 2023 katika Hospitali ya Agha Khan, Jijini Dar es Salaam.

Aidha, ofisi inaendelea kuwasiliana na familia ya marehemu kuhusu taratibu za mazishi. Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi, amina.

**WABUNGE FULANI:** Amina.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo haya, sasa naomba nimuite Mheshimiwa Waziri wa

Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Jenista Joakimu Mhagama kwa ajili ya kutoa hoja ya kutengua Kanuni za Bunge, Mheshimiwa Waziri, karibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba nilete maelezo ya hoja ya kutengua Kanuni za Bunge. Ninafanya hivi chini ya Kanuni ya 174(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari Mwaka 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mkutano wa 13 wa Bunge ulioanza tarehe 31 Oktoba, 2023 umepangwa kumaliza kazi zake tarehe 10 Novemba, 2023 na shughuli zilizopangwa kufanyika katika Mkutano huu haziwezi kukamilika iwapo Vikao vya Bunge vitafanyika katika siku za kazi peke yake (Jumatatu mpaka Ijumaa).

Mheshimiwa Mwenyekiti na kwa kuwa Kanuni ya 34(15) inaelekeza kwamba Bunge halitakutana siku za Jumamosi, Jumapili na siku za Mapumziko.

Na kwa kuwa, Kamati ya Uongozi ya Bunge katika Kikao chake cha tarehe 30 Oktoba, 2023 iliridhia kwamba katika Mkutano huu wa 13 wa Bunge Bunge likutane siku ya Jumamosi tarehe 04 Novemba, 2023 kwa ajili ya kufanya kazi.

Hivyo basi, ili kuleta ufanisi katika utekelezaji bora wa shughuli za Bunge naomba Bunge liliridhie Kanuni ya 34(15) itenguliwe ili kuruhusu siku ya Jumamosi ya tarehe 04 Novemba, 2023 itumike kwa ajili ya Vikao vya Bunge isipokuwa kwamba siku hiyo Bunge litaanza saa 03:00 Asubuhi hadi saa 8:00 Mchana na hakutakuwa na kipindi cha maswali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kufikiwa)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ahsante sana na hoja imeungwa mkono, tunashukuru sana Waheshimiwa Wabunge.

Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA KAMATI**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali kuhusu Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa hesabu zilizokaguliwa na Serikali Kuu, Mashirika ya Umma na Kaguzi za Ufanisi kwa Mwaka wa Fedha uliuoishia tarehe 30 Juni, 2022**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kuhusu Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka za Seriakli za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha ulioishi tarehe 30 Juni, 2022**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezajiwa wa Mitaji ya Umma kuhusu uwekezaji wa mitaji ya umma kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge ninayo orodha hapa ya wachangiaji, tutaanza na Mheshimiwa Mwita Waitara atafuatiwa na Mheshimiwa Deo Sanga na Mheshimiwa Ester Bulaya ajiandae.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru sana kwa kupata nafasi ya kuchangia hoja hii muhimu sana lakini nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwamba muda kama huu mwaka 2021 nilikuwa Bungeni, mwaka 2022 nilikuwepo na mwaka 2023 nipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimeshuhudia kaguzi hizi zikifanyika na ningependa sana kupata taarifa mimi na Wabunge wenzetu kwamba ukaguzi ukifanyika na ikaonyesha kuna mtu

mhalifu wa eneo fulani ni hatua gani zinachukuliwa? Au tunachukua ripoti tunatunza miaka mitatu, minne, mitano kumi kama kawaida? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpongeze Mheshimiwa Rais, Mama Samia, Mama wa Taifa. Kwamba ameongeza nguvu ya Serikali kumteua Mheshimiwa Doto Biteko, Naibu Waziri Mkuu kufanya kazi ya kusaidia Serikali lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu amefanya kazi kubwa sana na nzuri sana anapoenda katika Mikoa na Majimbo yetu kufanya ukaguzi na kuainisha wabadhirifu na mara nyingi kuchukua hatua katika umahiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais amemteua pia Mheshimiwa Mchengerwa nimefurahi kazi imeanza kwa kasi kwa kuwajibisha watu ambao wanafuja fedha katika Halmashauri na Mheshimiwa Rais ameunda Kamati ambayo ilipitia Wizara ya Mambo ya Nje na Afrika ya Mashariki na kumuonyesha namna ambavyo kuna uozo na upendeleo katika ajira maeneo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba Mheshimiwa Rais Kamati ile isiishie pale iende ikachunguze Wizara ya Mambo ya Ndani, iende ikachunguze Ofisi ya Rais, TAMISEMI, iende kuangalia ma *RAS*, iangalia ma-*RC* iangalie ma-*DED* na ma-*DC* kweli wanaweza kufanya kazi waliopewa na kama wanamsadia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwaombe Waheshimiwa Mawaziri wakitaka kutoa taarifa tunapochangia ripoti hii waangalie maswali ambayo wanaulizwa katika Bunge hili. Mbunge anatoa mishipa hapa anaomba apelekewe milioni hamsini kujenga zahanati wewe unatuambia kuna Mtumishi mmoja wa umma, Mtanzania mwenzetu amekula mabilioni anatembea na ma VX mtaana na bado tunampigia makofi. Naomba hili Waheshimiwa Mawaziri mliangalie sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapochangia hoja hii Mkaguzi Mkuu wa Serikali ni daktari ameenda amechunguza taarifa amekwambia hapa kuna wizi. Halafu wewe unaambiwa unaumwa *malaria* unasema hapana mimi siumwi hii siyo sawa,

siyo sawa hata kidogo. Kwa sababu hiyo kasi ya Mheshimiwa Rais kutafuta fedha ni kubwa sana lakini bahati mbaya kasi ya kuiba fedha za umma imekuwa kubwa sana vilevile. Maana yake ni kwamba unachota maji unaweka kwenye mkono wako wa kushoto halafu huku kibaka mwingine anatoboa ile pakacha maji yanavuja kwa hiyo, mwisho wa siku hautajaza hilo pipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba Waheshimiwa Wabunge tena wengi hapa ni Wanachama wa Chama Cha Mapinduzi karibu wote hapa. Kama kuna Waziri ataondolewa pale kwa uzembe ataingia kada wa Chama Cha Mapinduzi mwingine kama kuna Mtumishi mwingine atawajibishwa atakaeingia kwenye nafasi hiyo ni Mtanzania mwenzetu hili Bunge linasubiriwa na Watanzania kwamba mnasaidia Mheshimiwa Rais? mnawasemea Watanzania? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imetoa mapendekezo, Kamati hii imetoa mapendekezo mazuri lakini yamepungikiwa uzito mimi nilitarajia watatuambia hapa baada ya Ripoti ya CAG wangapi wamefungwa kwa wizi wa umma? Baada ya ripoti hii watuambie wangapi wamefukuzwa kazi? Baada ya ripoti hii watuambie wangapi wametapika fedha za Watanzania masikini ambazo wamekula? Na wangapi ambao wana kesi Mahakamani ni mpaka tunavyozungumza hapa leo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii taarifa hatujapewa, ingependeza tupewe hiyo taarifa lakini Waheshimiwa Wabunge mkumbuke tunazungumza mabilioni ya fedha yameibiwa lakini Watendaji wa Vijiji hawana hata baiskeli nchi hii, Watendaji wa Kata hawana hata pikipiki na pikipiki walizopewa hawana *spare,* hawana mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, waratibu wa Elimu ya Kata nchi hii wanatembea kwa miguu kukagua elimu. Sasa hivi wanafanya mitihani ya *form two* wanaenda mvua zinanyesha, wananyeshewa wakitembea kwa miguu, hawana hata kirukuu cha kuwapeleka lakini wapo watu hapa wamevimbiwa fedha za Watanzania wao wanapigiwa makofi na Wabunge tuwashangilie, hii haikubaliki, hii haikubaliki na hatuwezi kuunga mkono uzembe huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge lazima wafahamu kwamba katika Majimbo yetu tuna watoto wanakaa chini nchi hii hawana madawati. Kuna walimu hawana nyumba za kuishi, kuna walimu wetu wanadai madai mbalimbali tunataka posho ziongezeke, vijana wetu wako mtaani tungepata fedha hii ikafanye kazi vizuri maana yake Serikali ingeajiri vijana wa Tanzania waliosomeshwa na Wachungaji, Wakulima, Wafugaji na wako mtaani. Kwa sababu Serikali ina fedha nyingi ya kuajiri watu hao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mjadala huu tutawaomba wenzetu waliofanya uzembe katika maeneo mbalimbali na mimi nina mapendekezo ambayo siyo laini sana nchi kama Korea kuna mpaka watu wananyongwa kwa makosa kama haya. Sasa ningependekeza wale wote ambao wamethibitika pasipo shaka kwamba wamekula fedha za Watanzania na Waheshimiwa Wabunge wa CCM uchaguzi ni mwaka kesho Serikali za Mitaa na 2025 nimesoma mitandao. Mheshimiwa Rais tumsaidie na Wabunge tufanye maamuzi hapa, wale wote walioiba bila kuwaonea hawa watu wanyongwe kwenye nchi hii watoke, tubaki na watu wema katika Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale watu wote ambao wameonekana ni wazembe na wana nafasi katika umma hawa wafukuzwe kazi zao, wakae mtaani lakini…*there is no gain without pain* ni lazima tuwe na sindano kama unaumwa Malaria utachomwa *chloroquine* ili upone japo ni chungu…

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa, taarifa, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Maganga.

**TAARIFA**

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nataka nimpe taarifa mzungumzaji anaeendelea kuongea kwanza Viongozi wote wa Serikali wanaofuatilia mdahalo huu mimi toka mwaka jana nilisema bila kupitisha Sheria

ya kunyongwa watu, wizi hatuwezi kuumaliza. Kwa hiyo, naungana nae kabisa kwenye Sheria ya kunyongwa sisi ni Wabunge tupitishe hiyo sheria ili kusudi tumalize biashara, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika michango mizuri ya Mheshimiwa Maganga ni pamoja na Taifa hili ambalo naipokea kwa mikono miwili…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara taarifa unaipokea?

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeishaipokea kabla hajamaliza kuongea. Mheshimiwa… *(Kicheko)*

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa, taarifa..

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Anatropia.

**TAARIFA**

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa kwamba hii ripoti uliyoiona hapa ni *roughly* chini ya asilimia ishirini ya taasisi zote na Taasisi za Serikali Kuu. Kwa hiyo, sasa unaweza ukaona ni wangapi watanyongwa katika hii nchi? *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara taarifa unaipokea?

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea hii ripoti, hii taarifa yake. Maneno yangu leo hayafanani na suti niliyovaa, naomba niseme hivyo. Sina maneno mazuri zaidi ya hayo, nachopendekeza kwa Waheshimiwa Wabunge ni kwamba tumekuwa tunajadili mambo ya msingi katika Bunge hili lazima tujue Watanzania wengi wapo nje sisi tuna wawakilisha. Bunge likihairishwa tarehe 10 Ijumaa ijayo kila Mbunge ataenda Jimboni kwake, mnaweza mkaona kiwango cha umasikini cha watu wetu ambao wanashindwa kupeleka watoto shule kwa

sababu hawana uwezo wa kuwalipia watoto wale wanakuja kwa Wabunge tuwasaidie hata mpaka sare.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wako watu ambao, kwanza tukiwanyonga hawa hatujawaonea itakuwa ni haki yao kwa sababu katika Utumishi wa Umma ukiacha sisi Wabunge na Waheshimiwa Mawaziri ambao wanaweza wakawa Mawaziri kwenye sekta ambayo hakusomea. Watumishi wote wa umma wamesomeshwa na Watanzania, wana vyeti ukiwaambia walete *CV* wanakujazia mezani mpaka huwezi kuonekana kwa mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake hawa wanafanya makusudi na wanaiba kitaalamu uzembe ulipo sisi ni sisi Wabunge kwamba, mtu ameishaiba, ripoti ipo, taarifa ziko mezani, vyombo vipo hawawajibishwi hivi nyie Waheshimiwa Watanzania na Viongozi wenye dhamana mnawafundisha nini watoto wetu? Kwamba wakue wakijua kwamba, wala hata ukiiba utahamishwa kutoka Wizara hii kwenda Wizara, kutoka Kitengo hiki kwenda Kitengo hiki na hakuna uwajibikaji? Nendeni mjifunze wenzetu walioendelea…

**MHE. PHILIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo, mwongozo, mwongozo…

**MHE. MWITA M. WAITARA: …**unafanya makosa ambayo… muda wangu Mheshimiwa Mwenyekiti ulindwe…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwongozo.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Mbunge wa Chama cha Mapunduzi, moyo unaniuma. Mbunge mwenzetu anapochangia kwenye taarifa kama hii inauma kuona wanaohusika, Mawaziri wanachati na simu, wanaongea na simu. Hawajali kile anachokiongea Mheshimiwa Waitara kama vile ni jambo linapita. Mimi binafsi inaniuma sana. Naomba mwongozo wako.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Augustino Mulugo, basi mwongozo utatolewa baadaye. Mheshimiwa Waitara endelea na mchango wako.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mchango wa Mheshimiwa Phillipo ni muhimu sana. Waheshimiwa Wabunge wenzangu wa Chama Cha Mapinduzi, kwanza naomba niwaombe, dhamana tuliyopewa ni kubwa sana, na chama hiki ndicho ambacho kimetusaidia Watanzania kuwa hapa tulipo. Sisi Wabunge wa Chama Cha Mapinduzi na tumefuatilia Mabunge yaliyopita, sisi ndio wenye dhamana na Serikali hii ni ya kwetu na hawa watu ni wa kwetu. Tukiwawajibisha sisi, ni sisi wenyewe. Msisubiri kuja kuambiwa, chukueni hatua, na hatua ni sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi napendekeza, kama tutakuwa tunafanya ukaguzi, tunampa fedha *CAG* na magari anazunguka; Kamati zinakaa na tunalipwa posho; ripoti inakuja makabrasha ya kujaza makabati, tunayaacha eti mwakani tena tunaletewa ripoti kama hii. Mimi hiyo ikija mwakani kama nitakuwepo, Mungu akinipa uhai, siwezi kuchangia tena… *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana…

**MHE. MWITA M. WAITARA:** …kwa hiyo tunataka tuone hatua zinachukuliwa kwa watu ambao wanamkwamisha Mheshimiwa Rais. Mama anatafuta fedha, anajaza kikapu halafu wako vibaka fulani hivi wanakula hela…

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waitara…

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii haikubaliki. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya. Namwita Mheshimiwa Deo Sanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Ester Bulaya. Mheshimiwa Zainab A. Katimba, ajiandae.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuku na mimi kwa kuniona na kunipa nafasi ili niweze kuchangia juu ya Kamati hizi ambazo zimewasilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais wetu anahangaika sana kutafuta fedha usiku na mchana kwa ajili ya Watanzania. Kwa ajili ya shughuli za maendeleo. Sasa mimi nina mambo machache sana ya kusema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja; Serikali imetafuta fedha imeanzisha Kiwanda cha Dawa kule Njombe, Makambako. Kiwanda hiki cha kutengeneza mipira *(gloves)* tayari kimeanza. Vilevile kuna kiwanda kingine ambacho majengo yake yalishajengwa, cha kutengeneza vidonge pamoja na *syrup*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanda hiki tangu kimenunuliwa na majengo yamejengwa ni zaidi ya miaka miwili na nusu ili Serikali ipunguze gharama za kuagiza madawa nje, lakini hakuna kinachoendelea, kiwanda hiki hakijaanza. Huu ni uharibufu wa fedha ambazo zimekaa tu huku Watanzania wanasubiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sipendi niliseme sana kwa sababu Makamu wa Rais alipokuja alitoa maelekezo. Sasa kupitia Bunge hili, na Kamati husika ya Bunge ilishakuja na ilizungumza juu ya kiwanda hiki; naombe kiwanda hiki kianze kama ilivyokusudiwa ili kuongeza tija ya viwanda vilivyopo katika nchi yetu. Tutakuwa tumeitendea haki Serikali ya Awamu ya Sita ambayo imetoa fedha mabilioni na mabilioni kwa ajili ya kiwanda hiki, lakini zipo zimelala pale halafu, hakuna kinachoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na baadaye mitambo ya kiwanda hiki; kwa sababu haijafungwa, iko kwenye ma-*box;* baadaye itaonekana ni ma-*scraper* tu kwa sababu imekaa kwa muda mrefu. Kwa hiyo, tukuombe, Kamati inayohusika ihakikishe kiwanda hiki kinaanza kama ilivyokusudiwa. Tutakuwa tumeitendea haki Serikali ya Awamu ya Sita, ambayo imeleta fedha zimekaa tu pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, amesema Mheshimiwa Mbunge ambaye amemalizia hapa. Unajua

wanasema mtu akifanya kosa anatakiwa aadhibiwe. Sasa inategemea na adhabu wanazopata watu, inawezekana wanaona kama ni ndogo. Kwa sababu adhabu zingine ni kwamba unatolewa ulipo na unakwenda mahala pengine, ile ni kama si adhabu. Mimi nadhani adhabu hii aliyoisema Mheshimiwa Waitara, hii ndiyo itatufikisha; watu wataogopa. Kutumia vibaya fedha za Serikali, fedha za awamu ya sita ambayo mama anahangaika usiku na mchana kwa ajili yetu sisi Watanzania. Kwa hiyo, nilikuwa nadhani hii sheria hebu iletwe hapa, acha ile sheria ambayo mtu akiua anatakiwa auwawe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, hii akiiba mali ya Serikali auwawe; anyongwe mpaka kufa, litakuwa ni jambo la muhimu sana. Mimi naunga mkono kabisa hoja hii kwamba, angalau itapunguza watu kuiba hela za mama ambaye anahangaika, anatuletea mabilioni na matrilioni. *(Makofi/Vicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mawaziri wote walioko hapa hawalali, wanahangaika kuja kuwaambia wananchi huko kutembea kwa sababu ya fedha hizi ambazo zinaletwa za maendeleo katika nchi yetu. Sasa wanapatikana wachache wanakula hizi fedha. Ni lazima Serikali ichukue hatua ya kuona wanapewa adhabu.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE–SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Deo Sanga, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka.

**TAARIFA**

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kumpa taarifa Mbunge makini wa Makambako. Hatua ya kwanza ya kupambana na ufisadi huu ni kwa CCM kukubali kujitenga na wahalifu hawa. Mwalimu Nyerere amesema; "CCM iking'ang'ania umoja wa bandia na watu wasio waadilifu itaununua umoja huo wa bandia kwa gharama ya kuweka

itikadi yake na kukubalika kwake na umma" na Mwalimu akaendelea akasema "CCM isiyo na msimamo katika mambo ya msingi itakuwa ni sawa na gulio au soko lililowakusanya watu kwa nia ya kutaka madaraka" na Mwalimu anasema "Nani anaitaka CCM ya namna hiyo?"

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hatua ya kwanza ni Mawaziri wa CCM kujitenga na wahalifu ambao ni *accounting officers*, maafisa masuhuli walioingiza nchi hii katika janga la wizi. Namna ya kijitenga ni kuchukua hatua chini ya uongozi wa Waziri Mkuu makini, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa. Chukueni hatua, toeni maelezo hapa juu ya hatua mtakazo chukua. Vinginevyo azimio langu la mapendekezo litaendea kuwepo palepale.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Deo Sanga, taarifa unaipokea?

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, alikuwa anakazia kwa sababu ipo kwenye Ilani ya CCM, kwamba mafisadi watashughulikiwa. Iko kwenye Ilani, siyo jambo jipya iko kwenye Ilani. Ni hii tu sasa Bunge liweze kuona namna ya kutunga sheria ya kuwashughulikia hawa ambao wanaharibu hela ya mama ambayo ametuletea kwa ajili ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, juzi nimesema na sasa niseme tena; sasa niseme kwa unyenyekevu na utulivu mkubwa na upole kabisa. Tumepata heshima kubwa ya Dkt. Tulia Akson. Kwanza tunawashukuru wazazi wake kule Mbeya, pili, tunawashukuru Watu wote wa Mkoa wa Mbeya kwa kumlea kijana wetu vizuri na hatimaye ameweza kukubalika huko duniani. Tatu, tunampongeza na kumshukuru Mheshimiwa Rais wetu ambaye amesimama kidete kwa ajili ya Mheshimiwa Spika wetu Dkt. Tulia Akson.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu, kwanza kwa Watanzania na kwa wenzetu wa Mbeya; waone kwamba heshima tuliyopewa ya kiongozi wetu huyu kwa kupata heshima kubwa duniani; watu wa Mbeya niwaombe, chonde, hebu tumuache huyu. Mungu ana makusudi yake na Mheshimiwa Rais ana makusudi yake. Tumuombee Watu wa Mbeya, asijitokeze

mtu mwaka 2025. Mtaweka kikwazo cha mipango mikubwa ya Dkt. Tulia Akson. Bunge hili tunamuombea na Watanzania wote tumuombee Dkt. Tulia Akson kwa mambo makubwa ambayo yako mbele, Mungu ameyaweka, tusiweke kizuizi. Nimeona niliseme hili kwa dhati kabisa kwamba Mungu ana makusudi, tumuombee *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, nirudie kwa Mawaziri wangu mnafanya kazi nzuri. Mmekuwa mkija kutoa ufafanuzi wa maendeleo yanayotakiwa. Mnafanya kazi nzuri chini ya Mheshimiwa Waziri wetu, Kiongozi wetu wa Seikali Kassim Majariwa Majariwa. Anasimamia vizuri shughuli za maendeleo na tunamuombea sana. Na wewe Mheshimiwa Majaliwa Majaliwa kule Luangwa; mimi kama mzee, watu wa Luangwa chonde chonde, tunamuhitaji. Msijaribu kufanya kitu chochote, hebu mmuache aweze kufanya kazi ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na Mungu akubariki. Ahsante sana. *(Makofi/Vigelegele)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Deo Sanga. Mheshimiwa Ester Bulaya, atafuatiwa na Mheshimiwa Zainab Katimba. Mheshimiwa Miraji Mtaturu, ujiandae.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia. Mchango wangu utaanzia pale kwenye taarifa aliyopewa mdogo wangu, Mbunge wa Igalula; kwamba tusizungumze mambo kiujumla jumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mosi, tutazungumza kiujumla jumla kwa sababu taasisi zimetajwa kiujumla jumla halafu sasa tutawasaidia kuwataja waliohusika. Naanza na ukaguzi maalum uliofanywa kwenye Mfuko wa Tuzo na Tozo na Kufa na Kuzikana katika Jeshi la Polisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kifungu cha 66(3) cha Sheria ya Jeshi la Polisi na Huduma Saidizi Sura Na. 333, kimeainisha kuwa Inspecta Jenerari wa Polisi ndiye mwenye

mamlaka ya fedha kwenye mfuko huo. Mwaka 2018 mpaka 2020/2021 Inspecta Jenerari wa Polisi alikuwa Sirro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mfuko huu, umetajwa ufisadi wa shilingi bilioni moja. Anayeidhinisha fedha hizi, alikuwa Simon Sirro, mleteni kokote aliko aje apambane na hali yake. Hamuwezi mkafumbia macho hivi vitu. *(Makofi/Vicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mfuko huu umeanzishwa kwa dhamira moja ya saidia Askari wadogo wa Jeshi la Polisi. Wakifiwa na wenza wao zisaidie zile familia. Wanaopambana na Jeshi, wanaopambana kwa damu na Jasho katika kulinda nchi hii kwa kupambana na majambazi, wakipata madhara hizi fedha ndizo ziwasaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfuko huu wanaochangia ni askari wenyewe kwa kufanya kazi ya ziada kulinda kwenye migodi, benki na taasisi mbalimbali; halafu wanatokea vingozi wao wana-*take advantage* kwa ile nidhamu ya kijeshi kwamba hawawezi kuhoji, wanawadhurumu askari wa kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuulize leo Sirro yuko wapi, si ni Balozi? Arudishwe aje abebe mzigo wake. Hakuna Bunge la kulinda watu wa namna hii. Kuna wengine wametajwa waziwazi, leo ni Naibu Katibu wa Maliasili na Utalii. Katajwa waziwazi, tena tu baada ya Ripoti ya *CAG* anapata *promotion. Why? (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo askari hawa mbali na fedha zao kutafunwa kwenye huu Mfuko wa Tozo wanaochangia kwa jasho lao kwenda kulinda kwenye migodi fedha zao hazijulikani zilipo. Halafu unaambiwa alikuwa tu anachukua anaidhinisha, anatoa *BOT* anapeleka huku, anatoa huku anapeleka huku. Kati ya Kombania 62 amapeleka kwenye Kombania tano tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za ulinzi wa nchi hii, askari wanatoa mikoa yote. Watu wanasema alipeleka kwa washikaji zake, mimi sijui. Askari wana uchungu, na ndiyo hawa hawa wakistaafu wanakuwa wanapata kikokotoo cha shilingi milioni 17. *It is not fair*, si sawa. Mimi ni Mbunge naenda kwa *term* ya tatu; tumekuwa tukijadili sana vitu hivi, vinakera. Haya,

tuliwanong'onezaga nyie kuhusiana na ufisadi wa *MSD* hamkuchukua hatua mapema, *CAG* akasema. Wengine tuna uwezo wa kupata taarifa mapema. Haya mmempeleka wapi; nasikia amerudishwa Jeshini. *Is it fair*, mnataka tunyamaze? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukienda katika Mfuko wa Kufa na Kuzikana, mlezi ni *IGP,* na wa kipindi hicho alikuwa ni Simon Sirro. Ubadhirifu kwenye Mfuko wa Kufa na Kuzikana ni shilingi bilioni 4.6. Waheshimiwa Wabunge, fedha katika mfuko huu ni michango ya elfu tano ya kila mwezi ya watumishi wa Jeshi la Polisi. Walivyodai uitwe mkutano mkuu ili wahoji matumizi hakuna kilichofanyika. Miaka mitatu, mitano halafu leo nasikia wakati *CAG* anafanya uchunguzi walivyoenda kumhoji *IGP* msaafu anasema, huyo aliyehusika eti ametoweka; kweli, mtumishi wa Jeshi la Polisi katoweka na nyaraka? Mnataka tuyavumilie hayo? Aliyekuwa kiongozi wa ulinzi wa Jeshi anatoa amri; yeye anahusika na hivi vitu halafu mnampa Ubalozi. Arudishwe apambane na hali yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi mwenye sifa tutampa; na ninachukua fursa hii, maana huu uchunguzi haukuanzishwa bure; aliye-*engineer* alikuwa Katibu Mkuu wa Wizara hii. Sijui leo yuko wapi, Mungu amsaidie. Labda alinusa harufu ya rushwa. Kwa unyenyekevu mkubwa na kuipenda nchi yake akaagiza haya yafanyike. Inawezekana akaondolewa lakini watu kama hawa ndio tunu ya kulinda, wanaonusa harufu za wezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, atakayefanya vizuri tutamsifia na atakayefanya vibaya, popote alipo aletwe apambane na hali yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayasema haya kwa uchungu. Haya nije kwenye halmashauri. Ubadhirifu wa shilingi bilioni 11 ya makusanyo yaliyotakiwa kwenda benki kupitia *POS*, shilingi bilioni 11 watu wamekusanya wameweka mfukoni. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine baada ya kuona zimepelekwa hizi Mashine za *POS* kwa ajili ya kuzuia wizi; wengine walizima. Chamwino walizima mashine ya *POS* kwa siku 1,905, Uvinza walizima mashine ya *POS* kwa siku 1,133, Ushetu walizima mashine ya *POS* kwa siku 397, Sengerema walizima mashine ya *POS* kwa siku 185. Mnajua kwa nini wanafanya hivyo; ni kwa sababu tunawalea. Hawa wakurugenzi wapo. Halafu anakuja kwenye Kamati anakwambia, unajua tumewapeleka TAKUKURU. Tukawauliza muda gani wanadai miaka mitatu, kwa nini tusiseme kwamba TAKUKURU ni kichaka? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shilingi bilioni 11 za makusanyo kwenye majimbo yenu watu wametafuana; halafu wanatuambia wanapelekwa TAKUKURU; wengine bado wapo kwenye vituo vya kazi. Halafu mnataka tuyanyamazie haya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka wakati Rais anapokea ripoti alivyozungumzia mikopo hii ya asilimia 10, fedha ambazo hazijakusanywa zimeongezeka kutoka bilioni 47 mpaka bilioni 88. Mchanganuo wake sasa, mchanganuo wake unaambiwa milioni 900 ni vikundi hewa. Milioni zaidi ya 700 eti vikundi watu wamechukua mkopo halafu wakagawana. Bilioni 2.5 eti vikundi sasa hivi havijishughulishi na kazi yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwaambie, watoaji mikopo Mwenyekiti ni Mkurugenzi, yuko Afisa Maendeleo, yuko *DT,* yuko Afisa Mipango, inakuwaje kuna vikundi hewa vinapewa mikopo? Inakuwaje kuna vikundi vyenye thamani ya bilioni 2.5 eti havifanyi biashara? Inakuwaje eti kuna vikundi vya thamani ya milioni 700 eti watu wamepewa mikopo halafu wakagawana? Mnajua kwa kwa nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kanuni ya mikopo imesema wazi kabla hujatoa mikopo, lazima ukatoe elimu, lazima utembelee vikundi, lazima ujiridhishe na biashara wanayofanya. Halafu wanakuja kuleta majibu mepesi kwenye pesa zaidi ya bilioni 88 ambazo zingejenga zahanati, ambazo zingejenga vituo vya afya, wako ofisini. Sasa namshauri Rais …

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya, kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Shaban Ng'enda.

**TAARIFA**

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpa Taarifa dada yangu, Mheshimiwa Ester Bulaya, ambaye anazungumza kwa uchungu mkubwa sana tena kizalendo kwamba, mambo hayo ambayo yeye anayaona yana uchungu mkubwa katika ubadhirifu wa pesa za umma, ndio yanayowafanya Wabunge wa CCM waseme itungwe sheria ya kufanya watu wanaofanya hayo sasa wakatwe vichwa. Kwa hiyo, katika Bunge hili suala la ubadhirifu na wizi linawaudhi watu wote, Wabunge wote na wananchi wote wa Tanzania. Halina itikadi hili ndio maana Wabunge wa CCM wanasema tulete sheria ya kukata vichwa watu hawa. Dada yangu endelea. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester, Taarifa unaipokea?

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa ikitoka kwa kaka, *senior,* lazima niipokee, najua uzalendo wake wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wakati muafaka tukamshauri Rais, tuanze kuangalia sifa za Wakurugenzi, uteuzi wake. Mkurugenzi ndio *CEO* wa Halmashauri, anatakiwa awe na weledi wa kutosha, isiwe tu tunateuana kwa ajili ya kutoa zawadi, matokeo yake ndio haya, watu wanashindwa kutimiza majukumu yao kulisaidia Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Naunga mkono hoja taarifa zote tatu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nimemwita Mheshimiwa Zainab Katimba, atafuatiwa na Mheshimiwa Miraji Mtaturu na Mheshimiwa *Engineer* Ezra J. Chiwelesa ajiandae.

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa ili niweze kuchangia hoja zilizoko mezani. Kwanza kabisa nadhani sote tutakubaliana kwamba, Mheshimiwa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan, anafanya kazi kubwa sana ya kutafuta fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo, kwa ajili ya kutuletea maendeleo kwenye Taifa hili. Kwa hiyo, kuna kila sababu ya kuhakikisha fedha hizi zinakuwa na tija katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye ukurasa wa 11 wa Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali *(PAC)* utaona kwamba, wamebaini upotevu wa fedha nyingi ambao unatokana na dosari katika usimamizi wa ukusanyaji wa mapato. Mfano, ukiangalia, katika mwaka 2021/2022, *TRA* imerekodi nakisi ya bilioni 887.3 katika ukusanyaji wa mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye ukurasa wa 10 kwenye Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa *(LAAC)* utaona kwamba, wametoa taarifa na wameainisha kuwepo kwa mifumo dhaifu ya ukusanyaji wa mapato ya ndani pamoja na kushindwa kukusanya madai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano ni katika mwaka 2021/2022, kuna upotevu wa bilioni 11.07 zilizokusanywa na mashine za ukusanyaji wa mapato *(POS)* ambazo hazikuwasilishwa benki. Sasa kwanza, tunataka fedha hizo ziwasilishwe benki, hiyo ndio hatua ya kwanza. Hatua ya pili, tunataka wote waliohusika na ubadhirifu huu wachukuliwe hatua. Watanzania tunataka kuona hatua inachukuliwa, hii ni jinai, huu ni ubadhirifu, tunataka tuwaone wako katika mikono ya sheria wabadhirifu wa fedha hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, twende mbele tutengeneze Suluhu ya kudumu. Tunahitaji kutengeneza na tuendelee kuwekeza katika kutengeneza mifumo imara ya kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato, lakini katika manunuzi ya umma. Nafahamu Serikali imefanya jambo kubwa sana katika eneo hili, lakini tunahitaji kuwekeza zaidi. Hii mifumo iwe inasomana kwa sababu, tukifanikiwa kutoa mkono wa binadamu katika makusanyo ya mapato na katika manunuzi ya umma, basi,

tutafanikiwa kwa kiwango kikubwa kusaidia kuondoa au kupunguza kwa kiasi kikubwa upotevu wa fedha za umma, rushwa, lakini pia, tutakuwa tumeongeza uwazi katika matumizi ya fedha za umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 10 cha Sheria ya *Public Audit Act* kimefafanua majukumu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali *(CAG)*. Kwa hiyo, pamoja na majukumu yake ana jukumu kubwa la kufanya ukaguzi wa hesabu za Serikali kwa niaba ya Bunge. Kwa hiyo, *CAG* kimsingi ni jicho la Bunge katika kuisimamia Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kazi hizi za *CAG* mara nyingi kazi yake yeye anayoifanya *CAG* ni *post mortem,* yaani anakuta ubadhirifu ulishafanyika, fedha zilishapotea, wezi walikwishaiba kwa hiyo, yeye anatoa ripoti anaiwasilisha kwa hiyo, kazi yake inakuwa imeishia hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mtu muhimu sana anaitwa Mkaguzi wa Ndani. Mkaguzi huyu wa Ndani ni mtu muhimu sana, hii Ofisi ya Mkaguzi wa Ndani ni ofisi muhimu sana ambayo inahitaji kuwezeshwa kwa sababu, Mkaguzi wa Ndani anaweza kuzuia upotevu wa fedha. *CAG* anakuja kutoa ripoti, kuripoti ubadhirifu wa fedha, matumizi mabaya ya fedha, lakini huyu Mkaguzi wa Ndani ana uwezo wa kuziwia ubadhirifu wa fedha kabla haujatokea au kabla haujafika mbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kila mwaka Ripoti ya *CAG* inaletwa kwenye Kamati inajadiliwa, inakuja Bungeni, tunatoa maazimio, mwaka unaofuata tunaenda hivyo hivyo, lakini sasa ili kutengeneza suluhu tumwezeshe huyu mkaguzi wa ndani. Niipongeze Serikali katika eneo hili kwa sababu, katika kipindi cha bajeti, Mkaguzi wa Ndani ameweza kuanzishiwa Fungu Na.6 kwa hiyo, amewezeshwa kibajeti. Hapo awali tulikuwa tunaona changamoto, huyu Mkaguzi wa Ndani, kwa mfano, kwenye Halmashauri, alikuwa anategemea fedha ya kufanya kazi zake kutoka kwa Mkurugenzi na Mkurugenzi ndio huyohuyo anayekaguliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ukikuta kwamba, Mkurugenzi na yeye ni sehemu ya ubadhirifu, maana yake anatengeneza mazingira magumu ya Mkaguzi wa Ndani kufanya kazi. Atasema hamna fedha, atasema hamna gari, mara gari halina mafuta, lakini kwa kuanzishwa kwa Fungu Na.6, hili imeweza kusaidia kumuwezesha Mkaguzi wa Ndani kufanya majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa twende mbali kwa sababu, Ripoti ya Mkaguzi wa Ndani inaishia kwenye Menejimenti. Sasa Menejimenti yenyewe ndiyo hiyo hiyo mara nyingi ndiyo inayotuhumiwa kwa ubadhirifu. Kwa mfano, katika Halmashauri. Mkaguzi wa Ndani akileta ripoti katika Menejimenti ndio hao hao watuhumiwa wanaokaa kupokea hiyo ripoti. Unategemea nini kitafanyika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Ripoti ya Mkaguzi wa Ndani wa Serikali iende mbali zaidi. Tutengeneze mamlaka ya juu zaidi, tutengeneze mamlaka za kikanda, lakini iende juu ifike mpaka kwa mamlaka za juu ifike hata katika Ofisi ya Waziri Mkuu ambaye ndio msimamizi wa shughuli za Serikali. Pia, tunaweza tukaangalia ikafika hadi kwa Katibu Kiongozi, ili watu wachukuliwe hatua za nidhamu kabla ubadhirifu haujafika mbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoteza fedha nyingi sana kwa kusubiri kwamba, wezi waibe, wahamishwe vituo, ukaguzi ufanyike, fedha zimepotea, tunakuja kujadili hapa kila mwaka, kila mwaka ripoti hizi zinakuja zinajirudia. Kwa hiyo, tutafute suluhu ya kudumu na tuiwezeshe Ofisi hii ya Mkaguzi wa Ndani iweze kuwa imara, ili iweze kutusaidia kuepuka au kukinga ubadhirifu unaofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda Ukurasa wa 29 wa Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali *(PAC)* utaona kwamba, imeainishwa. Katika hoja za ukaguzi, kuna hoja za ukaguzi ambazo zinatokana na dosari katika usimamizi wa mkataba na athari zake katika matumizi ya fedha za umma. Mfano, utaona kwamba, Serikali imepata hasara ya bilioni 36.8 ambayo imetokana na tozo ya riba kwa *TANROADS* kwa kuchelewa kulipa wakandarasi na washauri wa miradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bilioni 36.8 ni fedha nyingi sana na fedha hizi ndio zinasababisha miradi itumie gharama kubwa zaidi kuliko ile iliyokuwa imepangwa. Mradi unakuwa umepangiwa kutekelezwa kwa milioni 100, lakini mwisho wa siku unashangaa mradi umetekelezwa kwa milioni 150. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunaomba sana, hizi fedha zinazopotea zingeweza kutumika katika maeneo mengine yenye uhitaji wa rasilimali fedha. tunaomba Serikali itafute suluhu ya kudumu ya kulipa fedha kwa wakati, wakandarasi walipwe fedha zao kwa wakati, washauri wa miradi walipwe fedha zao kwa wakati, ili tusije tukalipa riba ambayo ni hasara kubwa kwa Serikali na hizi fedha zinaweza kutumika katika maeneo mengine kwa maslahi mapana ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, naomba kuunga mkono hoja za Kamati zote tatu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Zainab Katimba. Nimemwita Mheshimiwa Miraji Mtaturu, atafuatiwa na Mheshimiwa *Engineer* Ezra Chiwelesa na Mheshimiwa Issa Mtemvu ajiandae.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hoja iliyoko mezani, Ripoti za Kamati zetu za *PAC, LAAC* pamoja na *PIC*. Sasa naenda moja kwa moja kwenye hoja yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipimo cha Serikali inayozingatia utawala bora kwa maana ya *good governance,* vipo vingi, lakini viwili ndio nguzo yake. Cha kwanza, ni kufuata demokrasia, kufuata sheria katika kuongoza, lakini ya tatu kwa maana ya haki, kutoa haki kwa wananchi wake ikiwemo huduma. Haya mambo makubwa matatu ndio yanakuwa yanaangaliwa katika vipimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ni kuzingatia matumizi bora ya fedha na rasilimali za umma. Haya mambo mawili ndio yanabeba sura ya utawala bora. Kwa hiyo, kwenye hili tumpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa dhamira yake njema ya

kutoa uongozi kwa maana ya kwamba, anaonekana kwa vitendo na maneno yake kwamba, anatamani nchi iongozwe kwa utawala bora. Kwa maana ya kwamba, demokrasia anataka watu tuongozwe kwa pamoja na kufuata sheria, lakini pia wananchi wapate haki zao na tumekuwa tukimuona waziwazi kwenye hotuba zake mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utawala duniani unaongozwa na aina mbili. Utawala unaoongozwa mojawapo na viongozi wa kisiasa, lakini pia kuna watumishi wa umma ambao ni *civil servants.* Kwa hiyo, watu hawa wawili ndio wanasaidiana kwa pamoja kuongoza nchi au kuongoza eneo lolote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo tunaona wote, Mheshimiwa Rais anakemea, Wabunge tunasimama hapa tunakemea, lakini hata Madiwani kwenye Halmashauri zetu wanakemea kwa maana ya uongozi, viongozi wa kisisasa wanayo dhamira njema ya kuisaidia nchi hii kwa sababu, tunaonekana kila mahali. Kwa hiyo, kupitia haya tumesomewa taarifa hapa, taarifa za Kamati zetu na naomba nijikite kwenye Taarifa ya Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza kwenye taarifa hiyo ambayo inaelezea upande wa *MSD* ambayo ni Mamlaka ya Dawa katika nchi yetu. Kupitia Ripoti ya *CAG* kumeonekana kuna upotevu au kuna madeni yanayokadiriwa kuwa bilioni 375, yaani *MSD* hawajalipwa, yaani wanadaiwa madeni yao. Walichukua dawa kwa washitiri, wakapata dawa wakazi-*supply,* hawajalipwa kwa maana wana madeni, kwa hiyo, imeonekana *CAG* ameona pale jicho lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama haitoshi hii inaathiri mtiririko wa utoaji wa dawa. Leo tunalalamika utoaji wa dawa katika vituo, kwa maana ya utoaji wa huduma katika Halmashauri zetu, hakuna dawa, ni kwa sababu, kuna mkwamo na Halmashauri zetu zimekuwa zikiomba dawa au kupeleka maombi ya kununuliwa dawa, bado haziletewi kwa sababu kuna deni kubwa liko pale wanadaiwa *MSD.* Hii maana yake nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii maana yake ni kwamba, tunasababisha tatizo la huduma kwa wananchi wetu kwa sababu tu, kuna baadhi ya watu hawajatimiza majukumu yao. Hili ni tatizo kubwa na *CAG* ametuonesha kwamba, kuna tatizo mahali. Kama tunadaiwa dawa za bilioni 300 ni wananchi wangapi wanakufa bila dawa vijijini? Ni namna gani Serikali inalaumiwa huko vijijini kwa sababu tu ya kikwazo hiki cha kudaiwa deni kubwa kiasi hiki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, maana yake ni kwamba, leo *CAG* ametuonesha kwamba kuna tatizo mahali. Ndio maana leo wananchi wakienda kwenye zahanati zetu, hakuna dawa kwa sababu ya misingi hii ambayo tunaeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo la *MSD* hapa imeelezwa kwenye ripoti zote za miaka mitatu mfululizo 2019/2020, 2020/2021 na 2021/2022. Kuna jumla ya aina 2,540 ambazo zilipokelewa zenye thamani ya bilioni 295.76, dawa hizi zilipokelewa zikiwa zimebakiza miaka miwili kwisha muda wake, lakini kama haitoshi katika hizo dawa ambazo ni thamani ya bilioni 28.4 zilikutwa muda wake umeshakwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajiuliza, hivi hakuna wataalam ambao wanaenda kukagua kabla dawa hizo hazijaja nchini? Wakati wanakagua walikuwa wamefumba macho? Wakati wanakagua vyeti vyao vilikuwa vimefungiwa kabatini kwamba, ni wasomi? Watu hao walikuwa hawana roho ya Mungu wakati wanakagua dawa za bilioni 28? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu hao sio wazalendo wa nchi hii? Watu hao ni wageni kutoka nchi za nje ambao wanawaletea wananchi wa Tanzania dawa zilizoisha muda wake ili waje wanywe wafe kwa sababu, dawa ikiisha muda wake inakuwa sumu. Ndio maana nilisema wenzetu baadhi ya watumishi wa umma hawana nia njema na Taifa hili, kwa sababu wasingekubali kuona mambo haya yanatokea …

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtaturu kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Innocent Bilakwate.

**TAARIFA**

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba nimpe Taarifa rafiki yangu Mheshimiwa Mtaturu, watu hawa hawawezi kuona kwa sababu ya rushwa. Ukiona mtu ananunua dawa ya miaka miwili ku-*expire,* ujue hapo kuna rushwa na rushwa hupofusha haki isiweze kutendeka. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Miraji, Taarifa unaipokea?

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio maana kwenye imani mojawapo ya Chama Cha Mapinduzi inasema wazi kwamba, rushwa ni adui wa haki, sitapokea wala kutoa rushwa. Kwa hakika naomba kuiombea CCM iendelee kudumu madarakani kwa sababu inatoa miongozo mizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana ndugu yangu Bilakwate, ameniongezea maneno haya, nitakuja kuhitimisha mwishoni, hivyo kulazimika dawa hizi kuteketezwa, ziliteketezwa dawa za shilingi bilioni 28. Dawa hizi zimeteketezwa fedha za walipa kodi hawa wananchi wa Tanzania. Watu hawa ambao wengine wanatozwa kodi baadhi ya maeneno wanashurutishwa, hawalipi kwa kupenda wenyewe, leo fedha zao zimeenda kuteketezwa kwa uzembe wa watu wachache ambao wapo kama watumishi wa nchi hii na wanalipwa mshahara na masurufu makubwa kabisa. Jambo hili haliwezi kuvumiliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu inaenda kuwa *dumping area*. Maana yake kama watengenezaji dawa zinaendelea kuisha na kuna watu watapitisha ziletwe nchini maana yake nchi yetu inaenda kuwa *dumping area*, maana yake tutaletewa dawa zilizoisha na zitaletwa na zitakuja kuteketezwa na hakuna hatua itachukuliwa. Jambo hili haliwezi kupita kwenye macho ya Wabunge makini kama hawa wa Chama Cha Mapinduzi,

wakaacha jambo hili liendelee. Ni hatari kwa afya lakini ni hatari kwa mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye jambo la pili ni Wakala wa Manunuzi ya Umma *(GPSA)*. Wakala huyu alipewa jukumu la kununua magari ya Serikali lakini ukiangalia kwenye ripoti ya *CAG*, kuna baadhi ya maeneo amesema tumekuta magari hayajanunuliwa. Wananchi waliingia taharuki kwamba kuna gari zimelipiwa hazijaja nchini, wananchi wakajua tumepigwa, kumbe ni Taasisi hii ya *GPSA* inachelewesha kuleta magari nchini wakati fedha zimeshalipwa na Halmashauri zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, gari za taasisi 14 zilinunuliwa zenye thamani ya fedha zaidi ya shilingi bilioni 28 zilikuwa zimenunuliwa, zimeshalipiwa gari hazijaja nchini. Maana yake ni kwamba, kumekuwa na urasimu mkubwa. Mkataba unasema utaleta gari ndani ya miezi minne au sita lakini tumeendelea kuletewa gari baada ya miaka miwili mbele. Jambo hili haliwezi kuvumiliwa kwa sababu wakala huyu amekuwa ana jambo baya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, dogo sana, dakika moja ni pamoja na kwamba, kengele nimeisikia Mheshimiwa nakuomba dakika moja nimalizie kwa pointi yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukinunua gari Japan, tunapewa *offer* ya kufanyiwa *service* kilometa 70,000 lakini gari hiyo ikinunuliwa eneo lingine hakuna hiyo *offer*. Kuna gari nyingi zimenunuliwa Halmashauri hazina *offer* ya kilometa 70,000 ambayo ni hasara kwa Serikali. Ombi langu ripoti imesema, watu waliohusika wote hawana sababu ya kuendelea kuwa ofisini. Serikali ichukue hatua ili kuisafisha Serikali ya Chama Cha Mapinduzi, kumsafisha Mheshimiwa Rais ambaye halali usiku na mchana akitafuta fedha kwa ajili ya wananchi maskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana Serikali ichukue hatua, maazimio yote ya Kamati yazingatiwe na tuweze kuchukua hatua na kuifanya Tanzania sehemu salama. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nimemuita Mheshimiwa *Engineer* Ezra Chiwelesa, atafuatiwa na Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, Mheshimiwa Zuberi Kuchauka ajiandae.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti na mimi nachukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika taarifa ya Kamati hizi tatu *PAC, LAAC* na *PIC*. Napenda pia niungane na Wabunge wenzangu kupongeza Kamati hizi tatu kwa taarifa nzuri ambazo wameziwasilisha. *Summary* nzuri hata kama una usingizi unasoma utaelewa. Kwa hiyo, nawapongeza sana Wanakamati kwa kazi hii kubwa mliyoifanya kwa niaba ya sisi Wabunge wenzenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwenda haraka, mimi naomba tu kwanza nijaribu kuongea na Wabunge wenzetu ambao wameaminiwa wakaenda Serikali, maana nimeona jana hapa mtifuano ulikuwa mkubwa sana. Napenda tu niwaambie Waheshimiwa Mawaziri, sisi ni wenzenu. Kuna wengine walikuwa huku sasa hivi wamerudi tuko nao huku, labda wengine watatoka wataenda huko. Tunawapenda zaidi kuliko hao *the so called* wataalam wanaojaribu kuwaambia *sometimes* tunasema jambo hapa, unasema wataalam waliniambia hivi na sisi kabla ya kuja humu Bungeni tulikuwa wataalam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo simaanishi kwamba tulivyoingia Bungeni humu akili zetu tulizokuwa nazo huko nje zimeisha, sasa hivi tumebaki *dull* kama hatujui chochote. Kuna Madaktari wengi sana humu, kuna Maprofesa wengi sana humu, kuna Mainjiania, kwa hiyo, tunaposhauri tunaomba mtupe nafasi ya kutusikiliza na ushauri wetu muupokee. Kwa sababu, ushauri huu ni wa kuisaida nchi. Tuko huko tunapambana na mambo haya yanapotokea, sisi ndiyo tunarudi Majimboni kwenda ku-*defend* Serikali yetu ya Chama Cha Mapinduzi, bila kujali yaliyofanyika huku, tunaenda kuwaambia wananchi nini kimefanyika. Ndiyo maana halisi ya taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii haiji kusifia. Ukiangalia ukurasa wa tatu wa taarifa hii inasema, "Kushughulikia maeneo yenye matumizi mabaya ya fedha." Kwa hiyo, ndugu zetu

tunayoyasema haya ni matumizi mabaya ya fedha, myasikie hata kama yanaumiza, ndiyo haya! Ndiyo kazi ya taarifa hii.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema haya mwaka jana wakati nachangia taarifa hii, *TANROADS* walikuwa wamesababisha hasara ya riba shilingi bilioni 68 na tukasema hapa. Mwaka huu shilingi bilioni 36, *in two years* shilingi bilioni 104. Zaidi ya bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara. Hizo ni riba tu zinaondoka. Hatuwezi kwenda namna hii! Ifikie hatua pale tunaposhauri msikie na mkafanyie kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa bajeti nilishauri hapa mwaka huu, nikasema haiwezekani mtu anatangaza bajeti na *tender* anaanza kutangaza, Wizara ya Fedha haijatoa kibali. Maana wewe unamaliza kitangaza kwenye Wizara ya Kisekta, umeshatangaza watu wamefanya kazi unanyanyuka na *certificate* kwa Mheshimiwa Mwigulu, Mheshimiwa Mwigulu unafika pale anakwambia, nimelipia *SGR* sina hela, zinaanza ku-*count* huku! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunayoona ni upande wa *TANROADS* tu, wapo watu wanafanya miradi ya maji hapa hawajalipwa zaidi ya miezi 12. Jana Waziri wa Ujenzi ameongelea Wakandarasi kulipwa kulipwa hiyo shilingi bilioni sabini, sabini, anaongea wanaofanya kazi *TANROADS* na Wakandarasi wengi wa Kitanzania maskini hawa, wako kwenye miradi ya maji na huko kwenye miradi mingine. Kwa hiyo, pesa wanazodai ni nyingi sana. Tujaribu kusaidia Watanzania hali kadhalika tuokoe hizi pesa. Kwa sababu, uhakika nilionao, kwenye hizi shilingi bilioni 68 na shilingi bilioni 38, hakuna mkandarasi wa Kitanzania hata mmoja anayelipwa riba! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata mimi ni Mkandarasi, sijawahi kulipwa riba, nadai hela zangu huko. Hizi pesa zinaenda kwa Wakandarasi wa kigeni! Sasa, Watanzania ambao mnaona ni wengi wanafanya kazi hizi, wako wanaumizwa lakini wageni tena wakija wanachukua hizi pesa wanaondoka nazo. Kwa hiyo, naomba hili tuliangalie sana tuweze kuwasaidia hawa watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo nataka kuongelea, nilikuwa napitia hii ripoti kidogo ukurasa wa 21. Kuna hawa watu wanaitwa *TANOIL*, yaani mtu anaamua tu kutoa *discount*, anaamua kuweka bei tofauti na *EWURA*, hawana uchungu na hivi vitu! Anajua hata tukipiga kelele humu na sasa hivi wanatuangalia, hii si ya mwaka 2021/2022? Bajeti tuliyopitisha mwezi wa sita, leo si ni mwezi wa 11 huu? Miezi minne imeshapita, hawa jamaa wanatuangalia tu hata huko nje. Wanajua watapiga kelele baada ya hapa ngoma imefungwa inaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *CAG* akija kukagua, miaka mitatu minne ndiyo tunaelekea kwenye uchaguzi, wanatuangalia tu. Sasa, mimi naomba Bunge hili tutoke na maazimio yenye maana zaidi. Maazimio ya kusaidia nchi hii. Kazi ya *CAG* ni kudhibiti na kukagua lakini nafasi ya udhibiti anakuwa nayo? Kama huwezi kufanya *real time auditing*, leo tunajadili kitu kilichotokea mwaka 2021/2022 hawa watu walishajenga majumba, walishahamisha hizi hela ziko huko nje, wengine walishaondoka, unawatoa wapi? Mwingine kahamishwa Wizara kaenda huko, unawatoa wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba, kwa sababu ripoti hii kwa sehemu kubwa inachokisema ni kwenye Mashirika ya Umma, mimi nitakuja na *proposal* hapa kama utaipokea. Kwa sababu, nimeona hata huyu wa *TANOIL* alikuwa anakiri kabisa. Ni kweli *EWURA* hawakuturuhusu, ni kweli hatukufanya hivi. Kwa hiyo, unaona ni mtu yuko *comfortable*, yaani anafanya anavyotaka kama vile hili ni shirika lake nyumbani, hata nyumbani huko saa nyingine unakuwa na bodi kama una shirika lako, iweze kukusaidia kuendesha, lakini hapa hamna kinachofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo jingine, nimepitia ripoti ya *SGR* ukurasa wa 46. Mwaka jana wakati wa bajeti nilionya hapa, maana Waziri wa Fedha alitamka kiasi ambacho kinaenda kutumika kwenye *lot six*, kutokea Tabora kwenda Kigoma. Waziri wa Fedha akatamka *2.1 billion dollar*. Nikasema *2.1 billion-dollar* ukii-*convert* kwenye *rate* ya wakati ule, ilikuwa inakua kama *4.8 trillion shillings*. Nikamwambia lakini ukiingia kwenye *TANePS*, huyu

mtu ambae anapewa kwa *single source* alikuwa amewasilisha pendekezo la 6.6 *trillion shillings*. Nikasema, ni zaidi ya shilingi trilioni 1.84, ongezeko linaloongezeka kutoka kwenye kile alichokisema Waziri na kile ambacho kinafanyika kwenye *TANePS*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilijibiwa hapa kwamba, watakaa naye yule mtu apunguze zaidi ya asilimia 38 na bado abaki na faida. Mkataba ulisainiwa kwa ile ile 6.6 *trillion shillings*. Sasa, tunapokuwa tunashauri tusikilizwe. Tunapata muda wa kusoma na sisi tunauelewa. Hilo ndilo tunaloliomba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona hapa mabadiliko, mtu anakwambia ana *justification* ya kwamba ile *1.3 million dollar* inayoongezeka kwa kila kilometa, ni kwa sababu kumekuwa na *fluctuation* ya bei na vitu vingine na miaka imeongezeka. Ndugu zangu tuko hapa, *TANROADS* wako hapa na Waziri wa Ujenzi yuko hapa, mimi ni *Engineer* naelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara kilometa moja ya *double surface* inajengwa kati ya shilingi bilioni 1.5 mpaka shilingi bilioni 1.8. Mbona hizo kwenye barabara haziongezeki ikawa shilingi bilioni 3? Huku kwenye reli peke yake ndiyo zinaongezeka? Kwani reli hazijengwi na madaraja? Lami haibadiliki bei? Sasa, vitu hivi mkija kufanya hapa muelewe na sisi wengine tuna akili tunasoma, msitufanye hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ambacho ninacho, mimi naomba nitoe ushauri sasa kwa kumalizia ili muda usiishe. Tangu mimi niko huko nje, kila ripoti ya *CAG* inaposomwa hapa, wizi, wizi, Mawaziri hawa watafukuzwa mpaka lini? Kuna Mawaziri wengine hata hawakuwepo wakati ule, walikuwa huku nyuma, wameshaenda huko mbele mambo haya yanaendelea. Hawa Watumishi wa Umma wamekuwa na *comfort zone* ambayo wanahangaika nayo, hamtakuja mkae muwaguse hata siku moja. Kwa sababu yeye ana uhakika Waziri ataondoka yeye atakuwepo pale! Kama Katibu Mkuu atahamishwa, yeye atakuwepo pale! Sisi tunakuja kwa kuchaguliwa. Ni kwa nini Wabunge mnakuwa *committed* kufanya kazi zenu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo wananchi wanatu-*monitor* huko nyuma. Ni kwa sababu tuna *timeframe* ya *five years*. *In five years* umechemsha wananchi wanakusubiri huko nje wakakupe adhabu yako. Ni kwa nini Watumishi wa Umma nchi hii tumewaacha waka-*relax* kiasi kwamba wao ndiyo wamiliki wa hii nchi? Tunaenda kuomba kura kwa wananchi tunawaahidi kufanya. Tunakuja hapa watumishi wanatuangusha. Ni kwa nini iwe hivyo? Chama cha Mapinduzi kinasemwa, viongozi wanasemwa, tutarudi huko nje tukahukumiwe lakini kuna watu wamekaa maofisini. Wako nyuma hawajawahi kuonekana. Wao ndiyo wanaotufanya tukaenda vibaya kwenye hii nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima ifikie hatua Watumishi wote wa Umma kuanzia ngazi ya Wakurugenzi, wapewe mikataba ya miaka mitano mitano, isizidi hapo. Kazi zitangazwe watu waombe. Sijawahi kusikia kampuni ya mtu binafsi hata siku moja kila siku inapata hasara, akawacha watu waendelee kuwepo. Wakina Bakhressa wanakua leo, kwa nini wanakua? Umepewa *job descriptions*, umepewa mkataba, umefeli wanakuondoa wanaleta mtu mwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona leo akina Rostam wanakua mpaka wanafungua viwanda huko nje, hawajakua kwa sababu waliwabeba watu, *There is no permanent employment* ukatengeneza faida, kuwe na *proper job descriptions*, kazi zile zionekane, waambiwe kabisa ukikosea hapa miaka mitano unaondoka. *(Makofi)*

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ezra, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Nusrat Hanje.

**TAARIFA**

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa mzungumzaji, anachokizungumza nakubaliana naye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi mwizi ni mwizi tu, ameiba na suti, ameiba na *system*, ameiba na begi, kaiba na *jeans*, mwizi ni mwizi. Tunajua ya kwamba mwizi anatakiwa afanyiwe nini. Mimi nafikiri tuwe *realistic* kidogo. Tumekuwa tunazungumza sana kuhusu ripoti za *CAG* na anachokizungumza pia ni ushauri mzuri, lakini kwenda kusema tunyongwe na vitu vingine, nafikiri tuwe *realistic*. Kwanza, hawa ambao wanatajwa wametajwa wanajulikana, ripoti zimeandikwa, tuwaone angalau kuna kesi zinaendelea Mahakamani, mchakato unaendelea Mahakamani ili wengine wawe wamefungwa, tuache kwenda mbali sana, tuangalie hawa, kwa sababu tunawaweza na kweli inaumiza sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ezra muda wako ulikuwa umeisha, basi malizia tu, muda wako umeisha. Taarifa hiyo unaipokea?

**MHE. ENG. EZRA J. CHILEWESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napokea taarifa. Kwa kumalizia naomba kitu kimoja ambacho nataka nishauri tufanye kama Bunge na tutoke na maazimio.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ezra kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisimama tu niliona *alignment* ya anachokisema Mheshimiwa Chiwelesa na walichokisema Wabunge wengine juu ya hatua zinazochukuliwa au zinazopaswa kuchukuliwa, pia, ameongea Mheshimiwa hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa vile hatupendi kuingilia michango ya Waheshimiwa Wabunge, ninataka niwahakikishie kwamba tunavyo vyombo *very competent* katika nchi, vinachukua hatua na sisi sote tunaona taarifa na ripoti za vyombo

hivi huwa zinaletwa humu Bungeni. Waheshimiwa Wabunge zile ripoti za vyombo vinavyofanya kazi zake hasa kwa mfano TAKUKURU, tuwe tunazisoma, tuwe tunazipitia. Tungeweza kujua hata angalau kwa hatu gani tumepiga hatua katika kushughulikia changamoto mbalimbali za uadilifu lakini za uaminifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, itafika wakati wa sisi Mawaziri tuta-*respond*. Tunaogopa sana kuwaingilia Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, tunapoongea, ongeeni kwa kiasi kwa sababu, tusiboboe sana, siyo kwamba hatuna nchi, siyo kwamba hatuna *system*. Kazi zinafanyika na tutatoa ripoti hapa kesho kama zamu yetu itafika, Mawaziri tutasema kazi gani zimefanyika.

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mulugo, hakuna taarifa juu ya taarifa. Mheshimiwa Chiwelesa malizia mchango wako. *(Kicheko)*

**MHE. ENG. EZRA J. CHILEWESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa naipokea. Kwanza labda nimwambie tu Mheshimiwa Waziri nina *10 minutes* tu ya kuongea hapa. Nikianza kuchambua tu huku ninao uwezo wa kuongea dakika ngapi na nikatoa maelezo yangu ambayo naona ni mawazo yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, Bunge linapomaliza hapa likaielekeza Serikali, Seriakali siyo kusema haichukui hatua, mkishachukua hatua TAKUKURU mmempeleka mtu Mahakamani, maana yake Bunge na Serikali mnakaa pembeni, yule mtu kapelekwa Mahakamani ni Muhimili mwingine hamtaingilia kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale watu ndiyo maana tukishawatoa hapa hatuwagusi kule, wanaenda kwenye haki wanapambana na wanasheria, wakishinda keshi wanakuwa huru. Ndiyo maana nasema, *we have to give them three years contract, five years contract*, akichemka *terms* zake ziko pale mnapambana naye huko, ameshatoka kwenye mfumo wa ajira ili Watanzania wengine waliosubiria huko nje wasio na kazi waje hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu wana uwezo, wako huko nje, mtu anashikilia nafasi mpaka anastaafu miaka 60! Wewe leo unateua Bodi…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA** Mheshimiwa Mwenyekiti namalizia. Unataka tufanye biashara sawa, unateua Bodi mtu kastaafu, unaenda unamwambia aongoze Bodi, Katibu wa Bodi ndiyo Mkurugenzi pale, kuna nini hapo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ezra, ahsante.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, atafuatiwa na Mheshimiwa Zuberi Kuchauka na Mheshimiwa Ndaisaba Ruhoro ajiandae.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** *Bismillah*! Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi ambayo umenipa na mimi nichangie kwenye taarifa hizi za Kamati tatu za *PAC, LAAC* na *PIC*. Pia, natamka wazi mimi natokana na Kamati ya Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza mchango wangu wa leo napenda kwanza kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jinsi ambavyo anaendelea kufanya kazi vizuri na maelekezo yake kwa ujumla wake, Wasaidizi wake wanayafanikisha kwa kiwango kinachofaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo maneno ya awali tu, moja, ninayo *slogan* mwenyewe ambayo nimewahi kui-*induce* kwa marafiki zangu Waheshimiwa Wabunge wengine, ikiwa inaitwa 'Kumtenganisha Mheshimiwa Rais na Mafisadi, kumtenganisha Mheshimiwa Rais na wezi!' Hii ni *slogan* yangu ya muda mrefu sana. Leo nimefurahi Kaka yangu Mheshimiwa Ole-Sendeka

ulipopata nafasi ya kutoa taarifa, ukasema uwatenganishe Waheshimiwa Mawaziri na wezi. Ukarudi chini kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, hapa niko tayari kutofautiana na haya maneno uliyoyaweka hapa. Mimi ninaamini Makamisaa wetu tumewapeleka kwenye Wizara mkamsaidie Mheshimiwa Rais, mkatusaidie Wabunge. Ndiyo maana mmekwenda wachache kule. Sasa, tunapofika sehemu na wewe pia tukutenganishe na hawa mafisadi, hao mafisadi tukawaita ni Maafisa Masuuli na Wasaidizi wao, sasa wewe unakuwa uko wapi? Umepewa *instruments* zote, una uwezo wa kuwafanya vyovyote katika Wizara ambazo mnazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nawaomba sana, ninyi pamoja na Wizara zenu mumsaidie Mheshimiwa Rais ili aweze kufikia yale ambayo anayatarajia.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Issa kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nafahamu ninayempa taarifa ni mtu anayejua *Local Government* vizuri sana, ni mtoto wa *Local Government. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria zetu za Fedha za *Local Government,* sisi tuliopo humu ndani ni Wajumbe wa Kamati ya Fedha za Halmashauri za Serikali za Mitaa, *kwa hiyo, mapungufu yote yanayotokea kule hata sisi humu ndani ni sehemu yake.* **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo....

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe taarifa...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, aah, taarifa!

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, ninaomba tusikilizane.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Waziri, utaharibu ushirika wa Bunge ....

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Simbachawene endelea.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** *Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Mtemvu kwamba iko haja, hatuwezi kutenganisha ni lazima wote tuwajibike, haya yanayotokea leo wote tunawajibika.* **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtemvu endelea na mchango wako.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wangu kwanza ndiyo uwe muhimu lakini kwa heshima kubwa ambazo huwa ninampatia za asilimia mia moja kaka yangu Mheshimiwa Simbachawene..

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtemvu na Waheshimiwa Wabunge, taarifa ni sehemu ya muda wako wa mchango, kwa hiyo, endelea na mchango wako.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, viongozi wetu wana muda wao wa mwisho wa kuhitimisha, ambao watapata nafasi ya kutujibu vizuri lakini kwenye hili ambalo ili nipokee hii taarifa, ninataka kumwambia ni kweli anachokisema, Waheshimiwa Madiwani ni sehemu ya maamuzi kwenye *Local Government*, vipi kwenye Serikali Kuu? Mimi nimesema hapa ni Mjumbe wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali, siyo *Local Government*, haya madudu ambayo sijaanza hata kuyasema yanatokea Serikali Kuu, huku sisi ni nani kule kwenye Serikali Kuu? Ni ninyi ndiyo mpo huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, taarifa hiyo ni nzuri, lakini kwenye upande mmoja wa *local government* ambapo ameniambia mimi pia ni mshiriki kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine la maneno ya jumla, kwa sababu sijaanza kuchangia, ni heshima kwa chama changu. Haya mambo ambayo yanatokea hivi kwenye kamati zote, heshima ya chama changu kwenye umma *(public),* mnaitikisa, kwa hiyo, yanatuuma sana. Ziada, ni heshima ya taarifa ya *CAG* kwa umma. Taarifa zina miaka zaidi ya mitatu au minne, *business as usual*. Hatuwezi kwenda hivi kama Taifa. Hoja zinakuja, majibu ni changamoto, wananchi wanapokea mwezi wa Tatu, tunakuja kujadili mwezi wa Kumi na Moja, na mambo bado hayaendi, tunaendelea kubishana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tujitahidi sana. Waheshimiwa Wabunge wengi wameelekeza au wametamani leo watoke na maazimio au kesho ambayo kwa kweli *public* itatuelewa. Sasa baada ya maneno yangu hayo ya jumla, nitatamani kuchangia katika maeneo mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la kwanza ni *Tanoil*. Kwenye taarifa humo naona hata nimenukuliwa huko. Ndani ya Kamati, nafikiri hapa nilikaa nao vizuri sana. Kwa sababu wengi wamezungumza kwa ujumla wa changamoto ziliyotokea ndani ya *Tanoil,* wala sitaki kufika huko. Kwa sababu najua yameshaingia vizuri kwenye *Hansard*. Nitazungumza eneo dogo ambalo wengi hawajalizungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na upungufu wote huo, moja, hakuna *monthly reconciliation* ambayo ilitusababishia tupate *opportunity loss* ya shilingi bilioni 1.8. Vile vile zaidi ya tani mbili, shehena mbili za mafuta za thamani ya shilingi bilioni 16.2, ambazo tungeweza kuzipata, tumeshindwa kuzipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la tatu ni hiyo ya *underpricing* ambayo watu wameielezea, kwamba *underpricing* na hii niitolee tu mfano, niwaambie tu vizuri kwamba ipo hivi, mwaka 2022 *Tanoil* palikuwa kuna bei ambayo, na ndiyo mwaka ambao tumefanya biashara vizuri. Kwa sababu mwaka wa nyuma yake tumefanya biashara kwa miezi miwili tu na ndiyo maana tulikuwa na *loss* ya shilingi milioni 166, lakini mwaka huu tunazungumzia *loss* ya Shilingi bilioni 7.8 ni kwa sababu *full year* (mwaka mzima) tumefanya biashara vizuri, lakini shida hapa imetokea nini? Kuna bei elekezi shilingi 2,610, hiyo ndiyo *EWURA*. Wao wakaenda kuuza chini ya shilingi 78.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelekezo wanayo, haki ya kupunguza kwa *percent* kutoka ile *base* ya *EWURA*. Kwa hiyo, hiyo ni *management standard,* hawakuitii, lakini hata ile ya *EWURA* hawakuitii. Kamati ilihoji juu ya kibali, lakini ikumbukwe sana *Chief Internal Auditor* wa *TPDC, parent company* alikiri kuwa walikuwa hawana kibali. Kuna mmoja akasema, sasa kama mpaka watu wanakili kwa sentensi moja, "hatukuwa na kibali na tumefanya." Sisi bado tunawatafuta hawa? Kwa hiyo, tunawatafuta wa nini? Yyaani mambo yako wazi kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya utetezi wao, wakasema walikuwa hawana wataalamu huko siku za nyuma, lakini najua *CAG* amepata wapi haya? Kuna mmoja alisema kule juu ya kwenye tozo na tuzo, Polisi kule. Kuna sehemu kuna watu, vijana wazalendo sana. Nataka niseme kwa sababu kwenye ripoti ya Kamati yetu tumesema iende *forensic audit* kule, wakafanye ukaguzi wa kiuchunguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna mtaalamu, kijana mdogo mwenye *CPA* yupo pale, ameenda kuwasaidia kutengeneza hizi hesabu, kaenda kuziona, madudu yote haya kayaona. Wamemwondoa, wamempa akasome magazeti, tena

kwa kumuumiza kweli! Hatuwezi kufikia hapa. Hii mifano ipo, amezungumza kule Mheshimiwa Ester Bulaya, lakini ikumbukwe kwenye michango ya nyuma kidogo kaka yangu wa Kigoma Mjini aliwahi kumzungumzia Meneja wa *TRA* mipakani na baadaye mkamrudisha. Watu wanafukuzana. Mdogo wangu Mheshimiwa Mrisho Gambo, amewahi kumzungumzia hapa *Internal Auditor* mmoja Arusha, vijana wazalendo ambao tunatamani watusaidie kama Taifa ambapo ninyi mpo huko kama wasimamizi, hamwezi kuwasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, si hata *management* mngeshaona kuna kijana kaumizwa, kwa nini katolewa? Mimi ningelikuwa ndio nipo mle ndani kama Kamisaa, huyu ndio angekuwa *Manager of Finance* au *Director of Finance* wa pale, kama siyo sehemu nyingine. sasa mnaenda kuwaumiza. Kwa hiyo, hiyo haikuwa na afya sana. Kwa hiyo, natamani sana Mheshimiwa Waziri mfuatilie, yupo mtu kaumia juu ya kutoa siri ya jambo hili. Kwa sababu tunapeleka uchunguzi kule, mtakuja kukuta hasara imeenda mara 12. Siyo Shilingi bilioni saba tu, zaidi ya Shilingi bilioni 60 kwa mwaka ujao, na mtakuja kunikumbuka na kwenye *Hansard* itabaki kumbukumbu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili. Ni riba ya shilingi bilioni 113.8 ambayo anadaiwa *TANESCO* na kampuni ya *Pan Africa Energy*. Upo mkataba ambao umeingiwa kati ya *Pan Africa Energy* na *TANESCO* kwa ajili ya matumizi ya gesi, lakini mkataba huu una-*requirement* yake ambayo wameekeana, kwamba kila ankara ya mwezi inapozalishwa inatakiwa ilipwe katika muda waliokubaliana. Kutoilipa kwa wakati, maana yake nini? Maana yake kutakuwa kuna riba ya asilimia nne na hii riba inakuja juu ya *LIBOR rate*. Maana yake ni nini? Kama riba ni asilimia nne na mwaka huo hii *London Inter-Bank Offered Rate (LIBOR)* itakuwa yenyewe ina-*vary,* siyo *fixed*. Kwa sasa ni asilimia 5.1, inasababisha tulipe asilimia 9.1. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzia Mkaguzi anaenda kukagua kwa huu mwaka 2021/2022 wa hesabu, zipo ankara 115 hazijawahi kulipwa. Maana yake nini? Maana yake ukiondoa deni halisi ambalo *TANESCO* analijua la kama Shilingi bilioni 245, tayari ndani yake kuna riba ya Shilingi bilioni 113. Hizi ni fedha nyingi

sana. Maana yake kila mwaka ina-*accumulate* riba ya Shilingi bilioni 11. Sasa shilingi bilioni 11 kwa mwaka hizi fedha, mimi Mbunge wa Jimbo la Kibamba Wilaya ya Ubungo, Wilaya ya Changamoto, ndugu zangu hapa ningekuwa na zahanati ngapi? *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Mtemvu, malizia mchango wako. Muda wako umeisha.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima niseme ukweli…

**MWENYEKITI:** Malizia sentensi ya mwisho Mheshimiwa, muda umekwisha.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaunga mkono hoja, nina ushahuri wa dakika moja. Ni kwamba, tuangalie mamlaka zote za uteuzi, muangalie *qualification* za watu *rather than nepotism* ili Taifa hili liweze kwenda mbele. Vinginevyo, hatutaweza kufika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mtemvu.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, atafuatiwa na Mheshimiwa Ndaisaba Ruhoro, na Mheshimiwa Joelson Mpina ajiandae.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Mwongozo wa Kiti, Mheshimiwa.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama chini ya Kanuni ya 76, kuomba mwongozo wako kwa kauli ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, rafiki yangu ninayemheshimu sana, *Comrade* Simbachawene kuhusu kuwahusisha Waheshimiwa Wabunge, kwa kitendo cha Wabunge kuwa Wajumbe wa Mabaraza ya Madiwani, kusema kwamba sisi ni sehemu ya uhalifu huo unaoendelea dhidi ya rasilimali za nchi hii katika halmashauri zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maafisa Masuuli katika Halmashauri ni Wakurugenzi Watendaji na wanawasaidizi wao hapo chini, na hao ndiyo wanaokaguliwa. Kama kuna jambo ambalo Madiwani wamepitisha kinyume cha sheria, itatamkwa kwamba tumepata hasara hii kutokana na maamuzi ya Madiwani yaliyokiuka sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ripoti tuliyonayo leo, sijaona mahali paliposema Madiwani wa Halmashauri fulani wamelazimisha fedha ziende katika eneo lingine. Kwa hiyo, kwa lugha nyepesi ni kwamba, waliohalifu dhidi ya rasilimali za nchi ni Maafisa Masuuli katika halmashauri zetu, Watendaji wa Maafisa Masuuli katika Wizara na mashirika ya umma ambayo wenye dhamana ya kuwasimamia ni Mawaziri waliopo katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo tukasema ni vizuri Mawaziri wajipambanue kujitenga na wahalifu wale kwa kuchukua hatua kwa wale waliopo chini yao wakiwemo Wakurugenzi, maana Madiwani siyo mamlaka ya mwisho ya Wakurugenzi, wao wanapendekeza tu, na wanaweza kupendekeza wakahamishwa na wasichukuliwe hatua nyingine yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilitaka kulinda heshima ya Bunge hili katika uhalisia, siyo kwa maana ya kufunika. Bunge hili siyo sehemu ya uhalifu katika ripoti hii ya CAG. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuomba mwongozo wako kama sisi ni sehemu katika jambo hili?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, ahsante umeeleweka.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Ole-Sendeka amesimama kwa mujibu wa Kanuni ya 76 akiomba mwongozo wa Kiti kama jambo lililosemwa na Mheshimiwa Waziri wa nchi, linaruhusiwa au haliruhusiwi.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa kanuni zetu, naweza nikatoa mwongozo sasa au baadaye. Kwa hiyo, nitatoa mwongozo baadaye. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Namwita Mheshimiwa Kuchauka, atafuatiwa na Mheshimiwa Ruhoro, na Mheshimiwa Luhaga Mpina, ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nizungumze. Namshukuru sana Mwenyezi Mungu aliyenipa kibali cha kusema haya nitakayoyazungumza.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tuwe wasikivu, naomba tusikilizane. Waheshimiwa Wabunge, naomba tusikilizane, mwenzetu anachangia.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, niseme neno moja kwa utangulizi. Neno 'dharau,' nitalifafanua kidogo huko mbele. Ipo dharau kubwa kwa watumishi wa Serikali ngazi za Wizara na ngazi za halmashauri kwa wanasiasa. Leo sisi tupo hapa, leo ni siku ya pili na hii hoja inakwenda siku ya tatu. Tutajadili humu, tutanyukana humu kadiri tutakavyonyukana, ukitoka nje kwenye makorido, hawa watumishi wa Serikali wanakwambia, hawa ni wanasiasa bwana, hizo ndiyo kazi zao. Ina maana kila kitu kinakwenda kama kawaida, hawabadiliki. Wanasema hizi ni kazi za wanasiasa. Kwenye kundi hili, Mawaziri hampo salama, ni kwamba na ninyi mnaonekana ni wanasiasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Serikali, lazima hatua zichukuliwe na zionekane zimechukuliwa ili dharau hii nayo iweze kuondoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuunga mkono hotuba zote za Kamati zote tatu, naunga mkono azimio la ziada lililotolewa na Mheshimiwa Waitara, Mheshimiwa Deo Sanga na jana Mheshimiwa Maganga na aliyomalizia Mheshimiwa Chiwelesa. Naunga mkono maazimio hayo yawemo kwenye maazimio ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kuchangia kuzungumzia mapato ya halmashauri zetu. Ni jambo lisilopingika, ndani ya miaka hii miwili hakuna halmashauri ambayo imepata chini ya shilingi bilioni 10 kutoka Serikali Kuu. Hiyo ni nje ya mapato ya ndani. Fedha hizi zinatafunwa, hakuna asiyejua. Naomba niwaulize, *Accounting Officer* wa fedha hizi mabilioni ni nani? Huyu Mkurugenzi amepatikanaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu namwona Mkurugenzi anatumbukizwa kwenye bwawa lenye mamba, kwa sababu yupo Mhasibu kwenye halmashauri ana miaka sita au saba; yupo Mkaguzi wa ndani kwenye halmashauri ana miaka sita au saba; yupo Afisa Manunuzi, ana miaka sita au saba. Leo unampeleka Mkurugenzi ambaye alikuwa Mwalimu akagombea Ubunge, mkampeleka pale akawa Mkurugenzi. Salama yake pale ni nini? Kwenye mamba wale, salama yake ni nini? Ni kuungana nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, twende mbele tuangalie, huyu Mkurugenzi ana-*know how* ya Uhasibu? Anajua mambo ya mipango? Anajua manunuzi? Anajua ukaguzi? Kama hajui, na wale ndio wakongwe pale, na hii inaenda mpaka mawizarani. Mheshimiwa Waziri, uliyechaguliwa leo, unaingia kwenye Wizara unakuta watu kwenye Wizara ile ndio mama wa Wizara. Mwezangu nami ili uweze kudumu kwenye ile Wizara, umefanya nini? Uungane nao. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu, narudi kwenye halmashauri. Huyu *DED* ambaye tumempa madaraka makubwa sana, hivi kweli Mhasibu wa Halmashauri, Mkurugenzi ni mamlaka yake ya nidhamu? Afisa Manunuzi, Mkurugenzi ni mamlaka ya nidhamu? Mamlaka ya nidhamu tumehamishia kwa Madiwani. Mkurugenzi anapeleka kesi kwa Madiwani. Madiwani wanasema hapana, huyu hana kosa, anarudi. Hivi Mkurugenzi huyu na huyu Mhasibu ambaye alimshitaki amerudishwa. Kuna kazi! Lazima eneo hilo tulifanyie mabadiliko. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwaambie, suala la uadilifu, kwamba tumpeleke mtu mwadilifu, hakuna. Huyo Malaika hatapatikana. Watu wanaishi kwa mifumo, kwa kusimamiwa. Lazima tutengeneze mifumo ya watu kuwasimamia, lakini kuwaacha kwa kusema kwamba kuna watu wenye nidhamu wenye uchungu na nchi hii, hawataiba, siyo kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, naomba nizungumzie suala lingine kwamba Mheshimiwa Rais amepeleka fedha nyingi sana kwenye halmashauri zetu. Kwa kuona usimamizi mbovu uliopo kule, amemteua Naibu Katibu Mkuu wa miundombinu aende akasimamie hizo fedha kule. Kwenye halmashauri zetu, hiyo idara ipo. Kwenye halmashauri hiyo idara ya Naibu Katibu Mkuu wa Miundombinu ipo? Kama ipo, ina watumishi? Jibu ni hakuna. Lazima kama huku juu kuna Naibu Katibu Mkuu wa Miundombinu, nataka nimwone kule kwenye halmashauri, kuna Mkuu wa Idara ya Miundombinu na ana nyenzo za kutosha

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudi kwenye ukaguzi wa ndani. Nashukuru Mheshimiwa Zainab, amesema kwamba tumetengeneza kifungu kwa ajili ya Mkaguzi wa Ndani, lakini bado Ofisi ya Mkaguzi wa Ndani ipo chini ya Mkurugenzi. Haiwezi kuwa sawa. Wazo langu, Ofisi ya Mkaguzi wa Ndani iwe inajitegemea. Hawezi kwenda kuomba mafuta kwa Mkurugenzi, aende akaombe gari kwa Mkurugenzi, halafu yeye mwenye anajibu kwa Mkurugenzi, na Mkurugenzi huyo ana uwezo wa kumshitaki kumpeleka kwa Madiwani akafukuzwa, halafu ndio

awe Mkaguzi wa ndani! Jambo hili mimi naona siyo sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajikita kwenye halmashauri. Ipo miradi ya Serikali Kuu kama nilivyosema, zaidi ya shilingi bilioni 10, 15, 20 zinakwenda kwenye halmashauri zetu. Hizi fedha zinapokwenda kule kwenye halmashauri zetu, zinataka zifanyiwe nini? Usimamizi. Usimamizi huu unafanywa na nani? Kweli Madiwani, sisi Wabunge, wote sisi kwa ujumla wetu ni wasimamizi, lakini nani ni *Accounting Officer?* Ni Mkurugenzi. Naomba hilo jambo lijadiliwe kwa umakini sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la watumishi. Kwenye halmashauri zetu pamoja na kupelekwa fedha nyingi sana, lakini bado kuna uhaba wa watumishi, hasa wenye taaluma hizi. Kama yule niliyezungumza, mtu wa miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu kuna tofauti moja nyingine kwenye halmashauri zetu, kuna fedha zinatoka Serikali Kuu na fedha za mapato ya ndani. Madiwani wanapanga matumizi ya mapato ya ndani, lakini Serikali Kuu inakwenda na maagizo kila siku kukicha. Halmashauri badala ya kutekeleza miradi waliyoipanga wenyewe, wanabaki kutekeleza maagizo kutoka Serikali Kuu, TAMISEMI. Huu ni mwanya mwingine wa watumishi hawa kula hizi fedha za halmashauri za mapato ya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni Diwani gani atakataa kupitisha fedha kwenda kumalizia kituo cha afya ambacho wananchi wanakitaka? Fedha zimepelekwa TAMISEMI, shilingi milioni 500, watu wamepiga, kituo cha afya hakijaenda. Mkurugenzi analeta maombi kwenye Baraza kuongeza shilingi milioni 200 kwenda kumalizia kituo cha afya. Ni Diwani gani atakataa kupitisha hiyo kituo cha afya kisimame? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hapa napo ni dirisha lingine la halmashauri kula fedha za umma. Wametafuna zile shilingi bilioni 10 za Serikali Kuu zimeisha, sasa wanaenda kushambulia mapato ya ndani. Jambo hili kwa maoni yangu twende tuliangalie, kama lina…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kuchauka, muda umeisha, malizia sentensi ya mwisho.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, basi kwa kumalizia, naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wote pamoja na hao niliyowataja, tuwajibike. Kwa Serikali tuweke mifumo. Hakuna Malaika wa kusema kwamba huyu tukimweka pale ndiyo atakuwa siyo mwizi. Mwizi analindwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kuchauka, tunashukuru.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kabla ya kuendelea kuna tangazo dogo hapa. Kuna wageni wa Mheshimiwa Mbunge. Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Eng. Mwanaisha Ulenge, ambao ni Ndugu Eng. Nancy Mduma, ambaye ni Katibu Taasisi ya Wahandisi Tanzania, Kitengo cha Wanawake na Ndugu Shamsia Danga kutoka Ujerumani, ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Utamaduni, Sanaa na Michezo wa *diaspora* duniani *(TDC Global)* na Mkurugenzi wa *DIWO* ambayo Makao Makuu yake yapo Tanga.

Nilimuita Mheshimiwa Ndaisaba Ruhoro, atafuatiwa na Mheshimiwa Joelson Mpina, Mheshimiwa Joseph Musukuma, ajiandae.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia. Tangu jana na leo asubuhi kila Mheshimiwa Mbunge, anayesimama kuchangia kuna watu wanashtuka. Naomba wale wanaoshtuka huko Wilayani, kwenye mikoa na hata humu humu Bungeni, wakae sawa sawa, kwa sababu haturudi nyuma hatuwezi kuvumilia hata siku moja, kuona pesa anayotoa Mheshimiwa, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kuna watu wanaitafuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna watu wanafikiri kwamba Waheshimiwa Wabunge walikuwa wanapoa poa *this time* mambo yamebadilika. Wale wanaosikia tunazungumza wanashtuka wakashtuke kweli kweli, kwa sababu tunakwenda kuwashughulikia. Wabunge tumeamua kufanya kazi yetu ya kulinda rasilimali za Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wenzangu wamezungumza na wameelezea umuhimu wa kuanza kushughulikia wezi wote. Mimi naomba mchango wangu niuelekeze kwenye kuboresha mifumo na taratibu za kikaguzi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na eneo la ushirikiano, maeneo mengi ambapo *CAG* anakwenda kufanya ukaguzi kwenye Taasisi. *CAG* amekuwa akifika pale anakuta kuna Wakaguzi wa Ndani wameshafanya kazi kubwa wamefanya ukaguzi wameandaa hoja, lakini kwa bahati mbaya *CAG* hafanyii kazi Taarifa za Wakaguzi wa Ndani. Matokeo yake unakuta *CAG* anatumia muda mrefu sana kufanya Ukaguzi na matokeo yake Serikali inalipa fedha nyingi. Jambo hili linaondoa ufanisi kwenye mchakato mzima wa Ukaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili, naomba niishauri Serikali, Serikali itoe maelekezo mahususi kwa *CAG,* anapokwenda kufanya Ukaguzi kwenye Taasisi iwe ni kwenye Halmashauri au kwenye Wizara, ahakikishe *CAG* anaanza kufanyia kazi Taarifa za Wakaguzi wa Ndani. Jambo hili litakwenda kuleta ufanisi litaokoa muda na litaokoa fedha za Serikali ambazo vijana wale wanalipwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo jingine ambalo ninataka kushauri na kuongelea ni kwenye uhuru wa utendaji wa Mkaguzi Mkuu wa Ndani, kwa maana ya *Internal Auditor General*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nikuambia huyu Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali anapewa fedha kutoka Wizara ya Fedha na anapewa fedha na Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha. Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha, katibu Mkuu - Wizara ya Fedha, ndiye anayetoa fedha kwenye halmashauri, Mamlaka zote za

Serikali za Mitaa na kwenye Taasisi za Serikali. Hawa *Internal Auditors* waliopo kwenye Taasisi wanaripoti kwa Afisa Masuuli ambao na wenyewe wanapewa fedha kutoka kwa Katibu Mkuu Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yake kinachotokea hawa Wakaguzi wa Ndani wamefungwa kamba. Hakuna hata siku moja watakuja kufanya kazi nzuri wafanye Ukaguzi ambao ni *independent* waibue madudu yaweze kushughulikiwa, kwa sababu ya mfumo na *set up* tulivyoiweka, Ofisi ya Mkaguzi wa Ndani nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapendekeza tuunde, Taasisi ya Ukaguzi wa Ndani, inayojitegemea ambayo haiingiliani na Maafisa Masuuli nchini. Huu ndio mwarobani pekee utakaowezesha, Ofisi ya Wakaguzi wa Ndani nchini kuweza kufanya kazi kwa kujitegemea na kwa kutoingiliwa. Kitendo cha kutofanya hivyo, kimesababisha mpaka hawa Wakaguzi wa Ndani kushiriki kwenye dili za kuiba na wao ni wezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani Mkaguzi wa Ndani yupo pale halmashauri anaripoti kwa Mkurugenzi watu wanacheza dili halafu yeye wakamuondoa wakamtoa mswaki, lazima na yeye apewe mgao. Lazima hii Taasisi ya Ukaguzi wa Ndani tuweze kuihuisha, tuifumue, tuitengeneze upya iwe huru na iweze kufanya kazi yake ya Ukaguzi sawa sawa, vinginevyo wizi utaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nataka kuchangia ni kwenye Kamati za Ukaguzi, zilizopo kwenye halmashauri. Kamati ya Ukaguzi iliyopo kwenye halmashauri inaundwa na Wajumbe wawili kutoka nje ya halmashauri, inaundwa na wajumbe wawili ambao ni Wakuu wa Idara zile za halmashauri. Mara nyingi wanavyowachagua wale wanawachagua wale wapigaji wanaojua kusuka dili, wale wanaojua kuchakata nyaraka, wale wanaojua kutengeneza dili pesa iweze kupigwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wajumbe wengine wa Kamati hizi za Ukaguzi wa Ndani ni Wakuu wa Idara hao wawili, Mwenyekiti

mmoja Katibu mmoja. Hii Kamati inayosimamia masuala ya Ukaguzi kwenye *council* na maeneo mengine inakosa nguvu thabiti za kuweza kusimamia masuala la ukaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka ni pendekeze mambo yote haya ya Ukaguzi ikiwezekana yafanywe na Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa na Wilaya chini ya Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa. Ninataka nikuambie Mkuu wa Wilaya akienda kusimamia pale akiwa Mwenyekiti wa hii Kamati ninayohusika kusimamia Masuala ya Ukaguzi hakuna mtu ataiba zile pesa pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakuta wamechaguana watu kwa dili wamepangana watu kwa dili wale wale. Kwanza, kinachofanyika pale watu wanatengeneza taarifa na nyaraka kwa ajli ya ku-*justify* tu. Watu wanapiga hela, ndio maana ukiangalia hizi taarifa namna ambavyo tumezipokea kwenye Taarifa ya *CAG*. Maeneo mengi pesa zimepigwa, kwa sababu ni *systemic* ni mfumo ambao umetengenezwa na bila kuubadilisha, bila kuufanyia marekebisho fedha zitaendelea kuibiwa na tutaendelea kulalamika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwezekana kama Kamati ya Ulinzi na Salama haiwezi kuhusika kwenye ule mchakato wakusimamia masuala ya Ukaguzi. Basi Mkuu wa Wilaya au Mkuu wa Mkoa, apewa mamlaka ya kwenda kushiriki kwenye zile Kamati. Kwanza, yeye ana *authority,* yeye ana nguvu na ni Mkuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama pale, anaweza akachukua hatua yoyote. Sasa matokeo yake tunasubiria pesa zinapigwa halafu tunakaa hapa Bungeni tunalalamika tunataka Serikali iagize sasa hivi vyombo vianze kushughulika na wezi walishaiba huko wameshajenga nyumba, wengine wameshahamishwa tunachelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ifike mahali tufanya maamuzi magumu kwenye nchi. Tuweke mifumo tuweke na watendaji tubadilishe, kwa sababu mambo hayaendi vizuri, ndio maana wizi unatokea. Twende kukafumue maeneo hayo tufanye mabadiliko ili tuweke watendaji watakaoweza kuisaidia, Serikali na watakaomsaidia, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mheshimiwa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mama

yetu ana kiu kubwa ya kuwasaidia Watanzania, mama yetu anajitahidi kutafuta fedha nje ya nchi lakini kuna watu wanazidonoa na kuna watu wanaziiba. Sasa ifike mahali waanze kushughulikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano ukiangalia kwenye *performance indicators* za Maafisa Masuuli nchi hakuna *performance indicator* ya kumfanya Afisa Masuuli nchini apimwe, ni kwa namna gani alifanyia kazi mapendekezo na hoja zote za ukaguzi. Ni kwa nini tusiongeze *performance indicators* kwa Maafisa Masuuli wote nchini? Ili wapimwe ni kwa namna gani walitekeleza Maagizo ya CAG kwenye Taarifa mbalimbali za Kiukaguzi zinazotokea kwenye maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kweli kama Taifa tumeshindwa kufika mahali tukawa *serious* tukafanya maamuzi na mambo yakatokeea. Ifike mahali sasa iwe ni mwisho, ifike mahali pesa ya Serikali watu wakiiona waikimbie kama vile umekutana na nyoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kipindi ilitokea watu walikuwa wanaona picha ya mtu fulani nyuma kwenye Ofisi akitaka kuiba hela akiona ile picha anashtuka. Ifike mahali ndani ya nchi hii mtu akitaka kula hela ya Serikali aweze kushtuka. Ninaomba kwenye *performance indicators* za Maafisa Masuuli wote nchi iongezwe kipengele cha kuwapima ni namna gani walishughulikia hoja zote za kiukaguzi zinazoibuliwa na CAG. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakaa hapa CAG anaibua vitu vingi anaviweka pale ili viweze kufanyiwa kazi. Matokeo yake hakuna kitu hata kimoja kinafanyiwa kazi, tunakutana hapa tunapiga keleke, tunakutana hapa tunalia. Fedha zinaendelea kuliwa wananchi wanakosa fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo na Taifa letu linakuwa linaendelea kwa kusua sua, kwa sababu kuna watu wachache wenye matumbo makubwa kuliko watu wengine wa wanajilimbikizia fedha, wanatafuna fedha za Serikali. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ndaisaba, kuna taarifa kutoka kwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange.

**TAARIFA**

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa mchango mzuri anaoendelea nao. Lakini tu nimpe taarifa kwamba katika *Key Performance Indicators* za Wakurugenzi ambazo tayari Ofisi ya Rais, TAMISEMI, ilishazifanyia kazi na kuwapa kwa maandishi. Moja wapo ni kuhakikisha kwamba wanadhibiti ubadhilifu katika fedha za umma katika halmashauri zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kuhakikisha kwamba wanakusanya mapato ya ndani kwa ufanisi unaotakiwa. Hilo Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi mara kwa mara mabadiliko ya Wakurugenzi yanapojitokeza tunaona Wakurugenzi wengi wanaachwa. Moja ya sababu ni pamoja na kutokidhi *Key Performance Indicators* pamoja na kutosimamia ipasavyo miradi na fedha za umma na Serikali itaendelea kufanya hivyo, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ndaisaba karibu, kupokea na umalizie mchango wako.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba akafukuze Wakurugenzi wote ambao hizi hela zimeibwa na wamepewa *performance indicators* hawajazifanyia kazi na hela zimeendelea kuibwa. Naomba Wizara na Waziri mwenyewe mhusika, kesho fukuzeni Wakurugenzi wote mahali kote ambapo fedha zimeoneshwa kwenye Taarifa ya CAG watu wameiba hela za Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahante Sana. Mheshimiwa Ndaisaba. Sawa, malizia.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba dakika moja tafadhali, naomba nimalizie hoja yangu kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa naomba mambo yafuatayo yafanyiwe kazi. Moja wezi wote waliohusika na kutajwa kweli Ripoti ya Mkaguzi wa Hesabu za Serikali, wakamatwe wapelekwe Mahakamani washughulikiwe na sisi hatuna huruma na wezi wanaokula fedha za Serikali hiyo ni moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbili, ninaomba Bunge lipitishe Azimio la kuhakikisha kwamba inaenda kufanyiwa *overhauling* Ofisi ya Mkaguzi wa Ndani, ili iweze kuwa *independent,* kwa sababu kwa *set up* na mfumo wa namna ambavyo Ofisi hii ilivyo kwa sasa, Ofisi hii haiko huru na matokeo yake hela za Serikali za Mheshimiwa Rais, zinaendelea kuibwa. Eneo hili linatakiwa liende likafanyiwe kazi liwe na Taasisi huru.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ndaisamba.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, japo sijamalizia yote. Naunga mkono hoja. Ahsante sana. Nitaonge wakati mwingine. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Ahsante. Nilimtaja Mheshimiwa Joelson Luhaga Mpina atafutiwa na Mheshimiwa Joseph Musukuma, Mheshimiwa Constantine Kanyasu, ajiandae

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza sana *CPA* Charles Kichere, kwa kazi nzuri sana yeye na timu yake ya Ofisi ya Ukaguzi kwa uzalendo aliouonesha. Kipekee pia ni mpongeze na kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuruhusu mawanda mapana ya ukaguzi na kukataa kabisa nchi yake kuwa pango la wezi, kuwa pango la wala rushwa, lakini kuwa pango la mafisadi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma taarifa ya *CAG* ya mwaka 2021/2022, nimesoma Taarifa za Kamati za Ukaguzi, nimesoma majumuisho ya majibu ya Serikali na Mpango wa Utekelezaji wa Taarifa ya *CAG*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majumuisho ya Mpango wa Utekelezaji wa Taarifa ya *CAG* ina kurasa 1,111; ukizisoma zote kwa pamoja huoni hatua mahususi ambazo Serikali imechukua mpaka sasa toka ripoti ya *CAG* itolewa Machi, 2023, hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi kusema hapa niliposimama Bungeni kwamba tumepoteza zaidi, tumepigwa zaidi ya trilioni 30 katika Ripoti ya *CAG* ya mwaka 2021/2022 na leo nasisitiza ni zaidi ya trilioni 230 na maneno haya yanathibitishwa na Taarifa ya *FIU* ambayo inasema zaidi ya trilioni 80 zimehamishwa ndani ya nchi na nje ya nchi, trilioni 280 na kati ya hizo trilioni 55.65 zimehamishwa fedha taslimu kupitia mipakani na maeneo mengine. Nyingine trilioni 222.81 zimehamishwa kupitia elektroniki. Sasa kama nchi hii masikini inawza kuwa taarifa shuku trilioni 280 usalama upo wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Kamati ya *PAC* kipengele cha 2.2.3.2…

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Luhaga, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuheshimu mchango anaochangia Mheshimiwa Mbunge ninaomba kumapa taarifa; moja ni miamala shuku ni *transaction,* siyo uhamisho, ni *transaction* zinazofanyika za *private sector* tu, anaweza akawa Mheshimiwa Kingu pale anaagiza mzigo wa vitenge Uganda, katuma halafu mhisani mmoja akataka kujua hiyo iliyokuwa inaenda kufanya vitenge ilikuwa nini, siyo uhamisho, ni shughuli za kila siku zinazoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika mwezi na katika mwaka ni dhahiri kwamba shughuli lazima zinaendelea na ni nyingi kweli na hatuwezi kama nchi tukazuia shughuli za kiuchumi katika nchi. Kwa hiyo, siyo wizi wala siyo uhamisho wa fedha ambazo zinatoka Hazina ama zinatoka kwenye Idara ya Serikali kwenda mahali fulani, ni shughuli za kiuchumi na anatokea mtoa taarifa ndio anatoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu la pili, ukisema umepigwa trilioni 30 wakati bajeti ya nchi ni trilioni hatujafika hata 50 na kwenye makusanyo ya mwaka mzima takribani trilioni ishirini naa ni mishahara inaenda kwa watu n a wanaipokea na trilioni 14 zinaenda kwenye miradi ya maendeleo; ukisema trilioni 30 naa zimapigwa namba zinakataa kwenye bajeti kwa sababu bajeti ya nchi hatujawahi kufika huko. *(Makofi)*

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa taarifa kwamba hzi nyingine ni shughuli ambazo zinakuwa zinaendelea.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Mheshimiwa Luhaga Mpina endelea.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza anamaliza muda wangu, halafu nashangaa Waziri wa Fedha ambaye hajui kazi ya *FIU*. Hajui kazi ya *FIU,* hajui miamala shuku maana yake ni nini. Kwa hiyo, sitaki taarifa yake na aniache niendelee kuchangia. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya *SGR* ya Kamati kipengele cha 2.2.3.2 katika *lot* namba 3 na *lot* namba 4; Kamati inakiri kwamba Serikali ilipoacha utaratibu wa njia ya ushindani ilipata ongezeko la dola za Marekani milioni 1.15 sawa na bilioni tatu kwa kilomita moja ya *SGR*. Kamati ina-*confirm* kwamba katika kipindi cha miaka mitano Serikali ilipokuwa inatumia njia ya ushindani kilometa moja ya *SGR* iliongezeka kwa shilingi bilioni 0.42 kwa miaka mitano. Serikali ina-*confirm* kwamba Serikali

ilipochukua utaratibu wa *single source* ikaacha uataribu wa ushindani bei ya kilometa moja iliongezeka kutoka bilioni 1.4 hadi bilioni 3.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia maelezo ya kwamba gharama ziliongezeka kwa sababu ya miaka sita ilikuwa imepiata siyo ya kweli kwa sababu mwaka 2020/2021 tulitangaza *tender* kwa njia ya ushindani ya Isaka - Mwanza ambayo *average* kwa kilometa moja ilikuwa ni bilioni 9.1 sawa na kipindi kile cha mwaka 2017 kwenye *lot 1* ambayo ilikuwa ni bilioni tisa. Kwa hiyo, 9 kwa bilioni 9.1 tofauti ya 0.1 tu. Kwa hiyo, *tender* hii ya *lot 3* na *lot 4* ilikuja kutangazwa baada ya mwaka mmoja tu 2020/2021 ikatangazwa mwaka 2021/2022 kwa hiyo maelezo hayo siyo ya kweli. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni kwamba lot namba…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mpina kuna taarifa kwa Mheshimiwa Naibu wa Waziri wa Uchukuzi Mheshimiwa David Kihenzile.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakubaliana anachokisema Mheshimiwa Mbunge mchango ni mzuri, lakini nilitaka pia nitoe ufafanuzi kidogo na taarifa kipi kinapelekea...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tuwe wasikivu. Waheshimi Wabunge, tuheshimu taratibu za vikao vyetu.

Mheshimiwa Naibu Waziri toa taarifa.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hii imezungumzwa kwa muda mrefu ambayo nampa taarifa Mheshimiwa Mbunge ya sababu zilizosababisha kutofautiana kwa

fedha kati ya *lot one* na *two visa vis three* na *four,* zipo hoja nyingi. Namba moja ukingalia kwenye *lot three* na *four* ilikuwa na *rift valley* kilometa 50, *one* tu haikuwepo; ukingalia kwenye *lot three* na *four* ilikuwa na *junction* pale kuna karakana, kuna Chuo cha Reli, kule havikuwepo; ukiangalia *three* na *four* kuna ujenzi wa kituo kikubwa ambacho kinakwenda mpaka Kigoma na kadhalika, huku hakikuwepo, lakini pia kuna eneo kubwa la *swamp*…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante. Mheshimiwa Luhaga endelea na mchango wako. Taarifa hizi unazipokea?

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hizo ni fujo atakuja kuzungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine, Kamati inakiri kwamba suala la kutumia mzabuni mmoja lilikataliwa na *PPRA* ambaye ndiye msimamizi mkuu wa manunuzi nchi hii, sasa Naibu Waziri huyu anaongea nini? Lilikataliwa na *PPRA*, lilikataliwa na Bodi ya Manunuzi. Na hawa hawakukataa tu, walikataa kwa sababu sheria za nchi haziruhusu, kwa sababu Sheria ya Manunuzi Na. 7 ya Mwaka 2011 iliyokuwa kazini wakati huo hairuhusu mambo hayo; wakakataa. Walikataa kwa sababu huwezi ukapata *value for money* kwa njia hiyo iliyotumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Fedha aliandika barua kupitia Katibu wake Mkuu, kutaka huo mkataba usainiwe ambao pia nao ni muendelezo wa kuvunja sheria za nchi. Lingine inasema kwamba, tulilazimika kutumia njia ya *single source* ili tupate mkopo wa *Standard Charted.* Mkopo wowote katika nchi hii unachukuliwa kwa mujibu wa sheria, hauwezi kuchukua mkopo kwa uvunja sheria za nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hoja hiyo ya kusema kwamba eti tulichukuwa kwa sababu ya mkopo huo tuliuchukuwa kwa sababu tunataka kukidhi matakwa ya sheria. Hapana, hairuhusiwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namba tano, manunuzi haya hayakuwa ya dharura na wala Yapi Merkez si kampuni pekee yenye uwezo wa kujenga reli hapa nchini …

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mpina kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Mheshimiwa Waziri wa Fedha naomba taarifa iwe fupi.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA FEDHA,** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitoe Taarifa ili Bunge lako lichukue kumbukumbu sawa. Hakuna mkopo wowote hapa nchini ambao umewahi kuchukuliwa kwa kuvunja sheria. Mikopo yote inayochukuliwa imepitishwa kwenye bajeti na Bunge hili na inafuata taratibu zote za ukopaji na inakuwa *vetted,* na hivyo ndivyo ilivyofanyika.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mpina taarifa hiyo unaipokea?.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, akae na taarifa yake. Sasa ninaomba niende kutoa mapendekezo ya nini kifanyike katika hili. Moja, katika kutumia hii njia ya *single source,* nimeshajiridhisha kwamba ni wizi, rushwa na ufisadi tu, kwa sababu hakuna kitu kingine. Kwa sababu ukiziacha sheria ukafuata utaratibu wako, hakuna kingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninapendekeza mapendekezo kwenye Kamati ya *PAC* kwamba, la kwanza; kufanya tathmini na kuvunja mkataba wa *TRC* kati ya Yapi Merkezi Lot 1 na Lot 3 na kuitangaza hiyo *tender* upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, Waziri wa Fedha Dkt. Mwigulu Nchemba, Waziri wa Uchukuzi Profesa Makame Mbwalawa, Mkurugenzi wa *TRC* Ndugu Masanja Kungu Kadogosa, Mkurugenzi wa Yapi Merkezi na wengine wote waliohusika, wakamatwe, washitakiwe, kwa makosa ya uhujumu uchumi. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Luhanga muda wako umekwisha, zungumza sentensi ya mwisho…

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa wabunge ninaomba tusikilizane. Bunge letu linaendeshwa kwa kanuni. Sasa Mheshimiwa amepewa muda wake umekwisha kwa hiyo, ninaomba tuwe watulivu tufuate utaratibu.

Ahsante sana Mheshimiwa Luhaga Mpina kwa mchango wako, tunakushukuru. Mheshimiwa Joseph Musukuma atafuatiwa na Mheshimiwa Michael Mkundi na Mheshimiwa Kilumbe ajiandae kama muda utaruhusu.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia. Kwanza, nizipongeze sana Kamati hizi zote tatu; na kwa kweli hizi Kamati tatu ni Kamati ambazo zimepewa watu wanaojielewa, niwapongeze sana. hizi ni Kamati ambazo sisi kama Bunge tunatakiwa kuwapa maua yenu. Kwanza unaenda kuwahoji watu wengine wana nyota wanakuja na nyota na walinzi, lakini mmefanya kazi yenu vizuri, mmeleta Taarifa ili na sisi tuweze kuchakata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, mimi huu ni mwaka wa saba najadili taarifa ya *CAG* yangu ya saba hii. Kwa kweli tufike mahala tuoneane huruma. Niliwahi kusema humu ndani, kama Bunge tunaletewa hizi taarifa kwa ajili ya kuzungumza na kwenda nyumbani ni bora mkabadilisha utaratibu mkamaliza huko nje kwa nje. Kwa sababu, mimi ninajiuliza tunazungumza kila siku kitu kile kile. Ninataka nizungumze kitu kinaitwa *KADCO*; huyu ni nani kwanza; mimi ninataka kujua nyuma yake kuna nani? Kwa sababu mimi kabla sijawa Mbunge akina Zitto Kabwe wanakaa pale wanazugumzia *KADCO,* mpaka leo *KADCO* yule yule tunahangaika kwenye kila taarifa ya *CAG*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni nani yupo nyuma yake au na yenyewe ni Chalinze ile? Au nayo ni ile Chalinze ambayo ilikuwa haina mwenyewe nyuma yake? Kwa sababu, ninajiuliza kila mwaka tunazungungumza kitu kimoja kile kile. Ninakumbuka rafiki yangu Mbalawa mwaka jana, Mheshimiwa Songe Mbunge wa Itilima, ukasimama hapa kwenye kuhitimisha ukasema unairudisha *TAA; s*asa bado tena *KADCO* amekuja humu ndani. Na bado mwaka jana tumeona tena mwezi fulani amesaini tena mkataba na waarabu kuchukua *Airport* ya Arusha. Sasa mnatuchonganisha tu na watu, maana watu ni hawa hawa tunakutana mitaani. Kwa kweli kama Bunge hatuwezi kuwa na meno ya kutoa maamuzi na Serikali ikafanyia kazi hatuna sababu ya kuleta humu ndani. Mnakuja kututafutia uadui tu. Unamzungumzia *IGP* na *General* halafu unakutana naye huko. Sisi ni binadamu ukikosea kadogo si utamaliziwa hasira?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuchukue maamuzi kama tunamzia mtu tunafikia maamuzi. Mnaambiwa mtu ni mwizi, mnahakikisha ni mwizi, chukueni hatua lakini mkileta humu kwa kweli tuinafika mahala sasa tunakuwa tunanyamaza mkose wachangiaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kuzungumza kuhusu *IPTL*. Hii *IPTL* tangu Mheshimiwa Olesendeka; alikuwa *role model* wangu; namuangalia anahangaika, akina Kafulila pia, lakini mpaka leo tena. Watu wakasema fedha ya mboga zikalipwa fedha; leo tena na sisi kizazi chetu ameibuka humu tena anataka kulipwa. Ni *deal* gani hizi jamani? hata najiuliza hivi hizi fedha mnazipeleka wapi? Kwa sababu ni fedha nyingi mno zinatajwa kuibiwa, mbona kwenye benki mzungukoni hazimo? Niamini kwamba sasa mnazihamisha kweli kwenda nje au? Yaani ni matriloni ya fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na Waheshimiwa Wabunge, mimi ninajiuliza; ukienda sehemu nyingi, ninaangalia hata ukiingia kwenye maduka bei za suti zimepanda kweli; na ukigusa shilingi milioni moja na laki mbili. Anakuja mwingine ananunua hata tano na kamoka kazuri na Kiingereza kingi, kumbe ni wezi. Ukimkuta mtu ofisini ameulamba vizuri amechomekea kumbe mtu ni mwizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, niwaombe, kama tuna uwezo wa kutoa maamuzi kuisaidia Serikali, kiukweli taifa hili linaibiwa fedha nyingi sana. Ukijumlisha hizi fedha tu zilizotajwa na *CAG* si fedha ndogo kwenye miradi ya maendeleo kama ingepelekwa. Ninadhani tuna maamuzi kabisa kama Bunge, sheria inaturuhusu kuchukua maamuzi kuielekeza Serikali; na msipotusikiliza basi tuchukue maamuzi kwenu wenzetu ambao tumewatuma mmechaguliwa kwenda kutuwakilisha huko kwenye Serikali. Kwa kweli fedha zinaibiwa mno, yaani unafika mahala, mimi elimu yangu ni ndogo najiuliza hivi *definition* ya shule ni wizi au ni kitu gani? maana mnatusumbua, wasomi ni wezi. Ukikutana naye *supermarket* amejaza machupa ya pombe ya gharama anakwambia *how much, harry up, give me bill;* kumbe ni fedha zetu hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani mimi ninajiuliza jamani. Itafika mahala tutakata tamaa hata kusomesha watoto kama *definion* ya elimu ni wizi ni bora tukafundishe watoto wetu wajitegemee kwa kulima. Namna hii hatuwezi kufika, lazima tufike mahala tuhurumie taifa. Hebu mwangalieni Mheshimiwa Rais anavyohangaika, kila siku tunaona mama wa watu anahangaika na fedha zinakuja. Na ninyi Mawaziri, unajua ukiuliza Mbunge humu ndani hakuna Mbunge hawaripotii *(kutoa taarifa)* wizi kwenye halmashauri zetu, mmemsikiliza Mheshimiwa Simbachawene; tunawaambia kila siku, mnaandika kwenye vi-*diary* kama unanisikiliza vile, lakini ukitoka unakachana ka-karatasi unakaacha hapo hapo. Sasa matokeo yake unakuja kutumbia sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawaeleza kila siku wizi wote unaofanyika kwenye halmashauri; mara mchakato unaanza TAKUKURU, *team*, uchunguzi, mwaka unaisha ripoti ya *CAG* inakuja inasema tumepigwa shilingi bilioni sita. Nimezungumza, nilikuwa huku na mkurugenzi wangu, mpaka nimelia tangu Waziri akiwa Mheshimiwa Bashugwa. Nimemsema hadharani na *document,* chukua mwizi huyo, akatolewa kwangu akapelekwa Misenyi, katoka Ilemela kapiga 11 kwenye laki, katolewa Ilemela kaletwa kwangu kapiga shilingi bilioni tatu, katoka kwangu yupo Misenyi mwakani tunaye *LAAC* tena; sasa hayo ni mambo gani? Si ni afahdali tunyamaze tuwaachie?

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani mimi ninataka mniambie nyie wasomi, *definition* ya shule, mnafudishwa kutusaidia ambao hatukupata elimu au kutuibia? Maana ninajiuliza kitu kidogo; kwa wafanyabiashara ukikosea tu kosa dogo *TRA* wanakuja wanakwambia funga *account*, chukua fedha. Ninyi mnaotuibia matrilioni kwa nini mpo nje? Mimi sitaki kwenda hata mbali kusema kunyonga kwa sababu kunyonga hatutajua kwa Mungu anapata adhabu gani, anaweza kusamehewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tufungue gereza. Tuna mashamba makubwa ya *NARCO*, fungua gereza, peleka gereza la kilimo walime mpaka warudishe zile fedha. Tunahitaji kupata nguvu kazi. Sasa, mwizi akijiuliza nikiiba nikikamatwa, kulima nadhani watu watanyooka; lakini kwa dizaini hii mzee, tunapigana taarifa. Huyu akizungumza, taarifa, taarifa. Tuogope kusema watu, hapana. Kwa kweli tumepigwa vya kutosha sisi kama Bunge; na Watanzania mkiangalia tokea jana wanavyolisema Bunge letu, ni Bunge la kiwango, lazima tutoke na jitu humu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru sana Mawaziri lakini watanisamehe. Unaweza ukapima, katika kipindi ambacho Waheshimiwa Wabunge wanataka kulieleza taifa ni kipindi hiki ambacho tunazungumza Taarifa ya *CAG;* lakini Mawaziri hawapo, wapo moja, mbili, tatu, wengine wapo huko kantini; hakuna u-*serious.* Kaeni hapa msikilize ili mjue tunachokisema humu. Na nimuombe hata Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Rais, futa safari zote mpaka watu wajadili hii taarifa ikamilike. Kwa sababu, matatizo haya tunawaeleza kila siku *(diary)* halafu ukitoka kantini mtu amesahau.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA**: Mnaanza!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Karibu.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, inaonekana Mawaziri hatupo. Ninaomba Mawaziri tusimame ili tuonekane.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Musukuma endelea na mchango wako.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamheshimu Mheshimiwa Simbachawene, tuangalie Mawaziri na Naibu Mawaziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajiuliza kwa hesabu ya kawaida, taarifa inasema tuna wafugwa 3,100, wamemaliza muda wao wanakula. Ukisoma humu ni wafungwa wa nchi za nje. Sasa, shilingi bilioni tano kwa mwaka, ukipiga tu hesabu, kwa nini tusitoe hata *Dream Liner* tukawarudisha kwao Ethiopia? Kwa nini tunaendelea kuwalisha? Na kwa nini wale bure? Kwa nini tusifungue magereza ya kilimo tukaweweka huko tukapata nguvu kazi. Kwa nini unakaa na watu, huna kazi nao, hukumu yao imeshakwisha? Hamuogopi hata dhambi kwa Mungu kwa Mnawaweka watu magereza? Chukueni ndege. Kama tunatoa ndege kupeleka timu ya timu ya mpira, kwa nini tusitoe ndege kupeleka wakimbizi kwenye nchi zao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni kuhusu *TANOIL*. Mimi nilikuwa Mjumbe wa Kamati ya Nishati, Mwenyekiti wangu Kitandula. Nilikataa hiki kitu kutoa fedha kuwapa *TANOIL*, nikawaambia zinaenda hizi fedha; znaenda kabisa hizi fedha. Leo tunazungumza *short* ya shilingi bilioni saba. Haki ya Mungu tuwe hai mwakani, shilingi bilioni 80 imeshaenda pale. Serikali msikubali kuanza kufanya biashara, mmefeli. Tumewapa mradi wa mabasi ya mwendokasi, barabara ya kwenu, magari ya bure leo yanatembea manne kutoka gari 300 na bado mnajenga mwendokasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwenye *projector* pale wanakwambia barabara ya Mbagala itakuwa hivi; unawekewa

wazungu wanakimbizana kupanda gari kumbe wezi watupu. Wewe mabasi unaweka kodi, mchakato, gari imedondosha *bolt* unaambiwa wa kusaini yupo Dodoma. Mabasi yote yameisha, bado mnaenda kufanya kazi. Serikali kwenye suala la biashara acheni, tuachieni sisi watoto wa kitaa.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Musukuma kwa mchango wako. Waheshimiwa ninamwita Mheshimiwa Michael Mkundi.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi hii, nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema kwa kutujalia uhai. Nipongeze Kamati zote zilizowasilisha taarifa kwa niaba yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa na mchango kwenye maeneo matatu. Kwenye Taarifa ya Kamati ya *LAAC* ukurasa wa 10 wanatoa mapendekezo baada ya kufanya tathmini na kuona kwamba kuna shida kwanye makusanyo kwenye halmashauri zetu. Kwa maana hiyo, Kamati ya *LAAC* inapendekeza ubunifu wa vyanzo vipya vya mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo jema, na kwa uzoefu wa miaka kadhaa tukipokea taarifa za *CAG* kumeonekana udhaifu kwenye makusanyo ya Halmashauri zetu, lakini vilevile kuna umuhimu wa kuanzisha vyanzo vipya vya mapato. Lakini mimi nilikuwa na mtazamo tofauti. Tuna vyanzo vingi vya mapato na katika vyanzo tulivyonavyo, baadhi vinakuwa ni kero kwa wananchi. Hii ni kwa sababu, moja, kunakuwa hakuna ufanisi kwenye vyanzo tulivyonavyo katika makusanyo yake. Matokeo yake ni kwamba kila mwaka taarifa inayoletwa inaonekana kwamba hatufikii malengo; lakini si kwamba vyanzo havipo. Vyanzo vipo lakini tuna udhaifu kwenye makusanyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo kinachopaswa si kuendelea kubuni vyanzo vipya kila kukicha bali mimi ninachokifikiri, katika vyanzo tulivyonavyo tuweke mifumo thabiti ya kuhakikisha kwamba ukusanyaji wa mapato kwenye vyanzo tulivyonavyo unakuwa ni wenye ufanisi; lilevile tunaziba mianya ya upotevu wa fedha kwenye vyanzo tulivyonavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mianya mingi sana inayopelekea upotevu wa mapato kwenye halmashauri zetu kupitia vyanzo vya mapato tulivyonavyo. Kwa hiyo, badala ya kuendelea kubuni vyanzo vipya vya mapato ambavyo vingi vinaweza vikawa ni kero kwenye jamii, zaidi tuwekeze kwenye kuongeza ufanisi kwenye makusanyo kwenye vyanzo tulivyonavyo na kuziba mianya ya upotevu wa fedha kwenye vyanzo hivi na hatimaye tutafikia malengo kuliko kuendelea kubuni kila kukicha vyanzo vipya ambavyo vingine vinakuwa ni shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwenye ripoti ya *CAG* kama ambavyo imewasilishwa na Kamati, kupitia mashine za ukusanyaji *(POS)*. Kulikuwa na upotevu wa takriban shilingi bilioni 11.07. Fedha hizi ni kwa sababu tu, ya kutokudhibiti mianya hii ya upotevu wa mapato. Kwa hiyo, niendelee kusisitiza, kwa kutumia Kamati zetu; lakini kwa kuwa Serikali mpo, tujenge mfumo ambao utaondoa udhaifu huu ili vyanzo hivi tulivyonavyo viwe ni vyenye tija lakini vilevile ufanisi katika ukusanyaji wa mapato kwenye vyanzo hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ambalo nilitaka kuchangia ni kuhusu ubadhilifu kupitia manunuzi kwenye halmashauri zetu. Nimpongeze Mheshimiwa Rais anafanya kazi kubwa sana. Hakuna kipindi ambacho tumepokea fedha nyingi kwenye majimbo yetu kama kipindi hiki. Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa sana kuhakikisha kwamba fedha zinapatikana, miradi ya maendeleo inapatikana kwenye majimbo yetu. Jukumu tunalokuwa nalo na ambalo tumeonesha udhaifu mkubwa ni kwenye kuthibiti fedha kwenye maeneo yetu kama ambavyo wachangiaji wengi wamesema, juu ya ubadhilifu unaofanywa na watendaji kwenye halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa natafakari baada ya kupitia taarifa hii, kwamba kwa mfano tumepoteza kwa *sample* ya halmashauri kadhaa zilizohojiwa na Kamati; kwamba bilioni 3.29 zimelipwa kwenye halmashauri zetu kwa ajili ya manunuzi ya vifaa ambavyo havijaweza kupokelewa; unaweza kuona. Kwa mujibu wa sheria, ukiangalia Sheria ya Manunuzi, Kanuni namba 242 na 248 inaonesha wazi taratibu gani zinapaswa zifuatwe wakati wa manunuzi. Kama inatokea fedha zinalipwa, bidhaa

hazijaletwa matokeo yake halmashauri itapokea bidhaa ambazo zina mapungufu au zisizokidhi viwango.

Mheshimiwa Mwneyekiti, na kama imechukuliwa kwa *sampeling* pekee, je, kwa halmashauri zote tumepoteza fedha kiasi gani? Kwa hiyo, tuna jukumu kama Bunge kuishinikiza Serikali iweze kusimamia eneo hili. Kwa sababu kanuni zipo, kusingekuwa na kanuni tungekuwa hakuna mahala ambapo tunaweza tukasema kwamba inawezekana kuna udhaifu, lakini udhaifu uliokuwepo sasa ni kwenye usimamiziwa kanuni hizi. Kwa hiyo niombe Serikali iliangalie jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la mwisho ambalo nilifikiri nilichangie ni juu ya miradi inayotekelezwa kwa *force accont*. Kwenye Taarifa ya Kamati imeonesha udhaifu kwenye miradi inayotekelezwa kwa mfumo wa *force account*. Kifungu namba 64 cha Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2011 na Kanuni zake, inaoneshani miradi gani na kwa mfumo upi miradi miradi inaweza kutekelezwa kwa *force accout.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mmoja kati ya watu wanaoamini katika mfumo wa *Force account* katika utekelezaji wa miradi yetu. Tatizo tunalokuwa nalo ni kwenye usimamizi. Hii ningependekeza, ukiangalia uzoefu wa miradi yetu tunayoitekeleza kwa mfumo wa *force account,* shida kubwa sana inatokea kwenye usimamizi na kufuata taratibu zinazoweza kusimamia utekelezaji bora wa miradi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeshauri, kama ambavyo baadhi ya nchi nyingine zimefanya. Nilikuwa ninapitia kijarida hapa cha nchi ya Zambia ambacho ninafikiri na sisi kama taifa tungeona umuhimu kwamba, tuwe na sera ya *monitoring and evaluation* ya kitaifa ambayo inaweza kufanya kazi kwa kusimamia miradi yetu ya maendeleo kwenye ngazi zote. Kwenye eneo la kitaifa, mikoa, wilaya, Wizara na kadhalika. Tukiwa na *national policy* ya *monitoring and evaluation* ninaamini miradi yetu mingi kwa kutumia mfumo huo wa *force account* inaweza kuwa na tija na fedha tunazozitumia kwa ajili ya kutekeleza miradi hii ikawa na tija kwa taifa letu na wananchi waka-*benefit*

kutokana na fedha hizi ambazo zinapelekwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi kwenye maendeleo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa nafasi. Ahsanteni sana. Ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi kwa mchango wako mzuri sana. Waheshimiwa Wabunge tumefikia mwisho kwa mchana huu, tutaendelea na michango jioni ambapo tutaanza na Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda, Mheshimiwa Priscus Tarimo, Mheshimiwa Hamis Tabasam, Mheshimiwa Vedastus Manyinyi, Mheshimiwa Noah Saputu na wengine tutaendelea kuwataja jinsi wanavyoendelea.

Baada ya kusema haya sasa ninasitisha shughuli za Bunge hadi Saa 11.00 Jioni ya leo.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA KAMATI

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali kuhusu Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu zilizokaguliwa za Serikali Kuu, Mashirika ya Umma na Kaguzi za Ufanisi kwa Mwaka wa Fedha ulioishia Tarehe 30 Juni, 2022**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kuhusu Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha ulioishia Tarehe 30 Juni, 2022**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kuhusu Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na mjadala ulio mbele yetu. Tunaanza na Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, atafuatiwa na Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda na Mheshimiwa Hamis Tabasam ajiandae.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa nafasi hii ya kuanza kuchangia mjadala huu kwa mchana wa leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na wenzangu wote walioanza kuchangia ambao walionesha hisia kubwa sana na masikitiko na wakawa wakali kuhusiana na taarifa hizi ambazo zimeletwa na Kamati zetu tatu na ambazo wenzao wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ambalo ningependa kushauri na wenzangu, baadaye nadhani wataalam watuongoze namna ya kulifanya, ni vizuri Taarifa hizi za CAG zijadiliwe kwa wakati (leo tunajadili mambo ya 2021/2022) ambayo yaliwasilishwa kwa Rais muda mrefu. Mengine yameshakuwa ni viporo na kama walivyosema wengine na watu wako makazini. Kwa hiyo tunakuja kukutana na hali halisi kwamba, uhalisia wa namna ya kupambana na hayo mambo tunakuwa tumechelewa sana. Ni vizuri tuelekezwe namna ya kutengeneza sheria, ili Taarifa ile inapowasilishwa kwa Rais na kipindi hicho hicho na sisi tuanze kuijadili ili tuweze kutoa mapendekezo ambayo yanaweza yakawa *effective* na yakawa yamekwenda na wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mambo mengine ambayo ni nje na hayo mahesabu, lakini ndiyo yanayotupeleka tunakuwa na matatizo mengine mengi tu. Kwa mfano, wakati tunapokuwa kwenye Bunge la Bajeti hapa ule Mwezi Mei unapoishia Mwezi Juni mwanzoni, Mfumo wa Mahesabu ya Halmashauri na nadhani ni wa Serikali nzima, unakuwa haufanyi kazi. Unakuwa haufanyi

kazi mpaka Mwezi Septemba, mwingine mpaka Mwezi Oktoba, lakini Serikali inatumia. Watu wanakusanya hela, watu wanatumia hela na wanatumia kupitia mfumo gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tuna nchi ambayo tunashindwa leo kutengeneza mfumo wa kisasa wa kielektroniki ambao unaweza uka-*switch* tu matumizi angalau hata wiki moja baada ya bajeti, tunazuia matumizi kuanzia Mwezi Juni, tunakuja mpaka Mwezi Septemba, hapo katikati hayo yanayofanyika maana yake tunakuja kutengeneza *duplicate* tu. Kwa hiyo vipo vitu vingine ambavyo vinasababisha haya matatizo na hivi vishawishi viwepo likiwepo hilo la mfumo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapata pia mashaka sana, ukisoma majukumu ya *CAG* ni Mkaguzi na Mdhibiti. Kudhibiti ni kuzuia pale ambapo panaweza kuleta matatizo baadaye, lakini hebu nitoe mfano mmoja. Tuna Kiwanda cha Karanga *Leather,* kimeanzishwa, nimeshaleta malalamiko, nimeshaleta mawazo, kuna wawekezaji wameshakuja, lakini Kiwanda kile bado hakifanyi kazi *effectively* kama vilivyo viwanda vingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka leo ni kiwanda ambacho nimeona huku kwenye mapendekezo ya Kamati ni kuiondoa Serikali kwenye biashara. Kile kiwanda kinatakiwa kizalishe, kiajiri watu karibu 3,000, mpaka leo kimeajiri watu 250. Mabasi yanaenda pale ya Kamati, ikitoka *PAC* inaenda Katiba na Sheria, inaenda sijui Kamati gani, Mawaziri wanapishana pale. Hicho kitu kinakaa, kiwanda kikubwa kama kile ambacho kimewekeza zaidi ya bilioni 150, kinasubiri kuleta *pair* mbili za viatu hapa Bungeni kuja kuuza na hizo hela ni za walipakodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa yeye ni Mdhibiti, kabla hajataleta matatizo, hiyo Ofisi ya *CAG* inafanya nini kuhakikisha ile hasara inayoendelea kupatikana pale, haiji tena tuje kuiisoma kwenye makaratasi? Tumeleta hoja, tumeleta mawazo mbalimbali, hakuna kinachofanyika. Lile jukumu la kudhibiti lipo wapi hapo? Kwa hiyo, tunasubiri ikishakuwa ni hasara kubwa tulete hapa tuseme hii ni hasara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda pale wanakwambia kile kiwanda hakiwezi kushindana kwenye soko, kwa sababu wale washindani wengine wanawazidi maarifa, lakini wao wanaiandikia Serikali kuleta hela ya matumizi pale. Huwezi kufanya biashara kama unategemea gharama zako zilipwe kutoka sehemu nyingine. Serikali itashindwa kufanya biashara. Tutafute mwekezaji, tuuuze hisa pale tubaki na hisa kidogo, wawekezaji wafanye kazi na watumie hela zinazotoka pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa Diwani vipindi viwili kabla ya kuwa Mbunge, nime-*deal* sana na halmashauri. Nielezee kidogo juu ya *force account*. Nilishawahi kutoa tena haya mawazo. *Force Account* inafanya kazi vizuri sana kama halmashauri zina wale wataalam, kuwe kuna *Engineer*, kuwe kuna *Architecture,* kuwe kuna *Quantity Surveyor* wameajiriwa ili wao wasimamie, lakini kama hao wataalam hatuna, *Force Account* ni jipu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu, ni kweli, kwenye hii miradi midogo darasa moja, sijui madarasa mawili shule moja ya msingi tunaweza, lakini miradi mikubwa hatutaweza kwa sababu ni *technical know-how* ya hawa wataalam inayohitajika, *Engineer proper* na siyo *Engineer* aliyetoka shule. *Engineer* ambaye ana-*experience,* tuna *Quantity Surveyor,* tuna *Architecture,* hii *Force Account* itafanya kazi vizuri sana, vinginevyo tunadanganyana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiiongelea *Force Account* huwezi kuacha kuongelea Sheria ya Manunuzi. Matatizo mengi yanayotoka kwenye Ripoti hii ya *CAG,* ukiya-*trace* ni kwenye Sheria ya Manunuzi. Kwenye Sheria ya Manunuzi itabadilishwa, inabadilishwa. Kwa nini, tunashindwa kuwa na *database?* kwamba kitu hiki, *quality* hii bei yake ni hii elekezi. Kwenye maeneo haya kama ni Kigoma bei ni hii, Kilimanjaro bei ni hii. Tuhakikishe kwamba tuna, haiwezekani kabisa kwamba kitu kimoja mtu binafsi unatengeneza kwa milioni 15, Serikali inatengeneza kwa milioni 40.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakaa hapa tunapiga makofi, tunakwenda tunakagua, ma-*VX* yanaenda pale ma-*V8* manini. Jamani Sheria ya Manunuzi ni jipu lingine, huwezi kuiongelea *Force Account* bila kuongelea Sheria ya Manunuzi, lazima iboreshwe zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kuongelea namna ambavyo Serikali yetu inafanya kazi na nitatolea mfano tena Mradi mwingine pale Moshi. Tulikuwa na *stand* ya Nganga Mfumuni katika miradi iliyoletwa na Serikali Kuu inaitwa Miradi ya Kimkakati. Ikaingizwa pale fedha shilingi bilioni 7.0 ya Serikali Kuu. Manispaa wameshaingiza hela yao zaidi ya milioni 700, Waziri Mkuu ameshatembelea pale akatoa maagizo kazi ikamilishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ninavyoongea na wewe ni mwaka wa nne Mkandarasi *CRJE* amekataa kurudi *site*. Sasa Mkaguzi na Mdhibiti hii *role* yake ya kudhibiti iko wapi? Kwa nini hajaingilia, atoe maelekezo ni namna gani sasa Mkandarasi arudi *site*. Ni namna gani kazi iendelee. Sasa anasubiri likishakuwa ni jibu sasa aje atuletee hapa kwamba kule Moshi kuna *stand* imetengenezwa bilioni 7.0 zimeingia haijakamilika, halafu sisi tufanye nini? Hela za wananchi zimeshakaa chini shilingi bilioni 7.0, zaidi ya miaka mitano hatusaidii. Kama siyo yey,e basi mamlaka gani nyingine ya kuhakikisha vitu kama hivi vinasimamiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee Bima ya Afya ambayo juzi tumepitisha Muswada ule wa Bima ya Afya kwa Wote. Katika taarifa hizi, moja ya matatizo ambayo Kamati zimeyaona kwenye bima ya afya. Moja, ni kuibiwa. Pili, ni mfumo mbovu. Tatu, wametaja fedha ambazo Serikali imechukua na haijarudisha. Hela za kutengeneza Benjamin Mkapa zaidi ya milioni 129. Hela iliyoenda *NIDA* sijui milioni ngapi? Hela iliyoenda sijui ni *MOI,* sijui ni wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunapokwenda kuboresha hii bima, ni namna gani tutasababisha au tuaweka sheria, Serikali isiwe inaenda tena kuchukua fedha huko. Ichukue iende ikafanye shughuli nyingine, vinginevyo tunaenda kuchukua hela kwa wananchi tunazikusanya tunasema ni bima ya afya, halafu sasa

unakuwa ni Mfuko wa ziada wa Serikali wa kwenda kufanya mambo mengine tena na hilo litakuwa ni jipu lingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni namna gani tumejibu haya matatizo ambayo yameonekana kwenye Kamati zetu hizi zimeeleza kwamba ni hayo matatizo ya bima yetu, ni namna gani, turekebishe pamoja na vifurushi? Sasa kama hatutachukua hatua mapema za kudhibiti, maana yake tutakwenda kupata matatizo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende eneo la miradi…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tarimo, muda wako umekwisha malizia.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia. Ni sheria kwamba miradi yote inayofanyika kwenye maeneo yetu, *BOQ* wapewe mpaka Wenyeviti wa Serikali za Mitaa. Leo Madiwani wenyewe hawapewi *BOQ,* iwe ni ya Barabara, iwe ni ya darasa, kwa nini hatuwezi kusimamia hilo ili na wale wawe watu wa kutusaidia kusimamia miradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, naomba tulisimamie ili Serikali iweze kufanya kazi inavyotakiwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Kilumbe Shabani Nge'enda, atafuatiwa na Mheshimiwa Hamis Tabasam na Mheshimiwa Constantine Kanyasu ajiandae.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa mchango wangu katika jambo hili kubwa la wasilisho za Kamati zetu tatu, juu ya Ripoti ya Mkaguzi na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali *(CAG)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kutujaalia uzima na afya ili tuendelee kufanya kazi ya Watanzania. Zaidi ya yote, niipongeze

Serikali, nimpongeze Mheshimiwa Rais wetu kwa kuendelea kusimamia Utawala Bora katika nchi yetu, maana hata haya anayoyafanya *CAG* ni sehemu ya kazi ya Utawala Bora. Vile vile nizipongeze sana Kamati zetu tatu za Bunge pamoja na *CAG* mwenyewe kwa kazi nzuri waliyoifanya na kutupa nafasi ya sisi sasa kuingiza mawazo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika michango ya wenzangu waliotangulia na mimi nikiwemo humu nasikiliza, lazima tuone kabisa kwamba sisi kama wawakilishi wa wananchi tumechoka. Hapa tulipofika tumefika kwenye hatua ya mwisho ya koma ya kuvumilia ubadhirifu na wizi unaoendelea kwa watumishi wa umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tumechoka zipo hatua za kuchukua kwa watu waliochoka. Sisi kama Bunge tuna hatua za kuchukua kama watu tuliochoka. Watu wengi hapa wanazungumza juu ya suala, kila wakizungumza wanasema hawa hawana uzalendo. Uzalendo hauendi kununuliwa dukani kama sukari kwamba, naenda kuwanunua kilo moja niwaungie watu chai wanywe, wapate uzalendo, hapana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu anayekosa uzalendo ni lazima utengenezwe utaratibu wa kumrudisha kuwa mzalendo. Utaratibu huo hauwezi kuwa wa lelemama, utaratibu huo lazima uwe wa nguvu. Ndiyo utaratibu wa utawala maeneo yote, hata Mungu mwenyewe ambaye ni Mtawala Mkuu, alipowataka waja wake kila maeneo wafuate msimamo fulani wakashindwa, basi alichukua hatua. Wale wanaosoma katika Vitabu Vitakatifu wanajua, Mungu alichukua hatua gani kwa watu wa Lutwi? Mungu alichukua hatua gani kwa watu wa Nuhu? Akafika mahala akagharikisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa lazima tutengeneze gharika ili kurudisha imani ya Watanzania kwa Serikali yetu. Katika hili niseme, leo nasema lakini Bunge lijalo nitasimama hapa na hoja ya kulitaka Bunge kwa kuangalia kanuni kama zinaruhusu, kwa utaratibu nitakaouomba, Bunge lipokee taarifa kutoka kwenye Serikali, watu wangapi wamechukuliwa hatua kutokana na Taarifa ya *CAG*? Kama hakuna, hakuna kuendelea na Bunge.

Kama hakuna hatua tusiendelee na Bunge, tusubiri mpaka Serikali ichukue hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wizi tunaouzungumza hapa ni ule ambao *CAG* kapata bahati ya kuufahamu, lakini upo wizi ambao CAG hakupata bahati ya kuufahamu. Kakuta nyaraka zote ziko sawa, lakini hakuna kilichonunuliwa na yeye hakujua. Wizi ni mwingi, mwingi, lazima tuchukue maamuzi magumu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu hivi karibuni alifanya ziara mkoani kwangu Kigoma. Kwa muda mfupi tu aliofanya, kapokea taarifa pale akafika mahala akasema Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma, Ujiji ambayo mimi ndiyo Mbunge kwenye Jimbo hilo, kuna hela zinatoka Hazina zinapigwa huko zinakuja hazina maelezo yoyote. Zikishaletwa kule watu wanazitoa, halafu wanagawana na wanagawana na waliozileta kutoka huko Hazina. Kwa hiyo kuna mtandao huku Hazina, kutoka TAMISEMI…

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kilumbe kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Shabiby.

**TAARIFA**

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nataka nimpe taarifa Mheshimiwa mzungumzaji kwamba, anayoyazungumza mengi sana ya ufisadi yanahusiana na halmashauri. Kila nikiangaza macho hapa simuoni Waziri wa TAMISEMI. Kwa hiyo nani sasa anayesikiliza, yupo Naibu, lakini na Waziri na yeye anatakiwa awepo humu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kilumbe taarifa unaipokea?

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeipokea, lakini inahusu Serikali, kwa sababu Waziri Mkuu yupo basi na huyu ndiyo Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni, yeye akisikia inatosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokusudia kusema ni kwamba, Mheshimiwa Waziri Mkuu akafika mahali akabaini, akaunda Tume. Tume imefanya kazi imefika mahala imegundua kwamba, kweli upo mtandao wa watu ambao wanachukua pesa huku wanazileta, hazina maelezo yoyote, siyo za shule, siyo za chochote zinapigwa kutoka huku. Kwa hiyo, upo mtandao ambao unatakiwa kushughulikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu, namshukuru sana kwa sababu amenisaidia katika kutengeneza ile Halmashauri yangu, ila namwomba wale watu aliowataja na kusema wapelekwe mahakamani mpaka sasa hawajapelekwa na wako kwenye ofisi zetu. Namwomba sana achukue hatua za haraka, watoke kwenye ofisi zetu, waende mahakamani, kazi ifanyike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Waziri wa Fedha ampe Waziri Mkuu ushirikiano wa kutosha, ili hawa wanamtandao ambao wako kwenye Ofisi yake na TAMISEMI, wote wachukuliwe hatua. Hakutakuwa na maana ya kuwapiga dagaa wadogo, ukaacha mapapa wakubwa wapo juu huko, hakutakuwa na maana yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wenzangu wamekuwa wakizungumza na mimi kwa nyakati tofauti hasa wa Kamati ya Serikali za Mitaa, juu ya hali mbaya ya makusanyo kwenye Halmashauri za Mkoa wa Kigoma. Hili jambo wamekuwa wakilieleza la kutuhusisha na umahiri wetu, kwamba, nyinyi mnaonekana mahiri sana lakini halmashauri zenu haziwezi. Ukiangalia katika sura moja kama kejeli fulani hivi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwaambie kitu kimoja, ni jambo la ajabu sana umkate mtu ngwala halafu ushangae ameanguka na wewe mwenyewe ndiyo umemkata ngwala. Huu mfumo wa kuzifanya Halmashauri zetu zisiwe na uwezo umetengenezwa, suala la Halmashauri kuwa na uwezo ni mzunguko wa fedha wa wananchi wenyewe, kama hawa wananchi umewanyima treni, umewanyima meli, umewanyima viwanda, halafu kila mfanyakazi anaefika mahala akafanya makosa ndiyo unampeleka Kigoma kwa adhabu! yaani Kigoma

imegeuka ni *Guantanamo* ya watu kwenda kuadhibiwa unategemea nini? Aliyeiba huko mkaona huyu mwizi peleka Kigoma, aliyekosa adabu huko peleka Kigoma, kwamba Kigoma ni eneo la adhabu halafu unategemea wakusanye vizuri inawezekana hiyo kitu? haiwezekani hata kidogo! Nawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwenye Kamati hii…

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kilumbe, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

**TAARIFA**

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ninampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa mchango mzuri ambao anaendelea kuuchangia. Ninaomba tu nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge kwamba utaratibu wa kuwa-*allocate* watumishi katika Halmashauri hauzingatii mwenye makosa apelekwe Kigoma au Halmashauri nyingine yoyote, Mtumishi mwenye makosa akithibitika hatua za kisheria na kinidhamu zinachukuliwa mara moja pale alipo, tunafahamu kuna mapungufu ambayo Serikali inaendelea kuyafanyia kazi.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, inatosha hiyo taarifa, nimeshaelewa maana unakula muda wangu. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kilumbe, taarifa unaipokea?

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hiyo nimeipokea kwa maana anasema utaratibu ndiyo upo hivyo haufuatwi, huo unaousema ndiyo utaratibu, sikusudii kusema kwamba watu wote au Watumishi wote wa Umma walioko Kigoma, labda ni wakosaji Hapana! Lakini kumekuwa na tatizo la wale wakosaji ambao wanakosa maeneo mengine adhabu mpeleke mbali huko Kigoma, mpeleke huko. Sasa hili ndilo jambo

lililochangia kwa kiasi kikubwa sana kufanya Halmashauri zetu mapato yake yawe madogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeeleza sababu za awali, kwanza za kiuchumi lakini nyingine za kiutendaji. Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma, Ujiji inapungukiwa watumishi chungu nzima ambao wangeweza kusaidia ku-*stimulate* utumishi na kufanya mapato yawe mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, idara ya fedha kuna upungufu, idara ya ukaguzi kuna upungufu.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kilumbe, taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Rashid Shangazi.

**TAARIFA**

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa mzungumzaji kwamba kwa kuonesha kabisa kwamba Kigoma imewekwa pembeni hata watumishi wanaofanya kazi katika Halmashauri ya Kigoma karibia wengi ni *single* hawaendi na familia zao.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kilumbe, taarifa unaipokea? Halafu malizia mchango wako muda wako muda wako umekwisha.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii ninaipokea, ni *single* kwa sababu wamekuja kwa adhabu, hakuna mtu anayekwenda jela na mke wake na mtoto, ukienda jela mke na mtoto unaacha huku wewe unaenda kukaa jela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono. *(Kicheko/Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kilumbe ahsante sana. Mheshimiwa Hamis Tabasam, atafuatawa na Mheshimiwa Constantine Kanyasu, Mheshimiwa Vedastus Manyinyi, ajiandae.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia, lakini naomba nitoe angalizo wakati naendelea kuchangia. Angalizo langu sana ni Mawaziri msipite mbele ya treni wakati imeanza kuondoka, kwa sababu kidogo leo sijaja vizuri sana. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni nchi huru, leo tunakwenda mwaka karibu wa 63 huko, sasa nchi imepata uhuru, ina mipango yake na mifumo na sera imejipangia, Chama cha Mapinduzi ni miongoni mwa Vyama imara sana duniani na Chama chenye heshima. Bunge lako hili nilitegemea leo kwamba angekaa hapa Spika, ningempa maua yake, ni kwamba Mheshimiwa Spika ni Spika sasa hivi wa Dunia kwa hatua hiyo kama ni Spika wa dunia basi hili Bunge sasa hivi la Tanzania linaangaliwa dunia nzima. Namna gani tunajiendesha, namna gani tunachukua hatua, hatua hazichukuliwi ndiyo maana watu wanakuja kujirudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina taarifa za *CAG* za 2020/2021 hazijafanyiwa kazi, tumepata 2021/2022 bado majibu hayajaja, Mheshimiwa Waziri Mkuu, tumekwenda nae Sengerema, mara mbili amekwenda Sengerema, safari nyingine amekuja na taarifa ya *CAG* moja kwa moja pale tumeibiwa bilioni 3.6, watu wametajwa kwa majina matokeo yake wale watu wamaondolewa pale na wako kazini wanaendelea ku-*drive* magari wakati bado kuna pesa zetu wamaeiba, sasa hii inakuwa ni hatari sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengi yaliyoletwa na *CAG* hapa ni kwamba hatua hazichukuliwi, sasa tunataka kujua nani anayechelewesha? Tunaomba Bunge lako tuje sasa tutengeneze Sheria kwanza, kama sasa hivi taarifa za *CAG* za 2019/2020 tuje kukaa hapa tujadili mwezi mzima hatua walizochukua Serikali watupe, taarifa za 2020/2021 na tuchukue taarifa nyingine za 2021/2022. Mama yetu Mheshimiwa Rais, anafanya kazi sana kutafuta hizi pesa, kuna familia hii inayoitwa Tanzania ina Mama anahakikisha watoto wake wasije wakalala na njaa, ana kundi kubwa la watoto wengi mle ndani kuna watoto ambao tayari ni waadilifu na *CAG* yuko pale anamletea

taarifa, ndugu zangu nilionao kwenye Serikali, taarifa hii hapa Mama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mama anapokea taarifa hiyo, siku anapokea taarifa hiyo hatukujua Mama alilala au alifanyaje, usiku kucha alikesha sijui kama alisoma taarifa yote ya *CAG* akaimaliza, lakini anao watoto wengine ambao ni Bunge ambao sisi katika hili Bunge humu humu ndani ya Bunge wamo hawa watoto wanaolalamikiwa kwenye taarifa aliyoleta ndugu yetu *CAG,* angalia hayo maneno yalivyo sasa, na wote tunakuja tunataka kula, sisi wengine tunakaa tunawaza tutakula nini kuna wenzetu wanawaza wataondokaje na mahawala zao kuwapeleka Dubai, kwenda *honeymoon* haiwezekani! Haiwezekani hata mara moja! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tuhakikishe familia hii yote ni yetu sisi na tunatakiwa tuhakikishe Mama yetu tunamsaidia, tutakuja tumsaidiaje sasa lazima tuchukue hatua, haiwezekani hata siku moja! Jamani lazima tuchukue hatua, Wabunge angalieni sana tumebakiza muda mdogo sana kurudi kwa raia huko na raia wanatuona hii hali tuliyonayo tunakuja humu ndani tunakuja kupongeza watu haiwezekani hata siku moja. Suala la kupongezana jamani Wabunge, liishe. Watu wanaotuibia sasa ifikie mara ya mwisho sasa naanza kuchangia. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la Halmashauri *POS* zinazimwa. Zimeibwa pesa bilioni 11, mwaka jana taarifa ya *CAG* zilibiwa pesa karibu bilioni 19 kwa hiyo kila mwaka wanakuja wanaiba hizi pesa, Mheshimiwa Waziri Mkuu ana-*suffer,* kila tunakomuona Waziri Mkuu anakuja anasema huyu mtu mwizi lakini madaraka hana ya kumfukuza palepale mnataka utawala bora gani huo? Yaani anayeonekana Waziri anakwenda wa Serikali za mitaa anaambiwa shule ilikuwa inajengwa hapa au bwawa lilikuwa linachimbwa hapa, bwawa halipo, bwawa limetoroka halafu tena huyu mtu kumtoa inaonekana kwamba bwawa halipo Waziri sasa afanyaje? Tumekwenda na Waziri wa Maji anaambiwa kuna *flow-meter* imekwenda kufungwa pale Sengerema Tabaruka ya kiwango Fulani, anakwenda kuangalia ni katoto ka-*flow-meter* Waziri afanyaje sasa, anabakia tu pale

Mheshimiwa Tabasam tuende hawa wako nje ya mamlaka yangu, haya ndiyo maneno sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ifikie mahala Waziri akitamka jambo kule ameliona yuko *site,* Waziri Mkuu anazunguka nchi nzima yuko *site*, akimaliza Waziri Mkuu pale yaani mtu ameshatembea, anatembea na Yesu, hakuna jinsi nyingine ifikie mahala lazima tu-*dictate* mambo mengine. Habari ya utawala bora kwenye wizi Hapana! utawala bora majambazi wanaendelea kuwepo tu, mtu anaiba kuku ameuwawa, majamaa yameiba pesa za kutosha haiwezekani hata siku moja!

Mheshimiwa Mwenyekiti, *POS* zimezimwa Sengerema hapa kwenye taarifa hapa imesomwa naona na Sengerema, *POS* zimezimwa mtu ameshaiba huko Ushetu, Mweka Hazina, kaiba Ushetu analetwa Sengerema anakuja kuzima tena *POS* za Sengerema bado mnamuacha tu!

Halafu ninyi Naibu Mawaziri wa TAMISEMI mko hapo mbele mnaendelea tu kuongea badala ya kusiliza haya maneno, haya maneno gani tena haya, badala ya kuandika kwamba kuna majambazi Sengerema wametajwa hapa! Hapa ilitakiwa kuunda *task force…*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tabasam, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jamani nimesema hivi ninavyozungumza, treni naomba tu mtu atulie anisikilize aje ajibu. Wanao uwezo wa kuja kujibu kesho, waje wajibu kesho watuachie muda anataka kunitoa kwenye reli. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, malizia mchango wako muda umeisha.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, waunde *task force* za kushughulikia miradi ya Serikali na hizo *task force* mimi ushauri wangu ziwekwe pale hizo *task force* za kwenda kusimamia miradi wawemo watu wa Ofisi ya Waziri Mkuu, watu wa TAMISEMI na watu wa Ofisi ya Rais na ikiwezekana watu wa Polisi na TAKUKURU wawemo waiangalie miradi yote nchi nzima. Hizi pesa za UVIKO tunazosema sasa hivi kwamba zimekuja kufanya kazi za kujenga huko Majimboni, Majimbo yanavuja kila kitu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tusitumie Wakandarasi, nchi hii ina Wakandarasi zaidi ya 6,000 wakafanye hizi kazi? Suala la hizi *POS* kwanini Wakuu wa Mikoa wasipewe *password* wakawa wanaangalia? Mtu unampa Mkoa, Rais wa Mkoa unamnyima *password* halafu mtu mmoja tu, wajanja fulani wako hapo TAMISEMI kazi yao kuiba hizi fedha yaani mchana mifumo imezimwa usiku wanaifungua, mahala ambako stendi inaingiza shilingi 1,200,000 inayopatikana kwenye *POS* shilingi 300,000. Haya ndiyo mambo yanayosababisha hizi Halmashauri zetu zinaibiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti ushauri wangu Mheshimiwa Waziri Mkuu uko hapa jamani kwenye sera zetu pesa zote zikusanywe na *TRA*, vijana hawana kazi kwenye nchi hii waajirini tu, tuna Ofisi za *TRA* sasa hivi nchi nzima, TAMISEMI waondolewe kukusanya pesa, mje muone kwa sababu Bajeti ya Halmashauri inajulikana Sengerema bilioni tatu, *TRA* atukusanyie bilioni tatu achukue *commission* yake, kinachobakia atuletee tuje tutumie, lakini kukusanya TAMISEMI hawawezi.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la *TANOIL* limekuja kwetu kwenye Kamati tumeomba sana tunaambiwa haiwezekani, leo tunakuja kuvuliwa nguo Kamati hapa kama sisi Kamati haifanyi kazi! Tumeomba sana kwenda *TANOIL*, tumeomba sana kwenda *TIPER* tumeomba sana kwenda kuangalia *flow meter* hatupelekwi katika maeneo nyeti, tumeomba sana kwenda kuangalia mifumo ya uagizaji wa mafuta, mifumo ya tenda za mafuta, kule Mheshimiwa Waziri Mkuu aende *CAG* akakague, Serikali ya Tanzania Mama yetu ame-*backup* pale tumeenda kuweka *subsidy* kwenye mafuta zaidi ya shilingi bilioni 400, zinaniuma sana hizo pesa! Watu

wameongeza pesa katika *premium* kwa kiwango kikubwa kabisa, nchi hii …

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, Tabasam…

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilindie muda wangu, akichokonoa nitaingia kwa treni nakuambia hapa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, Tabasam naomba usikilize taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Judith Kapinga, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati.

**TAARIFA**

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 68(1) inakataza Mbunge mwenye maslahi ya kifedha kuongea suala ambalo ana maslahi nalo. Mheshimiwa Mbunge, ana maslahi ya kifedha kwenye suala la *TANOIL*, kati ya zile bilioni 38 ambazo zina hati hati Mheshimiwa Mbunge, ana maslahi nazo. Kwa hiyo, tunaomba Mheshimiwa Mbunge aondoke kuzungumzia kwenye suala hili ambalo ana maslahi nalo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tabasam, taarifa unaipokea?

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siipokei. Labda niwaeleze wazi tu, mimi ni mfanyabiashara wa mafuta najulikana nimesha-*declare* humu muda mrefu, naomba muda wangu kwa sababu muda wangu upo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, malizia mchango wako, malizia sentensi za mwisho.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapana. Dakika zangu zimechukuliwa naomba sana, mimi naangalia dakika zipo hapa zimechukuliwa.

**MWENYEKITI:** Malizia mchango wako.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli nina maslahi nafanyabiashara nilikuwa na deni milioni 400 nimelipa na katika hao watu wanaodaiwa kule, kuna bilioni 78 na makampuni wamenunua vituo hewa, wamenunua vituo vya shilingi milioni 500 kwa bilioni mbili, haya maneno tunaomba iundwe Tume ya Bunge ichunguze jambo la mafuta nchini haiwezekani!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tabasam muda wako umeisha pia.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba iundwe Kamati Teule ya Bunge tufikie mwisho, tumsaidie Mheshimiwa Rais.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Tabasam. Mheshimiwa Constantine Kanyasu, atafuatiwa na Mheshimiwa Vedastus Mathayo, Mheshimiwa Noah Saputu ajiandae.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naunga mkono taarifa zote tatu, ninaomba kama ambavyo Wabunge wenzangu wamesema kila mwaka tunapochangia na kuna wakati mwingine tunaacha kabisa kuchangia kwa sababu tunaona kama tunachangia *ceremonial,* tunajikuta Wabunge na sisi ni sehemu ya kulalamika, tunalamika lakini yale tuliyoyalalamikia mwaka ulioisha utakutana nayo mwaka mwingine yanaendelea. Niombe wengine wameongea kwa hisia kali lakini naamini Serikali imeyasikia kwamba haya tunayoyazungumza, basi itafute namna ya kuyafikisha mwisho kwenye taarifa nyingine yasije tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya CAG haifanyi ukaguzi kwenye maeneo yote inachambua maeneo ya kufanya, kama ingetokea kwenye mwaka mmoja wa fedha ikaja taarifa ya mashirika yote na taarifa ya maeneo yote pengine nyumba hii

tungebanana. Sasa inatusaidia tu kuonesha mapungufu ya sheria tulizo nazo wapi tunatakiwa kuongeza nguvu kusimamia.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi kuwa Mjumbe Kamati ya Utawala na nikashauri, kwa sababu niligundua tatizo lipo wapi? Nchi hii tupo salama sana kwa sababu mfumo wakupeana taarifa kama kuna jambo la hovyo linataka kuipata nchi upo mpaka kwenye mtaa. Leo wewe ukitaka kufanya jambo ambalo lina madhara kwa Serikali haitakuchukua nusu saa watakuwa wamejua na wamefahamu watu waliopo Dar es Salaam, kwa nini, kwa sababu kuna *channel* fulani kalijengwa ambapo Serikali inaitumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wizi ni *process,* sisi tunakwenda kwenye matokeo, na unapoenda kwenye matokeo usitarajie utamaliza tatizo. Wizi unaanza huku ndani, unapopagwa mpango kwa mfano wa kujenga barabara kilometa 100, tayari kule ndani wanaanza mpango wa wizi. Wanapoandaa maandalizi ya gharama za ujenzi pale ndani kuna gharama ya wizi, wanapotangaza mpaka siku ya mwisho barabara inajengwa ndiyo maana yaani hauwezi ukaja leo hapa unazungumzia namna ya kukomesha wizi kwa sababu umengalia *process.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, amesema hapa Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda, utakuja *process* zote zipo *100 percent* lakini ndani kumeibiwa kwa sababu gani, hatuna mfumo unajitengeneza mwenyewe ndani kwa ndani wa kutuambia wezi wapo wapi. Sasa lazima tuwatengeneze hawa na nimewashauri alikuwepo Mkurugenzi wa *PCCB,* nilimshauri na watu wengine nilisema hebu tufanye *sampling* kwenye maeneo makubwa reli, wapi wapi ambapo tunafanya manunuzi makubwa, tutengeneze vijana kutoka kwenye *recruitment* huyu awe na kazi moja tu kila siku ya kuangalia ni wapi mtu anatengeneza *gap* la kuiba. *Otherwise* haya tutayazungumza mpaka tutachoka hatutamaliza wezi, kwa sababu wizi ni *process* yaani wizi siyo matokeo ni *process* inayotengenezwa tangu siku inajengwa hoja, inaanza

yaani siku ya mwisho sisi tunakuja kufikiri kumbe tuliibiwa tangu siku wazo linaanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema hivyo, kwa sababu ukiangalia taarifa nyingi na watu wengi wanaozungumzwa hata kama utawachukua leo utawapeleka Mahakamani. Ilikuwepo kesi moja maarufu sana ya Mkurugenzi wa *ATCL* nenda ukaangalie faini na kosa alilokuwa amefanya utagundua ni kichekesho, kwa hiyo, mtu anaweza kuiba hapa bilioni 100 halafu akaenda Mahakamani na Sheria inampa mamlaka Hakimu ya kuamua huyu anaweza kumtoza faini ya milioni tano, sasa *imagine* hasara ambayo tunakula! Kwa hiyo, nadhani hapo tuna shida, tupate muda wa kufumua haya mambo na kuyaangalia vizuri.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko jambo lingine moja linazungumzwa sana, kwenye deni la shilingi bilioni 88 ambazo wanadaiwa Halmashauri kwenye *ten percent*. Nilipata bahati ya kuingia kwenye kikao cha kumaliza hoja. Sasa hii hoja haitakaa iishe. Kwa nini? Mikopo mingine ni ya mwaka 2012, 2013 na 2014. Sheria inasema nini? Sheria inasema, dhamana *(collateral)* ya wakopaji ni kikundi cha watu watano na mkataba ni wa mwaka mmoja. Kwenye masuala ya fedha, mkataba ukiisha sheria inasema, una-*restructure* ule mkataba ili mkopo uendelee kuwa hai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumzia kukusanya madeni ya miaka minane, wakopaji walikuwa watano, wanne walishakufa, amebaki mmoja. *Collateral* ilikuwa ni watu watano, hivi hiyo hoja inakaaje kwenye vitabu vya CAG? Yaani hiki kitu kipo *very obvious, unless* tunasoma tofauti sheria, tunasoma tofauti hizo karatasi. Kwa hiyo, dhamana yangu mimi, nimeenda kukopa, ni kikundi cha watu watano. Unatakiwa ndani ya mwaka mmoja *follow-up* yako uhakikishe wale watu wana-*survive*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama biashara ile huendi kuitembelea kwa miaka minne au mitano, leo umeng'ang'ana na hoja ya shilingi bilioni 88; mwaka 2012 mimi nilikuwa na miaka 40, leo nina miaka 53. Kijana aliyekopeshwa wakati ule, leo ni mtu

mzima. Mama aliyekopeshwa wakati ule, leo ameshazeeka. Sasa matokeo yake ni nini? Nguvu inayotumika ni kubwa. Watu wanakamatwa, wanawekwa kwenye ofisi ya vijiji wanafungiwa humo usiku kucha, wanaambiwa kauze hiki, kauze hiki, halafu mtu mmoja huyo analazimiswa alipe deni la watu watano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu *CAG* aangalie vizuri hapa, kuna shida. Shida iliyopo hapa ni kwenye kutafsiri sheria. Hata benki ukikopa, kuna muda wanajua hili deni chechefu *(bad debt)* ndiyo maana ana *insurance.* Yaani likifika mahali wanaona huyu ni *non-performing,* wanaliondoa kwenye vitabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa utakuta kwenye Halmashauri mnajadili hoja ya mwaka 2010, halafu unajua majibu ni nini? Majibu ni maandishi, hayarudishi hela, hayamwajibishi mtu. Anakwambia, tunajibu hoja, hii hoja ina miaka mitano. Unajibu nini pale wakati waliokuwa wanahusika wameshastaafu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna haja ya kujitazama vizuri kuona kuna shida. Hii sheria ya mikopo ukiisoma, hakuna sehemu ambapo unaweza ukageuza hili kosa likawa *criminal* ukampeleka mtu Polisi, ukamweka Mahakamani, haipo. Imefanya hivyo kwa sababu wanaokopa ni watu maskini. Kwa hiyo, lazima u-*implement in a single year* na ukishindwa ku-*implement* uli-*structure* huo mkopo ianze *zero,* aendelee. Kama ameshafilisika, analala njaa, unafanyaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, mwaka jana 2022 tulipata hati ya kualikwa Ikulu kwenda kushuhudia uwekaji wa sahihi ya huduma ya maji pale Geita. Tukaambiwa hawa watu watafanya kazi kwa muda wa miezi 36 Mji wa Geita utapata maji. Leo nazungumza, bado wanapima udongo. Sasa huyu mtu, yaani hapa hapa tayari huyu mkandarasi ameshaanza ku-*default*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachozungumzwa na Kamati, haya ma-*interest* na mengine yanayokuja baadaye, tushichangae kwa sababu *it is likely* kuna vitu tunavianza bila kujiandaa na matokeo yake vinatutengenezea gharama. Hili ni tatizo tu la sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, kwenye taarifa ya Geita Mji, inaonesha kuna hati yenye mashaka, lakini unajua sababu yake ni nini? Kanuni na Sheria mbaya ambayo ipo kwenye Kanuni za *CSR* yule *Mining Right Holder* ndiye mwenye hela na ndiye anayeajiri mkandarasi, halafu Mkaguzi wa Serikali anakwenda kukagua Halmashauri, anaiandikia Halmashauri kwamba hapa mmekosea. Mmeshaona wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu sheria ingesema, wewe *mining right holder* tenga bajeti, Halmashauri tangazeni, simamieni, halafu Mkaguzi aje akague Halmashauri. Unamkaguaje halmashauri ambaye *Mining Right Holder* ame-*implement* kila kitu huku! Kwa hiyo, unaona tunazikosea hizi sheria tangu mapema. Tunategeneza mianya *(loophole)*, halafu tunakuja kuumana humu, kila Mbunge analalamika, hatufiki mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kanyasu kwa mchango wako mzuri. Mheshimiwa Vedastus Manyinyi, atafuatiwa na Mheshimiwa Noah Saputu, na Mheshimiwa Nancy Nyalusi, ajiandae.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia katika hizi hoja tatu za *PAC, LAAC* na *PIC*. Kwanza nianze na hili suala la *Tanoil,* sihitaji kulisemea sana, lakini nilichokigundua ni kwamba kwa bahati mbaya sana Serikali ikiwa imeamua jambo lake, hata kama mngeshauri mnalia, haitakubali, yaani lazima lifanyike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi kwa bahati nzuri katika kipindi kilichopita nilikuwa Mjumbe wa Kamati ya Nishati na Madini. Ilipokuja tu ile kwamba *Tanoil* wapewe uwezo wa kuanza kufanya biashara, nenda kwenye *Hansard* pale utaona ni kwa namna gani nilivyokataa kabisa na nikawathibitishia kwamba hata wafanyaje hiyo ni Serikali imeamua kubeba hasara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tayari tumeshabeba hasara, ndiyo tunaanza kulizungumza hapa. Kwa hiyo, ndiyo maana nasema kwamba kumbe Serikali ikishaamua jambo lake, sisi pamoja na kwamba kazi yetu ni kushauri, pamoja na kushauri huwa siyo rahisi sana haya tunayoshauri yakaweza kuchukuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine katika yale mambo, maana taarifa hii tunayoijadili hapa ni taarifa ambayo ilikuja mwezi wa Tatu. Baada ya *CAG* kuwa amei-*table* mwezi wa Tatu, baada ya hapo watendaji huko Serikalini wameendelea kuifanyia kazi. Wameifanyia kazi, sasa leo tumepata nafasi ya kuijadili baada ya zaidi ya miezi sita; lakini wakati watendaji wanafanya kazi au wanayafanyia kazi haya pamoja na Kamati, Kamati iliwaonesha wale watendaji kule Serikalini wakawa wanajibu. Mwisho wakakubaliana kwamba huu ni upungufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine nakuja kushangaa ninapoona Serikali inaanza kutetea hata baadhi ya mambo ambayo yapo wazi wazi, ndiyo maana nafikia mahali nasema, au hizi taarifa huwa siyo sahihi? Kama siyo sahihi, kwa nini wajadili kule kwenye Kamati na hatimaye wakubali kuzileta hapa Bungeni? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano inaonekana kuna upotevu wa shilingi bilioni 11, haya ni mapato yaliyokusanywa kupitia *POS*. Yaani fedha zilikusanywa halafu hazikuwasilishwa, *eleven billion*. Unakuja unaona hapa kwamba kuna mawakala wa ukusanyaji wa mapato kule tumewaweka, wakakusanya *4.9 billion* halafu hizo fedha hazikuwasilishwa. Yaani wamekusanya tu wakaweka mfukoni. Yaani *POS* kwa muda mrefu watu wamekuwa wakikuanya fedha wanaweka mfukoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana huwa nashangaa kidogo, hawa watendaji wetu, kwa maana ya viongozi wetu wanapoona kama hayo kama siyo makosa. Sasa mimi najiuliza, kama ni upungufu wa utaratibu, watu wote hawa ambao tumewapa dhamana ni wale ambao wamesoma, ni nafasi zao za kazi walizosomea. Watu kama hao wanafanya hayo makosa na kesho wanaendelea kuwepo kazini. Wakati huo tuna vijana wengi

wako mtaani hawana ajira na wamesoma vizuri. Kama kweli hatua zingekuwa zinachukuliwa, maana yake ni kwamba tulitegemea kuona ile ripoti tuliyoijadili mwaka jana 2022 tulipaswa kuona hatua zinachukuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unatuka mtendaji yule yule alikosea hapa, huyo huyo kesho unamwona bado yuko kazini. Kwa mfano, kati ya wale ambao wakati ule tulibishana wanasema jamani eeh, hii *Tanoil* hata mfanyaje ni fedha za Serikali zinapotea, kilichofanyika, unamwondoa tu hapo unamweka pembeni, maisha yanafanyaje? Maisha yanaendelea. *(Makofi)*

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mathayo kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Ester Bulaya.

**TAARIFA**

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa baba yangu kwa mchango mzuri. Analolisema ni sahihi. Kuna mfanyakazi kutoka Halmashauri moja ya Kigoma alikuwa *DT,* mdogo wake alikuwa ana makosa ya kuiba pesa za *POS* takribani shilingi milioni nane, kwa sababu yeye ni *DT* akaingia kwenye mfumo, akaondoa hiyo dosari, halafu vile vile huyo *DT* ametoka huko amehamishiwa kwenye mkoa mwingine wa Mbeya. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mathayo, taarifa unaipokea?

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo taarifa naipokea. Hayo yote ni madhaifu yanaendelea kuonekana. Nitoe tu mfano, mwanangu amenikumbusha pale hata juzi Bunda, *can you imagine lorry* la mifuko 600, yaani *lorry* zima, asingekuwa yule *DC* wa Bunda, maana yake ile tayari ilikuwa imefanyaje? Ilikuwa imeenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kushangaza sasa utaona tu hiyo kesi inaenda, basi hilo suala linaisha. Linapoisha, tayari

unakuta wale wahusika wote wamehamia mahali pengine halafu maisha yanafanyaje? Maisha yanaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri kama Serikali mwangalie, kusema kweli wananchi wetu wana taabu nyingi. Wananchi wetu wamejaa umaskini, kule mahospitalini hakuna dawa, sasa wanapoona fedha zinapotea kwa kiasi hiki, kusema kweli ni dhahiri kwamba hata wao hawako tayari kutuelewa. Kwa hiyo, tunapokuwa tunazungumza mambo haya ni vizuri na ninyi mlioko huko Serikalini tukawa kitu kimoja, tukaona namna bora ya kupunguza matatizo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine nafika mahali nasema Serikali wakati mwingine inaendelea kuonesha udhaifu wake. Kwa mfano, linapozungumzwa suala la *Force Account* halina tija kuliko kupewa wakandarasi, kumbuka kwamba unapotumia *Force Account* kule Halmashuri wapo watendaji na wataalamu wa ngazi zote. *Force Account* maana yake unatumia gharama halisi. Sasa leo gharama halisi inakuwaje kubwa kuliko gharama ya mkandarasi? Kwa hiyo, hiyo tu inaonesha ni kwa kiasi gani Serikali imefika mahali ina-*surrender* kabisa, inanyanua mikono kwamba… *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mathayo kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Ndejembi, Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

**TAARIFA**

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpa mzungumzaji taarifa kwamba *Force Account* imeiokolea Serikali fedha nyingi sana, hasa katika ujenzi wa miradi mbalimbali iliyokuwepo chini ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia *BOQ* ya wakandarasi na *BOQ* ambazo zinatengenezwa kwa ajili ya ujenzi wa miradi hii

kama madarasa, ujenzi wa madarasa kwa wakandarasi ni mara mbili au mara tatu kulingana na gharama ya *Force Account*. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mathayo, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda mdogo wangu hakunielewa. Mimi nimesema, ninashangaa kuona Serikali inakataa; yaani inafika mahali inasema kumtumia mkandarasi ni gharama wakati *Force Account* inatumia gharama halisi. Kwa sababu inatumia gharama halisi, maana yake ni *cheap*, lakini kwa sababu mnashindwa kuwasimamia, ndiyo maana mnatumia *Force Account* lakini bado wizi unatokea. Kwa hiyo, mjitahidi kutumia *Force Account* lakini muwe makini ili wizi usiendelee kutokea. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mathayo kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa wanatumalizia muda wetu kwa kweli.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana mchangiaji kwa sababu hiki anachochangia ndiyo uliokuwa msimamo wa Serikali kuanzia jana na wakati tunapitisha sheria. Tunakushukuru umesaidia kuwaambia Wabunge wengine waliokuwa wanaipinga hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, msimamo wa Serikali, hata jana nilisema pale kwamba ujenzi wa madarasa, zahanati unaojengwa kwa *Force Account* gharama yake inawezeka ikawa nusu au chini kwa zaidi ya mara tatu ingejengwa kwa kutumia mkandarasi. Tukasema, Bunge lilitushauri mwaka jana 2022 hapa tukaweka ukomo ili kuweza kudhibiti miradi mikubwa zaidi isijengwe kwa *Force Account*. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mathayo muda wako umeisha, Muda wako umeisha, malizia sentensi moja ya mwisho.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe tu ushauri wa mwisho ambao labda unaweza ukatusaidia kwamba, wakati mwingine hizi shida ambazo zinajitokeza, hasa hizi za ma-*accounting officer,* ni vizuri kutabadili utaratibu, ma-*accounting officer* wakaomba kazi hiyo na wakapewa mkataba, kama ni wa miaka mitatu au miaka mitano, amefaulu aendelee, hakufaulu asiendelee. Bila hivyo, maana yake hili tatizo litaendelea kuwepo na ni tatizo ambalo litaendelea kuiumiza nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Noah Saputu, atafuatiwa na Mheshimiwa Nancy Nyalusi, na Mheshimiwa Ester Matiko ajiandae.

**MHE. NOAH S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu. Vile vile kwa mara ya pili nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anayoifanya katika Taifa letu na tumwombee kila la heri katika kazi hii ambayo ni ngumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa maneno ya Hayati Baba wa Taifa, Julius Kambarage Nyerere, alisema kwamba msije mkasema kwamba watu wa awamu ya kwanza hakuna wala rushwa, ila tulikuwa wakali, wakali kweli kweli. Akasema, wakati mwingine hatukumwachia hakimu aamue mwenyewe. Tukasema lazima ahukumiwe viboko 24, akiingia jela apigwe 12, akitoka apigwe 12 akamwonyeshe mkewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inasikitisha kwa sababu mambo mengi yaliyokuwa yanazungumwa tangu jana katika Bunge hili, mambo ya ubadhilifu na wizi na ujambani na ufisadi, kama kweli tungekuwa tunaona uchungu, hizi taarifa za mwaka 2021/2022 leo tungekuwa tunazungumza jambo lingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia taarifa hii, watu wameiba zaidi ya kwenye eneo la manunuzi. Watu wanaiba kweli kweli bila huruma, bila hata haya. Mtu anaiba hata zaidi ya shilingi bilioni ya 104. Ni karibu shilingi bilioni 11, shilingi bilioni 6.6, shilingi bilioni 3.3, wanaiba zaidi mpaka imefika kwa kisehemu kidogo tu, imefika zaidi ya shilingi bilioni 253.353. Hiyo ni sehemu kidogo tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua hazichukuliwi. Pamoja na hayo, sisi tunaamini kwamba Chama cha Mapinduzi hakijwahi kuunga mkono ufisadi, wala wizi, wala ujambazi kwa sababu katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi sura ya 116 Ibara ndogo ya (b) nimechukua sehemu kidogo, anasema, nanukuu: "Chama Cha Mapinduzi katika kulinda katika kipindi cha miaka mitano ijayo, kwa kutambua kuwa rushwa ni adui wa haki na kwamba hakitavumiliwa vitendo vya rushwa na ufisadi kwa namna yoyote ile, ili kufikia malengo hayo, CCM itaelekeza Serikali kuchukua hatua hatua zifuatazo:"

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataja moja tu, akasema, "kudhibiti matumizi mabaya ya ofisi na upotevu wa fedha za umma na kukabili vitendo vya rushwa." Sasa kama mpaka Ilani ya Chama imesema, ina maana sisi tuliopewa dhamana na Mheshimiwa Rais katika nchi hii hatuoni kwamba tunapaswa kuchukua hatua katika kipindi chote cha Ripoti ya CAG ya kwanza, ya pili na ya tatu? Hatuoni hapo kuna maswali mengi ya kujiuliza sisi sote? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wale wasomaji, katika Biblia, inasema: "enyi Wagalatia, nani aliyewaloga msitambue hata wokovu mkuu namna hii? Hata leo wale Wagalatia wanaambiwa, sisi Watanzania nani walituloga tusitambue rasilimali za nchi hii ambazo zinatafunwa na baadhi ya watu wachache? Leo zingepatikana hizo fedha ambazo mafisadi wamekula, zingejenga hospitali, ingepeleka dawa, ingefanya kila kitu ambacho ni kwa ajili ya jamii na manufaa ya Taifa hili, lakini tunanyamaza kimya. Ninyi wahusika ambao mmepewa dhamana na Mheshimiwa Rais kumsaidia, mliopewa dhamana na Taifa hili kusaidia Taifa hili, mmelifikisha wapi kwa kutochukua hatua? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa la China wana adhabu tatu. Mtu akiiba mali ya umma, ukiachana na makosa mengine, wanasema utafungwa maisha ikiambatana na kufilisiwa; ya pili, wanasema, utauwawa hadharani. Utapelekwa uwanjani pale, unapigwa risasi, unamiminiwa mitutu mpaka huo wizi na ujambazi na ufisadi ukome. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kweli tuko *serious* katika Taifa hili na kila mmoja awe na uchungu, tulipokuwa kwenye Kamati ya *LAAC,* unasoma taarifa mpaka kichwa kinauma, moyo unatetemeka, unapata *pressure*, wengine wakawa wanasema wanaenda kumeza vidonge, tunakaa mpaka saa sita usiku, haya yote ni kwa sababu ya uchungu ya Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Wamasai tuna neno moja ambalo tunasema (Wamasai walioko humu watanielewa), kama likitokea jambo la hatari katika jamii ya kimasai, kuna milio miwili tofauti akina mama wanalia. Kama ng'ombe wakiibiwa kuna mlio wake, kama ni mtu amekufa, kuna mlio wake ambao akina mama wanalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kila sauti ilisikaka katika hili jumba la Bunge. Je, mnataka kuniambia kwamba leo tunatwanga maji kwenye gunia na kwamba keshokutwa tutarudi tena hapa tusomewe Taarifa ya *CAG* halafu hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii ilipowasilishwa kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ni nani ambaye hakumsikia Mheshimiwa Rais alivyoumizwa na ufisadi na wizi siku hiyo? Ni nani ambaye hakumsikia Mheshimiwa Rais akitoa maneno makali na ya huzuni na kusikitika siku hiyo alipokabidhiwa taarifa hii? Kila mtu mwenye masikio aliyesikia taarifa hii ilipowasilishwa, Watanzania walikuwa wanasema, hili Bunge limekaa kimya, mbona lenyewe halijadili Taarifa ya *CAG* na imeshawasilishwa? Sasa leo tuko kwa ajili ya taarifa hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima kama Watanzania tufike mahali tuwe na uchungu na Taifa hili, tuwe na uchungu na watoto wa Taifa hili ambao hawana dawa, hawana madawati

ya kusomea na wengine wanakaa chini katika maeneo mengine. Madarasa yametoboka, vyoo ni vichache kwenye maeneo mengine na maeneo mengine hakuna kabisa, lakini mafisadi tumewaacha waki-*relax,* wakihitimisha ule wimbo unaosema, "wacha ni-*enjoy,* maisha yenyewe mafupi." *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ina maana kwamba sisi tunawaangalia tu, wanaendelea ku-*enjoy* maisha haya, huku wananchi maskini wanaendelea kuteseka. Kwa kweli inaniuma na niendelee kusema, kama tutaendelea na tabia hii ya kutokuchukua hatua, ni bora Bunge hili likanyamaza kimya bila kujadili taarifa hizi kama tukifika hapa hatua hazijachukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali, katika Bunge lijalo tulete taarifa kwamba hao mafisadi, wezi na majambazi wameshughulikiwaje katika kipindi hicho cha Taarifa ya *CAG* ili tuweze kuona kwamba kweli Serikali inakitendea haki Chama cha Mapinduzi, inamtendea haki Mheshimiwa Rais na inalitendea haki Bunge hili. Kama msipochukua hatua, ina maana hamumtendea haki Mheshimiwa Rais, hamkitendei haki Chama cha Mapinduzi na hata sisi hamtutendei haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachotaka kusema ni kwamba, hali ya Taifa hili, kila anayekuja anafanya Taifa hili kama shamba la bibi. Sasa ifike mahali Bunge hili lihakikishe kwamba tatizo hili la wizi, ufisadi na rushwa vinakoma.

Mheshimiwa Mwenyekliti, baada ya kusema hayo, naomba niseme, naunga mkono hoja za Taarifa zote tatu, lakini naomba waliohusika wachukuliwe hatua kali na za haraka kwa mujibu wa sheria za nchi yetu na ikiwezekana iletwe sheria hapa ya kuongeza nguvu, watu wahukumiwe na ikiwezekana hata kama ni kunyongwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mtu ameiba dawa za hospitali, si ameua watu waliokosa dawa hospitali? Kama wameweza kuiba labda vifaa vya shule, si wamewakosesha watoto madarasa? Kama wamefanya huo wizi wa kila kitu, wamewadhulumu Watanzania wangapi? Sasa kwa nini nao

wasiuawe? Biblia inasema, mshahara wa dhambi ni mauti. *(Makofi)*

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Saputu, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Amar.

**TAARIFA**

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli mzungumzaji anazungumza kwa uchungu. Nimpe tu taarifa kwamba wizi huu, katika Halmashauri ya Nyang'hwale hivi ninavyozungumza, zimeibiwa *computer* saba kwenye Ofisi ya Mkurugenzi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Noah, unaipokea taarifa?

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipokea taarifa na ninampa pole. Pole sana. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, tulienda ziara kule Mlele, kule Katavi sijui wapi, tukakuta Mkurugenzi amefanya wizi wa majengo zaidi ya bilioni, wakati huo Serikali imepeleka karibu shilingi bilioni nne na kitu, lakini hospitali ni magofu na ilikuwa ni mpya, matofali yameibiwa, lakini yule Mkurugenzi amehamishwa, amepelekwa kwingine kusikojulikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwingine alikuwa pale Tunduma, ametolewa pale amepelekwa kule Momba kwa dada yangu Mheshimiwa Sichalwe.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Noah, ahsante sana.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hii taarifa ya uhamisho haisaidii. Mtu ahukumiwe hapo hapo *tit for tat*, atacha wizi na ujambazi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Noah ahsante sana. Mheshimiwa Nancy Nyalusi, atafuatiwa na Mheshimiwa Esther Matiko, na Mheshimiwa Innocent Bilakwate, ajiandae.

**MHE. NANCY H. NYALUSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia hoja hizi ambazo ziko Mezani. Nampongeza sana *CAG* na kikosi chake kizima kwa kazi kubwa na nzuri waliyoifanya ya kuweza kubaini madudu haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo mawili, jambo la kwanza ni riba kwa wakandarasi. Ucheleweshaji wa malipo ya wakandarasi umesababisha riba ya shilingi bilioni 68.77 kwa Serikali, kwa taasisi 12. Hapo bado hatujazungumzia halmashauri na Wizarani. Kwa hiyo, hali ni mbaya na hili tatizo ni kubwa na limeendelea kukua siku hadi siku. Ifike mahali watendaji wa Wizara wamwonee huruma Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Rais, anahangaika usiku na mchana kuhakikisha kwamba anatafuta pesa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Watendaji mnaosimamia mnamwangusha Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina ushauri, naomba ufanyike ukaguzi maalum kwenye taasisi zote 12 ili tujue chanzo cha tatizo ni nini? Tuweze kutatua tatizo hili. Maana inaonekana inaweza kuwa ni chaka la watu kuiba pesa za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni *KADCO*. Bunge la 12 Mkutano wa Tisa, tarehe 2 Novemba, 2022 Bunge liliazimia kwamba shughuli zote za Uwanja wa *KIA* zisimamiwe na *TAA*, lakini hadi kufikia Septemba, 2023 shughuli za *KIA* bado zilikuwa zinasimamiwa na *KADCO*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba utakapompa nafasi Mheshimiwa Waziri, aje atuambie, *KADCO* inasimamia Uwanja wa *KIA* kwa utaratibu upi na kwa mkataba upi? Kwa masikitiko makubwa, Wizara husika imepuuzia Azimio la Bunge kwa sababu hawajafanyia kazi utekelezaji huo na hakuna taarifa yoyote. Hii ni kuonesha dharau kubwa kwa Bunge letu Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani tunakaa hapa tunaumiza kichwa, tunatoa maazimio lakini hakuna kitu

kinafanyiwa kazi. Kwa hiyo, tunaomba Watendaji kwenye Wizara, lazima muone namna ambavyo sisi tunahangaika kwa ajili ya mambo haya na jinsi ambavyo tunaumiza vichwa kwa ajili ya haya mambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja taarifa zote tatu na mapendekezo yote ambayo yametolewa kwenye Kamati.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nancy Nyalusi, ahsante sana. Mheshimiwa Esther Matiko, atafuatiwa na Mheshimiwa Innocent Bilakwate na Mheshimiwa Phillipo Mulugo ajiandae.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa nami kuchangia ripoti hizi tatu kutoka Kamati ya *PIC, PAC* na *LAAC*. Kwanza kabisa niseme naunga mkono hoja, mapendekezo na maazimio yote ya Kamati hizi tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tunatambua kuanzia jana, Waheshimiwa Wabunge, tumepata hasira sana kutokana na madudu ambayo yametokea katika hizi ripoti. Kwa mfano, kwenye Kamati yangu ya *PAC,* hiki tulichokileta hapa ni asilimia chache sana. Mathalani, katika Ukaguzi wa *CAG* kwenye Serikali Kuu tumeweza kupitia mafungu 18 tu ambayo ni asilimia tano tu ya mafungu 339 yaliyoletwa. Sasa mnaweza mka-*imagine* hii ni asilimia tano tu ina haya madudu, je, tungepitia ripoti yote ya *CAG*? Ukija kwenye Mashirika ya Umma na Taasisi, tumepitia 39 tu *out of 203* takribani ni asilimia 19 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata *CAG* mwenyewe anafanya *sampling* kama tulivyoeleza hapa, na Kamati ya *LAAC* wanasema ni *only 40%* pamoja na kwamba walikuwa wanatoka *midnight*. Kwa hiyo, mnaweza mkaona kuna ni kwa kiasi gani kuna ubadhirifu mkubwa sana wa fedha za Watanzania maskini ambazo zinakuwa zikifanyika kwa kujirudiarudia. Wabunge tunakaa hapa tunasema, lakini utekelezaji *(action)* ambao unachukuliwa ni mdogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mathalani, kwenye Ripoti yetu ya *PAC* tumepitia taasisi tano tu ambazo zimeainishwa hapo na zikaonesha dosari ambazo zimejitokeza kwenye kukusanya mapato na kusababisha hasara kwa Serikali takribani shilingi trilioni 1.9, kwa Mashirika matano tu; *TRA, TBA,* Tume ya Madini, *TAWA* na *TANOIL*. Shilingi 1,009,620,000,000, fedha hizi kama tungeziwekeza hata kujenga ukumbi wa mikutano wa kimataifa tungekuwa tunakuza utalii wa mikutano. Leo tunavyoongea, Spika wetu ni Rais wa *IPU*, tungeweza kuleta hata mikutano ya *IPU* hapa, lakini sasa hivi *we cannot do that*, kwa sababu hapa hatuwezi ku-*accommodate* mkutano mkubwa kama ule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, hizi fedha tungesema tuziwekeze kwenye michezo ya kukuza utalii wa kimichezo, tungejenga angalau *arena* tano kama zile za pale Rwanda ambayo ingekuza uchumi, utalii wa kimichezo na vipaji vya Watanzania, lakini leo uzembe tu unatokea, zinapita tu. Tunaongea hapa inaenda, mwakani ripoti nyingine itakuja tutaongea *the same*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge tunatakiwa tu-*take action.* Serikali iwawajibishe watendaji wote wanaofanya ubadhirifu huu kwa sababu hapa tumesema sana. Ni kweli Mama anahangaika kutafuta fedha, lakini pia Watanzania ni maskini na wanalipa kodi ili tufanye maendeleo. Leo kule kijijini unakuta Mtanzania anakamatiwa kuku ili kuchangia kujenga darasa au *dispensary, yet* tunapoteza *trillions of money* kwa uzembe. Hii haikubaliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hizo taasisi tano nimezungumzia *TAWA,* mathalani uzembe mdogo tu. *TAWA* waliendesha mnada kwa njia ya ki-*electronic,* kuuza hivi vitalu vya uwindaji wa kitalii. Kuna kampuni inaitwa *MS Game Hunters Limited* ikachukua vitalu saba *and then* ika-*default* kulipa, yaani kwa makusudi tu wakasema hawawezi kulipa, dola 500,999 takribani ni shilingi bilioni moja laki tano sabini na kitu. Leo wamekuja kwenye Kamati tunawauliza kwa nini mwaka wote umepita hadi imekuja hoja ya kiukaguzi? *Simply* wanasema walikuwa hawana *legal stand* ya kuchukua *against* huyu mtu aliye-*default*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna watendaji Serikalini, tuna wanasheria; tunawauliza ehe, *thereafter,* na huu siyo muda wa kwanza kufanyika kwa njia ya ki-*electronic,* ni mnada wa tano. Huu ni mnada wa tano. Yaani wa kwanza, wa pili, wa tatu, wa nne, wa tano ndiyo ikatokea huyo *defaulter* mmoja. Wanakuja wanasema, "*no*, ilikuwa haijawahi kutokea, tulikuwa hatujaweka hizi *legal stands.* Sasa hivi ndio tunajikusanya tetengeneze kanuni, tushirikiane na Wizara ya Fedha." *Are we serious?* Kama nchi *we are not serious* kabisa. Serikali, *you are not serious, I can say that. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezungumza hapa kuhusu riba. Kwenye Kamati ya *PAC* tume-*indicate* riba mbili tu; riba ile ya *TANESCO* na *Pan Africa* shilingi bilioni 113.8, kuna riba ya *TANROAD* shilingi bilioni 36.8, ukijumlisha ni shilingi bilioni 150.6. Hizi pia ni hela nyingi sana. Ukisema ukajenge madarasa, ukisema ukajenge vituo vya afya uwasaidie akina mama wajawazito wanaofariki na wazee kutembea muda mrefu kutafuta huduma ya afya zingesaidia. Fedha nyingi zinapotea kwa uzembe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Pan Africa* wameingia mkataba na *TANESCO* na mnaandika hii mikataba na wanasheria wenu, kwa nini mnaingia mikataba ambayo mnajua kwamba hamtaweza kuikidhi? Amesema Mbunge wa Kinondonihapa, ankara zaidi ya 115 kwamba, *the moment* wanatoa ankara, ukifanya ucheleweshaji unatozwa 9*.1 percent*. Sasa hizi riba zimeji-*accrual* mpaka shilingi bilioni 113. Yaani malipo shilingi ni bilioni 246, shilingi bilioni 132 ndiyo *cost* halisia, *out of it* shilingi bilioni 113 ni riba, *so at a time* unaweza ukajiuliza au ni chaka la mtu? Halafu tulipowauliza, Bodi inasema," hatuna majibu kwa sababu tuko kwenye majadiliano." Majadiliano gani? Mmeingia mkataba, lazima mlipe riba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TANESCO* inauza umeme tena kwa bei ghali zaidi. Kama una-*receive gas* unatengeneza umeme, unapopata *revenue* kwa nini usijipange kulipa hivi ili ku-*avoid* hiyo riba? Lazima tuyakatae haya, tena kwa sauti kubwa sana. *The same applied* kwenye *TANROADS*, umeelezea hapa. Ni

lazima tuhakikishe kwamba mikataba tunayoingia tuna-*avoid* kupata hizi riba, halafu zinakuwa ni za mabilioni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikia kengele imegonga lakini la mwisho ni vishikwambi. Hii nayo ni hoja ambayo hata nashindwa kuielewa. Vishikwambi 300,000 ambavyo vilikuwa *procured* kwa ajili ya sensa ambayo ilifanyika hapa kwetu Tanzania, vina upungufu mwingi sana wa mfumo mzima wa ununuzi. Kwanza walifanya kwa mfumo wa manunuzi ya dharura.

Mhesimiwa Mwenyekiti, hivi kweli Watanzania tunajua sensa ni kila baada ya miaka kumi, leo unakuja kabisa bila aibu unasema eti, "tulifanya kwa manunuzi ya dharura." Manunuzi ya dharura! *Yet* wakafanya kwa kuvigawa kwa *lots* sita kwamba vishikwambi viweze kupelekwa kwa elfu hamsini, elfu hamsini, elfu hamsini, wakati kama wangefanya *bulk* ya pamoja, ingeweza kuwa na *cost* ambayo ni ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawakuishia hapo, kama jana walivyokuwa wanaongea wenzetu hapa, wanatoa mikataba bila *performance security*.

**MBUNGE FULANI:** Ayaa!

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki kitu kimekuwa ni ugonjwa sugu sana kwenye Serikali, sijui wana shida gani? Kwa mfano, kuna mzabuni mmoja ana jina la kichina sijui kama nitaweza kumtamka huyu *(Silvech Technology whatever),* alipewa na akaambiwa a-*deliver* ndani ya *40 days*, lakini akawa amechelewa kuleta hivyo vishikwambi 150,000, wakashindwa hata kumkata hata hiyo *liquidated damage*. Kwa nini? Hawana maelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Waheshimiwa Wabunge, ni lazima tukae tukatae. Ikitokea hizi hoja tumeziainisha zote na maazimio yamepita, wakija mwakani hawajafanya lolote, lazima wawajibike. Kwa sababu Watanzania maskini wametuleta hapa Bungeni kuhakikisha kwamba rasilimali za nchi yetu zinatumika vilivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni ombi. Kama kuna uwezekano, tubadilishe hii sheria, angalau CAG akishakuwa ame-*table* ripoti yake, tuwape tu mwezi mmoja wajitafute kuanzia Aprili au Mei tuanze kuipitia hii ripoti ili tuweze kuitendea haki, twende kwa ufanisi zaidi ili tukija kusema hapa tuwe tumeipitia kwa kina zaidi kuliko sasa hivi tunavyofanya kwa *piecemeal.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko, ahsante sana kwa mchango wako. Mheshimiwa Innocent Bilakwate atafuatiwa na Mheshimiwa Phillipo Mulugo na Mheshimiwa Mhandisi Stella Manyanya ajiandae.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Napongeza Taarifa zote ambazo zimeletwa na kwa kweli wamefanya kazi kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mungu ambaye amenipa nafasi hii nami niweze kuchangia. Wakati mwingine unasema Mungu nisaidie nisije nikaongea vibaya, lakini kuna vitu ambavyo vinaumiza, vinasikitisha na vinaleta aibu kubwa kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani kila siku Mheshimiwa Rais anashinda anapambana kutuletea vyumba vya madarasa, atujengee shule mpya, lakini kumbe anapozileta hizi fedha, kuna vibaka, wezi na majambazi wamejaa kwenye halmashauri zetu. Haya, mambo yanaumiza sana. Ninaamini Mheshimiwa Rais ana maumivu makubwa sana, tuna kila sababu ya kumwombea. Hivi vitu vinasikitisha na wakati mwingine unaona mtu anasimama anataka kujilinda, sasa unajiuliza hivi kweli ina maana hii ripoti iliyoletwa hapa siyo yenyewe, au ni ya kutungwa? Kabla sijaendelea sana, naiomba sana Serikali, mtusaidie na mumsaidie Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu Mungu amwamini katika taarifa hili. Watanzania tumekuamini na Mheshimiwa Rais amekuamini. Umekuwa ukichukua hatua

mbalimbali za kukemea uovu katika Taifa hili. Tunakuomba sana, tutakapomaliza kuhitimisha hoja hii, ukae na timu yako msafishe Taifa hili, maana hali ni mbaya. Haya mambo tunayoyazungumza wakati mwingine watu wanacheka wanafikiri ni mambo mazuri, lakini yanalitia aibu Taifa. Usiogope, Mungu atakusaidia. Simama na timu yako ya Mawaziri mkafanye maamuzi magumu ya kumsaidia Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani mambo yanafanyika ovyo ovyo halafu watu wanaendelea. Naomba sana tusimalize kuongea hapa yakaishia hapa. Tunataka tujue taarifa iliyopita ya *CAG,* aliyoileta, tujue jina la kila mmoja aliyehusika na amechukuliwa hatua gani. Haiwezekani tunachangia hapa halafu yanaishia hapa, lazima tujue hatua zipi ambazo zimechukuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuja kushangaa kama hili litakubalika na Mheshimiwa Spika ukalikubali hili. Utakuta mwingine ametoka Kigoma amepelekwa Mbeya. Hakuna vitu vilivyofanyika. Haya mambo ni ya aibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimejiuliza swali moja, unakwenda kwenye halmashauri *POS* imezimwa siku nne mpaka siku 1,905; huyu Mkurugenzi alikuwa amekufa, Mhasibu alikuwa amekufa na wote kwenye ile halmashauri walikuwa wamekufa. Ni miaka mingapi? Hawa watu walikuwa wapi? Haya ni mambo ya aibu. Hiyo ni hiyo ni Chamwino. Ukienda Uvinza, 1,133. Huyu Mkurugenzi alikuwa wapi? Hawa Wakurugenzi, Wahasibu na hawa watu gani wote wamechukuliwa hatua zipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo ambalo linasikitisha. Pia, hizi usifikiri walizizima kwa bahati mabya. Hii ilikuwa ni njia ya kutengeneza kula hela, ndicho kilichokuwa kinafanyika hapa. Haiwezekani wote wamekaa kimya na hakuna kinachojulikana kwa siku elfu moja naa! Haya ni maajabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine ambalo nimejiuliza, mtu yeyote unapofanya biashara ni lazima ufanye biashara yenye faida. Hakuna anayefanya biashara mwaka wa kwanza anapata hasara, mwaka wa pili anapata hasara, mwaka

wa tatu anapata hasara halafu bado anaendelea na biashara hiyo. Haya mashirika ambayo yanatengeneza hasara, wanaendelea kula, wanaendelea kunenepa si mkayafute? Yanafanya nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nashindwa kuelewa, mnasema wametengeneza hasara na hakuna faida. Tafuteni na wekeni utaratibu mwingine ambao unaweza ukatupatia faida. Vile vile, ukija kuangalia haya mashirika ndio wale ambao wanajilipa hela nyingi sana, ndio walionenepa na wamewanda, hawajui kinachoendelea. Haya mambo hayakubaliki. Kwa hiyo, mimi niombe sana Serikali iliangalie hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine. Mheshimiwa Waziri Mchengerwa, unafanya kazi nzuri. Nendeni mkaboreshe mifumo ya makusanyo. Kama mmeshindwa, njoo tuwawekee mikono tuwaombee ili Mungu awape hekima na maarifa ya namna ya kwenda kufanya kazi. Kwa sababu hawa watu wanaoiba na wao wanakwenda huko kwa waganga wanaroga; sasa, njoo tuwawekee mikono mapepo yatoke ili mwende mkafanye kazi vizuri. Unaona Waziri anahangaika, anapambana lakini kwa nini watu wanamvuta na kumrudisha nyuma? Boresheni mifumo ya makusanyo ili tuweze kuona namna gani tunapambana na hawa watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine ambalo nataka kulisemea. Mimi naishauri Serikali tuje na utaratibu wa ajira ambazo zitakuwa ni za muda maalum. Ili, mtu apimwe uwezo wake, apimwe uaminifu wake, lakini pia apimwe namna gani anaweza kuwa mbunifu. Siyo mtu anakaa tu anaendelea kula lakini hakuna anavyopimwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiweka ajira za muda maalum kila mmoja atakuwa anapambana ili aweze kufanya vizuri aendelee. Lakini kwa sababu wanajua nimekwishaingia nimeingia bwana, hapa nani wa kunitoa? Ataiba na atafanya anachotaka kwa sababu hakuna kinachoendelea. Kwa hiyo niombe sana Serikali iliangalie hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, inawezekana hawa watu wanaiba kwa sababu sheria zetu ni dhaifu. Kazi ya Bunge ni kutunga sheria. Leteni hizi sheria za mtu anaiba, ameiba bilioni tano wanasema eti akalipe faini milioni moja. Hizo ni sheria gani? Leteni Sheria hapa tuzifumue, ili tuanzishe Sheria ambazo zitawabana ili wanyooke. Haiwezekani tunalea vibaka kwa sheria ambazo inawezekana hazina uwezo. Sasa, kazi kwenu Serikali tuleteeni. Kama mna nia ya dhati ya kumsaidia Mheshimiwa Rais, leteni hizo sheria tuzibadilishe ili watu wanyooke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vitu ambavyo kwa kweli vinauma na vinaumiza sna. Hata hivyo, mimi ninaamini wako watu wazuri, wako Mawaziri wazuri. Tukiwa na sheria nzuri mnaweza mkasimamia haya mambo yasifanyike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala la kuhamisha hamisha watu hovyo. Hapa tukimuuliza kila Mheshimiwa Mbunge kama ana Mkurugenzi au Mhasibu (DT) aliyehama kwake utakuta mwingine amehama kwa sababu hapa aliharibu, anapelekwa sehemu nyingine. Mtu akishafanya makosa aondoke moja kwa moja asiendelee kuchafua eneo lingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nakushukuru na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Innocent, ahsante sana. Mheshimiwa Phillipo Mulugo, atafuatiwa na Mheshimiwa Mhandisi Stella Manyanya, Mheshimiwa Seif Gulamali ajiandae.

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa unyenyekevu mkubwa, kwa dini yangu ya Kikristo naomba niamini kwamba nitakachokizungumza hapa ni kile kinachotoka ndani ya moyo wangu kwa imani niliyonayo mimi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najiamini, mimi ni mtu mwaminifu na mkweli. Pia, huwa siwezi kubabaika na uongo uongo, najiamini. Hata ukinifanyia *vetting* mimi ndivyo nilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kusema, kwamba, mimi nimekuwa Mbunge awamu hii ni ya tatu. Bunge la

Mama Makinda, Bunge la Mheshimiwa Ndugai na sasa Bunge la Dada yangu Dkt. Tulia. Kwa hiyo nina ka- *experience* kidogo, na nimekuwa kiongozi kwenye Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mandhari (mazingira) haya ninayoyaona kwa taarifa ya mwaka huu ya *CAG*, sijui nianzie wapi lakini hatujawahi kufikia hapa. tumekwishawahi kufikia hapa kwenye Bunge la Mama Makinda, tulitoka saa sita hapa. Wabunge mliokuwepo enzi hizo akina Mama Kilango mtanisaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulibishana humu ndani tukamaliza saa sita. Mheshimiwa Kigwangala ulikuwepo. Leo, watu tunachukulia hizi taarifa kirahisi rahisi. Ndiyo maana nasema moyo wangu unavuja damu. Nimekuwa nikiangalia mjadala huu toka jana na leo. Ndiyo maana asubuhi moyo uliniuma sana nilipoona Wabunge wanachangia mjadala huu kwa hisia kali sana, halafu Waheshimiwa Wabunge wenzetu waliopewa dhamana na Serikali kusimamia haya tunayoyasema wana-*chat* kwenye simu, wanaongea na simu na wanazunguka zunguka. Niliumia sana. Hata ukiangalia sasa hivi ndiyo mnaniangalia ninavyoongea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wakati Waheshimiwa Wabunge wengine walikuwa wanaongea hapa, watu wanaongea kama vile hakuna jambo kubwa kitaifa. Yaani unaweza ukaangalia pale, nilikuwa namuona Kaka yangu Mheshimiwa Waziri Mkuu, angalau anaangalia, Mheshimiwa Profesa Mkenda anaangalia pamoja na Waziri wa Ujenzi. Wengine tuna-*chat*, tunaongea ongea tu. Haiwezekani. Ninyi ndio mmepewa dhamana ya kusimamia haya. Taarifa ya CAG Mheshimiwa Rais amesomewa Mwezi wa tatu, leo ni miezi sita mmefanya nini kwenye ofisi zenu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ni kweli katika *instrument* ya Waziri uko pale pale Wizarani, hakuna namna ya kuwajibishana pale katikati? Hakuna *management team* mnaweza mkakaa mkasema hili limesomwa kwa Mheshimiwa Rais kutoka kwa CAG, mhusika ni fulani na fulani angalau mmfanyie uchunguzi wa ndani? Jamani haiwezekani, tumefikia hapa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu jana na leo kila Mbunge akisimama anaongelea hayo hayo. Sasa tufanyeje? Tunamsahuri Mheshimiwa Rais avunje Baraza la Mawaziri kuanzia kesho. Huo ndio ushauri wangu kwa sababu moyo unauma sana. Si kama naona wivu na mimi nilikuwa huko. Siyo kwamba nataka kurudi. Hapana. Lakini tulipofikia ni pabaya. Nchi inakufa sasa twende wapi? Pia, na nyie mnaotakiwa kuwawajibisha watu hamtaki kuwawajibisha. Wanafanya kazi Mawaziri wawili. Unamuona tu Mheshimiwa Mchengerwa anachukua hatua na nini. Sasa wengine mnafanya nini? Jamani hakuna kabisa? Yaani hela zinaliwa hivi hivi halafu mnakwenda kukamata wenye kesi za ng'ombe na kuku mitaani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mawaziri mnakuja hapa mnajibu maswali kwamba, huko atakayefanya hivi atachukuliwa hatua; mbona ninyi mmeshindwa kuchukua hatua? Mbona *CAG* amekwenda maabara amepima malaria, kwamba hii hapa ni malaria sasa tukupatie dawa, halafu hamtaki kuchukua hatua, hamtaki kumuonesha dawa, sasa sisi tufanyeje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tufanyeje? Umekwishapimwa, unaumwa Malaria, unaumwa *typhoid*, unaumwa Kisukari ni kutibiwa. Sasa tunatibiwaje. Yaani tuyatoe wapi mashirika haya ya umma yalioharibu hali hii kama siyo Mawaziri husika ndiyo mmfanye?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaheshimu sana hawa Waheshimiwa Wabunge, msitusonye kwa sababu sisi tuko huku mbele. Ni utaratibu tu kesho na ninyi mnakuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hii inayoelezwa kwamba ndiyo ambayo imekithiri kwa matumizi mabaya ya fedha

zinazozungumzwa, ndiyo Serikali iliyofanya kazi kuliko Serikali nyingine zilizopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kama kuna Mbunge atashindwa kurudi, atashindwa kurudi kwa sababu zake yeye; lakini kwa miradi iliyofanyika kwenye majimbo yetu haijawahi kutokea. Taarifa ya kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya pili; kesi ambazo zimefunguliwa kwenye Serikali hii …

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ni moja asinipotezee muda. Taarifa ni moja.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa yangu ni moja. Naomba nitoe taarifa sasa. Ni kwamba, kesi ambazo zimefunguliwa na Serikali hii kutokana na watu ambao ni wabadhilifu, wezi, walaji fedha ambao tunawazungumzia hapa, kuanzia mwaka 2021 mpaka mwezi Juni, 2023 ni kesi 1,790. Katika kesi hizo… *(Makofi)*

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** … kesi 965 zote Serikali imeshinda na watu wamechukuliwa hatua…

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, malizia.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** … kwa hiyo, isielezwe hapa kwamba Serikali ya Awamu ya Sita hakuna ilichokifanya na ndiyo Serikali ya watu wezi…

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** … hapana

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** … utagundua kwamba, kulikuwa na sasa hivi hali imebadilika. *(Makofi)*

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Mulugo, endelea na mchango wako umalizie.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba, naomba sana; tusijifanye hapa ni mabingwa hapa wa kuelezea vitu ambavyo kama vile sisi hatujui. Jambo hili liko wazi. Ukianza kusema kwamba Serikali hii imeleta nini na nini, nani asiyejua kwamba miradi inakwenda vizuri? Sasa, kama hela zimeibiwa si zipo ndiyo maana tunasema zimeibiwa tu. Sasa hatuwezi kuingia kwenye chaka la kwamba Serikali imeibiwa hela eti kwa sababu hela zinakuja kwenye halmashauri. Sasa zingekuja nyingi zaidi ndiyo tungefurahi zaidi lakini hizo zimeibiwa lazima tuziseme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa kaka yangu Simabachawene, ni Waziri wa muda mrefu nakuheshimu sana; tena ni Waziri wa Utumishi na ni Mwanasheria. Nisingependa wewe ujiingize katika jambo hili wakati liko wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hivi, CAG ndiyo Mkaguzi wa fedha za umma…

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo.

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *CAG* amekagua akatoa ripoti, imesomwa mbele ya Mheshimiwa Rais na Rais akachukizwa sana na jambo hilo. Sasa, leo limekuja kwetu tunajadili halafu mnatetea. Mnatetea nini? Kama ni hatua si mngechukua huko huko yasingekuja hapa? Naomba tuwe huru tujadili jambo hili ni kubwa na ni kubwa mno.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mulugo, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Tabasamu.

**TAARIFA**

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumza hapa mapema, kwamba Bunge hili sasa hivi limegeuka kuwa Bunge la Dunia. Tunaonwa na Dunia nzima. Muda wa kutoa maelezo Mawaziri wanao kesho. Wawaachie Wabunge waongee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba hivi tunavyozungumza, taarifa za wizi zimeletwa na *CAG* siyo sisi Wabunge; na alikabidhiwa Mheshimiwa Rais na tunajua jinsi Mheshimiwa Rais anavyozitafuta hizi fedha kwa shida. Sasa, zinapoibiwa na sisi hapa tunakuja kumsaidia Mheshimiwa Rais, tunajua kabisa kwamba ameleta fedha nyingi kwenye nchi hii. Hizo hela zinaibiwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mulugo, unaipokea taarifa hii?

**MHE PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea kwa mikono miwili na miguu miwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni kwamba, naunga mkono azimio la Kamati. Hata hivyo, kabla sijaunga mkono

ninachotaka kusema ni kwamba, hebu Waheshimiwa Wabunge jambo hili, tukitaka kuweka historia ya Bunge hili ni hapa. hatuoni wivu kwa Mawaziri, mimi nilishawahi kuwa Naibu Waziri, sioni wivu. Hata mkinirudisha kesho naweza na ninaweza kufanya kazi nzuri kuliko hiyo. Mimi najiamini mno. Ninajiamini kwa sababu ni kuchukua hatua na hakuna kingine. Leo mambo yanakwenda hovyo hovyo na holela holela katika namna hii, haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nimesema tangu mara ya kwanza, kwa nini Serikali haitaki kuwawajibisha watu wanaoiba hela? Sisi tukimbilie wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale wananchi hawana nguvu ya kuja hapa Bungeni kuongea. Wametuchagua sisi tuje tuongee haya. Vile vile, huko hali ni mbaya jamani. Hebu naombeni tuchukue hatua. Mungu asimamie hii nchi jamani…

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE–SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Philip, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Ole-sendeka.

**TAARIFA**

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE–SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi nimpe taarifa rafiki yangu. Hayati, Edward Sokoine, aliwahi kusema "*umefika wakati wananchi wanashindwa kutofautisha kati ya viongozi wa chama na viongozi wa Serikali kwa upande mmoja na walanguzi*", mwisho wa kunuku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Rais alifika mahali akatumia lugha ya kusema *stupid* kuonesha hasira dhidi ya mafisai. Wanaomwakilisha Mheshimiwa Rais hapa, wanaowakilisha Serikali hapa ni Mawaziri. CCM inasema kukiri mapungufu siyo dalili ya kushindwa bali ni ishara ya kujiimarisha. Walio wadogo zenu wamefanya uhalifu si ninyi, kwa nini hamtaki kujipambanua kwa

kusimama kusema, mimi ninawatuhumiwa hawa na ninakusudia kuchukua hatua kesho kutwa ili mambo haya yakome na yasirudie? Kwa nini mnapiga dana dana hapa? Tamkeni kauli ya kushughulika na mafisadi tutakuwa pamoja. Hamtamki, sisi tulikula kiapo. Cheo ni dhamana sitatumia cheo changu au cha mtu mwingine kwa faida yangu. Rushwa ni adui wa haki, sitapoke a wala kutoa rushwa. Pia, ninyi mmekula hivyo hivyo. Ninyi si sehemu lakini mkinyamaza watu watashindwa kuwatofautisha. Wataona na ninyi ni wabia. Kitakachobaki kutokujulikana ni kiasi cha…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ole-sendeka ahsante. Mheshimiwa Mulugo, taarifa hiyo unaipokea?

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, hakuna taarifa juu ya taarifa.

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya Mheshimiwa Ole-Sendeka, ninaipokea kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa naomba umalizie muda wako umekwisha.

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeongea dakika sita tu.

**MWENYEKITI:** Naomba umalizie, muda wako umekwisha.

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** …huko kote walikuwa ni wengine. Mimi bado sijaongea *point* zangu.

**MWENYEKITI:** Naomba umalizie. muda wako ambao umewekwa umekwisha.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Naona muda umekwisha.

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshindwa kuongea. Nimeghadhibika.

**MWENYEKITI:** Pole. Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Mhandisi Stella Manyanya, atafuatiwa na Mheshimiwa Seif Gulamali, Mheshimiwa Esther Malleko ajiandae.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa siku hii ya leo. Pia, nichukue nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu ambao wamekwishachangia katika hoja hizi muhimu ambazo zimewasilishwa na Kamati zetu tatu. Ninawapongeza kwa kweli Wenyeviti wa Kamati hizi kwa kazi kubwa waliyofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwenye Bunge hili ni kati ya wale ma-*senior* kidogo, hiki ni kipindi changu cha nne tangu Bunge la Tisa. Tumekuwa tukishuhudia taarifa hizi zikijitokeza hapa na pale lakini wakati mwingine taarifa za ubadhilifu zimekuwa zikijitokeza kupitia hata kwa watoa habari *(whistle blowers)* na zimekuwa zikifanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kitu ambacho nimekiona, kwanza ile dhamira ya kuchukia ule ubadhilifu au rushwa, je, ipo kweli ndani yetu sote? Hilo swali najiuliza kila siku, na bado naendelea kulitafakari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, najaribu kuangalia hata kwa upande wa sheria zetu, wanasheria wetu. Kwa sababu Bunge kwa mamlaka yetu tumeambiwa kutunga sheria. Hata hivyo, katika kutunga sheria zinaletwa baada ya kufanyiwa kazi na Serikali ndiyo tunaletewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao wajibu na nafasi kwa yeyote ambaye anaona kwamba kuna jambo, anaweza akaleta Muswada wake; lakini hili ni nadra kutokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nafikiria katika hayo mapungufu ambayo tunaona ni ya kisheria, katika kuchukua

hatua, Bunge hili liliopewa mamlaka ya Kikatiba na humu kuna watu wenye uwezo wa aina mbalimbali ukiacha ile kwamba mtu yeyote anaweza kuchaguliwa kuwa Mbunge, lakini tunao wataalam kwenye Bunge hili. Kwa nini tusiunde chombo maalum cha kulisaidia Bunge ndani yetu sisi wenyewe ukiacha Kamati ambazo kila mmoja lazima aingie kwenye Kamati, ili kuweza kutafakari kwa kina na ikiwezekana kuangalia *whether* hili jukumu tulilopewa la kusimamia, maana yake sisi tumeambiwa kazi yetu sisi kusimamia na kutetea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuangalie katika kuisimamia Serikali, tunasimamia, lakini unatosha usimamizi wa aina hii au usimamizi huu unatakiwa kuwekwa katika sura tofauti kidogo? Maana yake ni miaka mingi toka Katiba yetu hii ipo, inasema sisi tunasimamia, lakini mwisho wa yote tunasimamia tunasema humu, tunasema humu na wakati mwingine hata hizo hatua zimekuwa zikichuliwa lakini unakuta baadaye tena watu wanakwenda Mahakamani yuleyule aliyekushauri kwamba chukueni hatua hii, yuleyule anasimama tena upande wa pili anasema chukueni hatua hii, matokeo yake tunalipa mabilioni ya hela. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa naona bado hatujapata njia sahihi ya kushughulikia mambo yetu yanapokuwa mazito kama haya. Ni wakati umefika kuitafakari vizuri Katiba yetu juu ya majukumu yetu katika hii Mihimili yote mitatu ilivyo, lakini vilevile kuangalia hata Vyombo tulivyoviunda vinatusaidia kwa kiasi gani. Kumekuwa na hii Mahakama ya Kiufisadi, pengine na mambo yanayojadiliwa humu yangekuwa yanapelekwa kule *automatic,* halafu mtu akajitoe mwenyewe kule kupitia hiyo Mahakama ya Kifisadi. Sasa kwa hali hii iliyopo mimi naona kwamba tunatumia nguvu kubwa sana kulalamika, kulaumu, kusema kwamba hatuko sawa, kujiapiza lakini mwisho wa yote tunatoka kama tulivyoingia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naongea haya kwa uchungu kwa sababu nimehusika na Kamati za Richmond, hizo za akina *Dowans* nyingine zimepita humo katikati za watu wengine, lakini mwisho wa yote unakuja kukuta kwamba fedha zinalipwa tena kwa watu walewale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, toka nimekuwa *senior* zaidi kidogo Mkuu wa Mkoa, Naibu Waziri na huku nimekuwa sipendi kuzungumza sana, nimekuwa napenda kusikiliza zaidi na kushauri kwa upole lakini katika hili nasema kwamba bado hatujawa na tiba sahihi katika kushughulikia mambo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata Taarifa ya *CAG* yenyewe ukiiangalia, wakati mwingine inakuwa *too mechanical. Analysis* yake haiendi kwa kina. Kwa mfano nichukue mfano mdogo tu ukisema leo *Force Account* haijafanya kazi kubwa, bado huitendei haki jamii ya Watanzania. Binafsi, kwa sababu *Force Account* ukifuatilia ni kama mwendelezo wa zile jitihada walizokuwa wanafanya wananchi kujenga madarasa yao wenyewe. Miaka nenda rudi wamekuwa wakijenga madarasa yao wenyewe, toka tuliposema kwamba kila kijiji kiwena shule kila kata iwe na sekondari, wananchi wamekuwa wakijitolea wakijenga madarasa hayohayo walikuwa wanajenga bila huo ujuzi, siku hizi tumeongezeka ujuzi kidogo, utaalam zaidi kidogo na ndio maana tumefanikiwa kujenga haya madarasa mengi kupitia hizi fedha alizotoa Rais Mama Samia.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninachozungumza ni nini? Kinachotakiwa sisi siyo kuichukia *Force Account* badala yake kuweka…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Stella kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha Ulenge.

**TAARIFA**

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi ya kutoa taarifa kwa *Senior, Engineer* Dada yangu Mheshimiwa Stella Manyanya. Tunapozunguma suala la *Force Account* hatusemi kwamba haifai kabisa isipokuwa ni miradi ya aina gani, ya ukubwa gani ndio kinachozungumzwa hapa. Huwezi kupeleka huko chini kwa mtu ambaye hana taaluma ukiwa wewe ni Mwanataaluma *Electrical*

*Engineer* mradi wa bilioni tano, unafanywa na *local* fundi huku ni kukiuka hata Sheria yenyewe ya Manunuzi ya Umma. Hiyo ndio taarifa ambayo naomba kumpa Dada yangu *Engineer* Stella Manyanya, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya, hiyo taarifa unaipokea?

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana naipokea taarifa yake kwa misingi kwamba ni ujumbe ameuzungumza, lakini kama alivyosema mimi ni *Senior* na siyo *Senior* tu wa kuzungumza niliyefanya kazi za kiuhandisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosema ni nini? Tunapokuwa tumefanya kazi fulani, tumepitiia miradi fulani kama nchi ni vizuri kuangalia pia yale mazuri ili yatuwezeshe kwenda mbele vizuri zaidi. Ukiangalia *cob cycle* inakwambia leo umefanya unajitafsiri unajitafakari, unarekebisha, unaenda tena mbele. Kwa hiyo hatuwezi kuona kwamba mahali pakiwa na upungufu, kwa mfano sasa hivi kwenye Halmashauri zetu hakuna wahandisi kule, lakini hao wamejitahidi kusimamia kufika mpaka hapo tulipofikia utasemaje *Force Account* haikufaa kabisa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninachosema siyo kusema tu kwamba mradi wa bilioni kadhaa tuseme mradi wa kiasi fulani wenye kuhitaji ujuzi maalum. Unaweza ukawa ni mradi kwa mfano mwingine alisema isizidi milioni 200, madarasa yanafanana ya milioni 500 kwa nini wasijenge? Ambayo ujuzi wake unafanana tu wa kujenga madarasa. Kwa hiyo kuna vitu vya kuangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ukiacha hiyo niliyosisitiza sana kwamba kufanya uchunguzi na namna gani Bunge letu liweze kuchukua hizo hatua. Nikirudi katika kumuunga mkono Mheshimiwa kaka yangu Kirumbe kuna Halmashauri zinanyanyasika, zinahujumiwa, siyo kwa kukusudia, lakini bila kuzitafasiri. Nimesema kuna halmashauri ni za ki-*TASAF* yaani maskini kuliko hata zinavyoangaliwa. Kwa mfano Halmashauri yangu ya Nyasa imo katika Halmashauri zenye Hati ya Mashaka, lakini unakuta Watumishi wanaopelekwa ni kweli wale ambao

wanakuwa wameambiwa huko watoke wanapelekwa pale kama adhabu, watafanya kazi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninao mfano wa Mwalimu aliyetolewa Musoma amebakiza mwaka mmoja kustaafu anapelekwa Nyasa akaanze maisha kule upya maana yake ni nini? Kwa hiyo kuna mambo tunayafanya si ya haki, Halmashauri zile ni changa mapato yake ndio vyanzo unaanza kuviimarisha, kuviunda, lakini kuna Halmashauri zinapata fedha nyingi kutokana na mapato na zimewekezewa sana huko, utasikia miradi ya *SGR* utasikia miradi ya *flyover,* utasikia miradi, mikubwa, mikubwa yote inaenda kule ndio hayo Majiji makubwa yanakusanya mapato makubwa, halafu unataka yafanane na sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imefikia kiasi kwamba Diwani anapunguziwa posho yaani kikao kinajadili kupunguza posho halali ili Halmashauri iweze kulipa isipate Hati Chafu. Mkurugenzi anapunguziwa malipo yake kwa mfano ya *night* eti ili tusipate hati chafu, basi angalau tuwe tunalipana hivi. Yaani watu wanaishi kwa ilimradi waishi, ndio kama Halmashauri yangu ya Nyasa. Utalinganishaje mazingira kama hayo? Wataachaje saa nyingine ku-*swap* mahali ambapo wanaweza ku-*survive*? Kwa hiyo ninachoomba Bunge kama Bunge, tusiende kwa hamaki, naomba tuangalie kiundani na Serikali watusikilize na Mheshimiwa Rais amesema watusikilize halafu tuyafanyie kazi. Naomba sana kwenye kuchukua hatua tusiogope, japo ukichukua hatua mara nyingi wewe maisha yako yanakuwa hatarini, ndio maana watu hawachukui hatua. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa hatuwaungi mkono wanaochukua hatua, tunawaona ni wabaya, hiyo ndio changamoto kubwa ya nchi yetu, watu wanaoiba ndio wanasifiwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa muda wako umeisha, malizia.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Seif Gulamali atafuatiwa na Mheshimiwa Esther Malleko na Mheshimiwa Mohamed Issa, ajiandae

**MHE. SEIF KHAMIS S. GULAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi leo ili niweze kuchangia kwenye hii ripoti ambayo imeletwa na Kamati, kwanza tunaipokea na kuiunga mkono. La pili, toka jana tumeanza mijadala juu ya hii ripoti. Wachangiaji wengi wamesikitishwa na imekuwa kawaida tunasikitika kila inapokuja ripoti hii na siyo mara moja tu mwaka jana tumesikitika, mwaka juzi tumesikitika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo taarifa mpaka tunafikia hatua tunasema kuna wizi kwa sababu *CAG* ni jicho la Bunge na jicho la Serikali katika kuangalia sehemu ambako kuna uvujaji wa fedha za Serikali na inatuonyesha kwamba hapa zimeibiwa kadhaa kama ambavyo tumeona kwamba kwenye *POS* kuna upotevu wa zaidi ya bilioni 11, lakini kuna sehemu zingine wamesema hawakukusanya Halmashauri bilioni 37, yaani mwaka 2021/2022 bilioni 37 hazikukusanywa, mwaka wa nyuma yake mwaka 2020/2021 bilioni 14, ni uzembe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaonyeshwa na *CAG*, lakini tunakuja kuonyeshwa hapa kwamba Serikali imepata hasara kupitia *TANOIL* tumepata hasara ya bilioni 7.0. Hizi zote tunaonyeshwa na *CAG*. Halafu anatokea mtu mwingine anasema, hapana hatujaibiwa, tuko salama, sasa tunajiuliza hiki chombo cha *CAG* kipo kihalali au hakipo kihalali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kipo kihalali kinatuambia kuna wizi vipi tunatokea tunasema hakuna wizi, maana yake tunapingana wenyewe kwa wenyewe na kama tunaona Taarifa ya *CAG* si sahihi, basi tukifute, tuiondoe hii *CAG*, kwa nini kila mwaka inatuletea taarifa za wizi humu ndani na tunatoa maelekezo hatua zichukuliwe na hatua hazichukuliwi. Halafu mwaka unaofuata tunaletewa tena ripoti, Wabunge wanasikitika

na wengine wanalia, wengine wanatoa na machozi *as if* kwamba ni ripoti mpya kwamba haikuja mwaka jana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme, tumeona huko kwenye Mahakama wamejaa wezi wa kuku, wezi wa mbuzi, wamegombana huko mtu na mke wake ndio zimejaa, lakini kesi za majizi yanayoiba fedha za Serikali huyaoni huko. Sasa tunaelekea wapi? Hili si suala la kuvumilia, lazima tuchukue hatua, mwizi wa kuku anafungwa miezi mitatu au miezi sita, lakini mwizi wa mabilioni ya hela anahamishwa, anapewa tena sehemu nyingine akaendelee kula keki ya nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu utaratibu ifike hatua hebu tuziangalie Sheria zetu za Utumishi, Sheria za Utumishi wa Umma yawezekana zinawalinda sana Watumishi ili waendelee kula fedha za nchi hii. Hili haliko sawa na watu wanasikitika na ndio maana wakati mwingine unakuta wananchi wa kawaida wanasema tumeshawazoea, mnafanya maigizo Bungeni, mnazungumza tu mnaibiwa, mnaibiwa lakini hatuwaoni hao wezi wakipelekwa kwenye hizo Mahakama. Tulifikia hatua tukasema tuwe na Mahakama za Mafisadi, lakini mbona hatuoni hao Mafisadi wakipelekwa wenye hizo Mahakama?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ni kweli Mheshimiwa Rais mwezi Machi alisimama akilihutubia Taifa akisikitika juu ya wezi hawa, ndio tumeweza kuona kuna mabadiliko ya Baraza la Mawaziri, lakini je, huku chini kwa Wakurugenzi mnaweza mkabadilisha mnawahamisha, lakini mnahamisha wezi tu kwamba mnamtoa mwizi *point A* unampeleka mwizi pointi B ili akaendelee kuiba, hapo ndio umetatua tatizo? Hatujatatua tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tunaweza tukaona hata hawa Wakurugenzi hawali peke yao, katika Halmashauri unakuta yupo Mkurugenzi, yuko Mweka Hazina, yuko Afisa Mipango, yuko Afisa Manunuzi, yuko Afisa Biashara, hawa watu wote hawa wanatakiwa wachukuliwe hatua suala la kumchukulia hatua Mkurugenzi peke yake Mweka Hazina unamwacha kumbe yule Mweka Hazina uliomwacha ndiye mtaalam wa kuiba. Kwa hiyo

ukileta Mkurugenzi mwingine, anamuonyesha njia ya kuendelea kuiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukifanya hivyo, hatuwezi kutibu tatizo, ukiondoa Mkurugenzi tumwondoe Mkurugenzi, tumwondoe Mweka Hazina, tumwondoe Afisa Mipango ili tupeleke timu mpya zikafanye kazi. Zamani tulikuwa na uhaba wa Watumishi, wasomi, leo tunao wasomi wengi, vijana wako wengi wenye uchungu wa kulitumikia Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwaingize vijana wafanye kazi, isiwe lazima tuwabadilishe, tuwabadilishe tulikuwa tunawabadilisha kwa sababu tulikuwa na uhaba wa Watumishi wa Umma leo idadi ya Watumishi wa Umma wasomi kwenye Taifa hili wako wengi na hawana kazi, tunasema wacha mtu afanye kazi mpaka azeeke, mpaka astaafu, nini tunalindana, tunalindana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hili suala la kulindana…

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gulamali kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Sagini.

**TAARIFA**

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda pia naomba ku-*declare* kwamba nimewahi kuwa Mtumishi wa Umma ngazi ya chini mpaka ngazi ya Mtendaji Mkuu. Nataka niseme kwamba hii *generalization* kwamba Watumishi wa Umma wanaofanya matendo yasiyofaa kama wizi udokozi na kadhalika wanalindwa kwa ujumla wake, haiwezi kuwa ya ukweli kabisa. Nikichukulia mfano kwenye Wizara yetu ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kwenye Mfuko wa Kufa na Kuzikana, Watumishi 18 hivi sasa wako Mahakamani, Watumishi 16 walifukuzwa kazi, Watumishi nane walisimamishwa kazi na

Watumishi wawili waliotoroka wanatafutwa na Jeshi la Polisi. Kwa hiyo kwa ujumla kwamba wanalindwa, si sahihi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Gulamali taarifa hiyo inaipokea?

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wale Matrafiki wanaochukua rushwa huko na wale waliotajwa kwenye ripoti? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nenda kwenye Halmashauri ambazo zimetajwa kwenye ripoti ya *CAG* kwenye Halmashauri zetu. Hii imetoka juzi tu, lakini bado na yenyewe kuna watu wengi tumesema tuna-*generalize* hii Taarifa ya *CAG* ndio jicho la Bunge…

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gulamali kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Condester Sichalwe

**TAARIFA**

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani sikudhamiria kutumia muda wa Mheshimiwa Gulamali, msemaji, lakini nataka nisome kanuni ndogo kwenye Kamati ya *PAC*, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali kama ilivyobainisha katika kifungu cha 13 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023, kuna vitu vitatu inaeleza, naruka viwili nasoma cha mwisho, "kutoa mapendekezo na ushauri kwa Wizara na Serikali na Mashirika ya Umma kuhusu matumizi mazuri ya fedha za umma ili kupunguza matumizi hayo mabaya".

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema nini? Tunawaheshimu sana Mawaziri wetu na tunawapenda, tume-*table* Taarifa zetu za Kamati, huu ni muda wa Wabunge

kuchangia kutoa maoni yao kwa ajili ya changamoto ambazo tumeziona kama ambavyo Mawaziri huwa wanapata nafasi ya kufafanua pale tunapochangia na hairuhusiwi sisi kuwaingilia wanapotoa ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, toka tumeanza jana Wabunge hawatulii kuchangia kutoa mawazo yao, kila wakati Serikali inaingilia kati, hawatakuwa na muda wao kuja kujibu hizo hoja? Tunawaheshimu na tunawaamini, tunaheshimu mawazo yao, tunaomba waandike chini watakuja kutoa ufafanuzi kuhusu mawazo ya Waheshimiwa Wabunge.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Condester, Mheshimiwa Gulamali malizia mchango wako.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimechangia mpaka sasa hivi dakika tano na nusu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine kwenye Taarifa ya *CAG* inasema kuna malipo ya bila risiti ya bilioni 10, malipo bila risiti. Sasa kama Serikali inasema ukinunua dai risiti, unawahamasisha wananchi wadai risiti, lakini Serikali hiyohiyo inalipa haidai risiti na inamkamata mwananchi ambaye anafanya malipo bila risiti, anatozwa faini milioni tatu, hii ambayo imelipa bilioni 10 bila risiti, faini yake ni shilingi ngapi? Faini yake ni shilingi ngapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa unaweza kuona kwamba, haya ni madhaifu ambayo yameonyeshwa kwenye Taarifa, sasa hii utasema kwamba Gulamali najisemea au tunafanya ku-*generalize,* haiwezekani Taarifa imeeleza madudu ni mengi, sasa kama madudu ni mengi yameelezwa humu ndani, tunaiomba Serikali inatoa fedha nyingi, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, ametafuta fedha nyingi, anatupa kwenye Majimbo yetu, lakini walaji ni kina nani? Tunapata sisi wananchi, lakini hawa hawa Watumishi nusu na wao wanajimegea. Mwisho wa siku miradi mingine inakamilika mizuri, miradi mingine inakamilika ikiwa chini ya kiwango na malipo mengine yanafanyika bila risiti. Sasa kama malipo yanafanyika bila kuna nini kinajificha nyuma yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yamejitokeza kwenye *POS,* tumesikia hapa *POS* kuna bilioni 11 zimepotea. Haya unataka kusema kwamba na yenyewe tuyatafutie ninii, kuna timu nzima ipo pale, kuna Mkurugenzi, Mwekea Hazina, kuna Afsia Mipango kuna Afisa Biashara. Hawa watu wanahusika na masuala mazima ya makusanyo ya fedha katika Halmashauri. Tuombe hili jambo la hizi Halmashauri kwa kweli unakuta hata zile fedha za miradi ya maendeleo tunazielekeza Halmashauri asilimia 40 zitoke, bado hata zile asilimia 40 na zenyewe wanazila. Sasa tunataka tufanye nini? Hizo fedha zinatoka kutokana na mapato yanayokusanywa kwenye Halmashauri husika siyo kwamba zinasomwa zitakuja, hapana, unazokusanya katika kumi, 40 warudishie, hiyo wewe unazokusanya 10, 40 hupeleki, unakula zote. Hapa hatuwezi kufika lazima Serikali iangalie na Bunge lijalo katika maazimio, hizo Halmashauri siyo tu waishie Mkurugenzi kuhamishwa au kuchukuliwa hatua na safu nzima na mnyororo wake hii itaweka nidhamu kwenye Utumishi wa Umma na utendaji wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Gulamali. Mheshimiwa Esther Malleko atafuatiwa na Mheshimiwa Mohamed Issa na Mheshimiwa Joseph Tadayo ajiandae.

**MHE. ESTHER E. MALLEKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia kwenye hoja hii muhimu sana ya *CAG*. Nimepitia taarifa zote tatu kwa umakini mkubwa na nimezisoma vizuri, lakini kutokana na muda nitachangia kwenye taarifa mbili za Kamati nikianza na taarifa ya *LAAC* na baadae taarifa ya *PAC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaanza kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wangu mpendwa Mama Samia Suluhu Hassan, ninayasema haya kwa moyo wa dhati kwa namna ambavyo Mama yetu ameweza kufanya kazi kubwa, tunaona miradi mikubwa inayofanyika huko katika Majimbo yetu na Mikoa yetu. Nitakuwa ni mnafiki kama nisipomsifia Rais wangu, Mama Samia Suluhu Hassan, Mama yetu huyu halali usiku, mchana anahangaika ni namna gani anaweza kuleta maendeleo kwa Watanzania. Kwa hiyo, sisi tusipopongeza kwa namna ambavyo

anajituma na kwa namna ambavyo anaitetea Tanzania tutakuwa ni wanafiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaanza kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya, miradi mikubwa inatekelezeka, tunaona barabara zinajengwa, tunaona hospitali zinajengwa, tunaona vituo vya afya vinajengwa, tunaona shule za mifano zinajengwa, ni lazima tumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naenda moja kwa moja wakati Mama yetu akipokea taarifa ya *CAG*, mwezi ule wa Tatu Ikulu - Dar es Salaam. Ninanukuu maneno aliyoyasema Rais wetu mpendwa. Mheshimiwa Rais alisema: *"Watendaji wa Serikali wasimamie vema rasilimali za Nchi kwa kutumia mifumo na kuweka nidhamu kinyume na kufanya hivyo tutaenda kuiua Nchi yetu, tena tukakwenda kuiua wenyewe." (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge kazi yetu ni kumsadia Mheshimiwa Rais na Chama chetu cha Mapinduzi ili kiweze kutekeleza Ilani, kwa sababu sisi ndiyo wenye mkataba na wananchi huko. Ninashukuru sana Mama yangu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu kwa kazi anayoifanya lakini pia tunaona ni namna gani wameanza kuchukua hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na Mheshimiwa Waziri Mkuu, tumeona akipita kwenye Halmashauri huko akichukua hatua kwa wale ambao wamebainika wakiwa ni wabadhirifu. Haikuishia hapo, ninampongeza Kaka yangu Mheshimiwa Mchengerwa umeona ni namna gani ameanza kushughulikia watu hawa wanaomkwamisha Mheshimiwa Rais. Kwa kuona Mama yetu anakusudi la kuitetea nchi yake na kuleta maendeleo tunaona mfano wa bandari, ilikuwa haifanyi vizuri ameibinafsisha na leo tunaona kazi inaenda kufanyika tofauti na ilivyokuwa zamani. Hayo ni maendeleo tunapaswa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika taarifa ya *CAG* na Kamati ya *LAAC* waliona baadhi ya changamoto na mapungufu yaliyotokea ambayo yalisababisha Halmashauri kupata hasara.

Nikianza na ukiukwaji wa Ununuzi wa Umma Sura Na. 410. Kutokana na mapungufu hayo Serikali ilipata hasara ya shilingi bilioni 106. Mama yetu halali anatafuta hizi fedha lakini tunaona kuna namna ambavyo kuna watendaji wanashindwa kuzisimama na Mheshimiwa Rais amewaamini akawapa nafasi hizo ili waweze kumsaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na watu ambao wanamsaidia Mama Samia Suluhu Hassan, wapo walioajiriwa, wapo waliochaguliwa, wapo walioteuliwa, hawa wote ni jicho la Mheshimiwa Rais kumsaidia ili aweze kutimiza malengo yake kama Rais wa Tanzania. Tukianza kabisa chini kabisa kwenye *WDC*, kule kwenye Kata. Tukianza kufanyakazi kuanzia kule chini ninaamini tutakapokuja tena hapa wakati mwingine hatutaanza kuja kukutana na hivi tunavyokutana navyo leo. Nasema hivyo kwa sababu gani? Kule chini kwenye *WDC* wale wanakuwa na taarifa ya kushughulikia kama kuna mradi au kuna kazi inayofanyika kule kwenye vijiji. Kwa hiyo, kwenye Kamati ile anaingia Diwani, kwenye Kamati wanaingia Wenyeviti wa Vijiji, Wenyeviti wa Vitongoji na Wenyeviti wa Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale wanapaswa wanapoenda kusimamia ile miradi au kuikagua wawe na *BOQ,* lakini tatizo linaloonekana hapa wanaenda wakiwa hawana *BOQ*. Kwa hiyo hawajui wanaenda kukagua nini, wanaweza kuona shule imegengwa vizuri, wakashukuru na kusema imejengwa katika kiwango kinachopaswa lakini ukifuatilia *BOQ* na kile kilichofanyika ni vitu viwili tofauti. Kwa hiyo, tuanzie hapo ili tuweze kumsaidia Mama yetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukiukwaji huu wa manunuzi ya umma, unakuta Halmashauri imejipangia mkakati wake wa mwaka lakini hapo katikati Watendaji wanaenda kufanya manunuzi nje ya yale ambayo walikuwa wamejipangia. Kwa hiyo, unakuta mwisho wa siku ile Halmashauri haiwezi kufikia malengo yake. Ninasema hivyo kwa sababu gani? Taarifa hii ikianza kwenye *WDC*, taarifa hii ikatoka ikaenda kwa Katibu Tarafa ambaye Katibu Tarafa atapeleka taarifa kwa *DAS* lakini kuna Baraza la Madiwani ambalo linaongozwa na Mheshimiwa Mwenyekiti wa Halmashauri pamoja na Meya kwenye Majiji,

hawa watu wote wakiweza kuwasimamia hawa watu kuanzia kule chini kuna namna ambavyo tunaenda kupunguza huu wizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hapo tu kuna ma-*Internal Auditor*, hawa watu wanafanya kazi gani? Au taarifa wanazozitoa wao huwa hazitumiki? Kwa sababu huwezi kusema hawa wote wameaminiwa, wameajiriwa, wanalipwa mishahara lakini bado wanaendelea kumkwamisha Mheshimiwa Rais kwa nini? Kwa nini tunamkwamisha Mheshimiwa Rais? Lazima hawa watu wachukuliwe hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaishia hapo kuna Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya, kuna TAKUKURU, kuna Jeshi la Polisi, namshukuru sana Kaka yangu, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ameweza kusema kwa hatua zinazochukuliwa. Namshukuru sana Mheshimiwa Simbachawene amesema kwa hatua zinazochukuliwa. Sisi kama Wabunge tunataka kuona hawa watu ambao wanakiuka hii mikataba, hawa watu ambao wanakiuka ununuzi wa umma wanachukuliwa hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge hapa tunalalamika, tunalalamika kwa sababu hatuoni hawa watu wakiwa wanatoka hadharani Watanzania wawajue hawa ndiyo wezi. Kule Magereza kumejaa watu ambao wameiba kuku, wamegombana na wake zao, wamefanya nini hawa ndiyo waliojaa lakini kuna watu ambao wameliibia Taifa hili, kuna watu wanaomkwamisha Mama Samia Suluhu Hassan wanatembea huko barabarani wakihamishwa kutoka Halmashauri kwenda Halmashauri nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna nchi ambazo zinafikia hadi hatua ya kuwakata masikio au vidole wale wanaobainika kutumia hovyo au kufanya ubadhirifu kwenye hela za umma. Leo sisi tunamuona Mheshimiwa Rais anahangaika akitutafutia hela za maendeleo, kwa nini basi hizi hela kwa sababu kila mahali ukiangalia, huko kwenye *POS* zilivyozimwa ni shilingi bilioni 11. Hizi fedha zote mimi nimefanya mahesabu kwa hatua chache ni zaidi ya shilingi bilioni 500. Hizi hela haziwezi kwenda kutumika kwenye kumalizia hata Mradi wa *SGR*. Haziwezi kwenda kukamilisha vituo vya afya, kuna Bwawa la Mwalimu Nyerere. Kwa hiyo, sisi tuwe

hapa tukisaidia ni namna gani ya kumsaidia Mama yetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan aweze kwenda kutimiza maono yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye suala la uendeshaji usiofaa wa Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu. Katika Ripoti ya CAG ya mwaka 2021 ilionesha kwamba kulikuwa na ukiukwaji wa utolewaji wa hizo fedha na katika ukusanyaji walishindwa kukusanya kiasi cha shilingi bilioni 47.07 lakini leo 2020 tunatoka pale kwenye elfu 47…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ESTHER E. MALLEKO**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba dakika moja kukamilisha hoja yangu.

**MWENYEKITI:** Malizia Mheshimiwa.

**MHE. ESTHER E. MALLEKO**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Mheshimiwa Rais aliona anawasaidia akinamama, anawasaidia vijana na watu wenye ulemavu ili na wao waweze kujikwamua kiuchumi. Sasa tunapoona hivi vyote vinatendeka ina maana kuna namna tunamkwamisha Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo, mimi nashauri Bunge hili tuweze kutunga sheria ambazo zinaweza kuwadhibiti hawa watu lakini tusiache kupongeza Serikali kwa namna ambavyo imeanza kuwashughulikia hawa watu ambao wanakiuka au wanafanya ubadhirifu. Napongeza na kuunga mkono hoja zote za Kamati zote, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Ahsante sana Mheshimiwa Esther Malleko. Mheshimiwa Mohamed Issa, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Tadayo, Mheshimiwa Justin Nyamoga, ajiandae.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi walau nitie neno kidogo katika jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru sana kwa kunipa hii nafasi usingenipa hii nafasi maana yake ningekuwa sina

utetezi, leo ni siku ya tatu sijawasiliana na wake wangu na watoto wangu kwa kusoma hii taarifa, ningeshindwa kujitetea mimi kama usingenipa hii. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nilishindwa kuwasiliana nao? Nilikuwa nasoma hii taarifa ya CAG, nasoma nafika katikati, nasoma nafika karibia mwisho, nasoma nafikia robo, kila nikisoma naona ni wizi mtupu, nikisoma ni wizi mtupu, nikajiuliza hii taarifa ni taarifa ya *CAG* ya ukaguzi ama ni taarifa ya wizi? Hapa ndiyo nilishindwa kujua lakini kwa kweli mimi binafsi nasema hii ni taarifa ya wizi mtupu. Nakushukuru sana kwa kunipa hii nafasi.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema hivyo, mimi nimesoma kidogo tu mimi si Mjumbe wa *PIC*, wala si Mjumbe wa *PAC* si Mjumbe wa *LAAC* lakini naunga mkono maazimio yote yaliyoletwa na Kamati hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la kusikitisha sana kwa watendaji wetu wa Serikali, huu wizi unaofanyika ni wizi ambao unafanyika kule chini ambako huduma hizi za Halmashauri ndiyo zinatakiwa ziwafikie wananchi, sasa kama hawa watu tuliowaamini katika hii *layer* ya chini kabisa ya uongozi ndiyo wanatuibia, inakuaje leo sasa tutaendeshaje hii Serikali? Maana yake Serikali hii ndefu, kuna eneo la Rais, kuna Waziri Mkuu, kuna Makamu wa Rais, kuna Waziri mpaka unawafikia hawa Wakurugenzi umefika mbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii hali haiwezi kuvumilika, nimeangalia sehemu ndogo tu mimi kwa upande wa Halmashauri shilingi bilioni 1.68 hizi fedha zimetumika katika matumizi ambayo siyo sawa, maana yake ni nini? Watu wamejipongeza, wamefanya kipaimara, wamefanya sherehe zao binafsi, maana yake hayo matumizi hayajulikani, hayatambuliki, sasa hili tutaliacha hivi hivi kweli?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niguse hapa kwenye Mfumo wa *POS*, shilingi bilioni 11.07 zimesoma kwenye mifumo kwamba hizi fedha tayari zimefika lakini jambo la kusikitisha hizi fedha hazikupelekwa benki, kwa nini? Ziko wapi au ndiyo kuna *safe* pale Halmashauri ambapo zinaweza kukaa hata mwaka mmoja,

miaka miwili, mitatu. Hili jambo halivumiliki, zile mamlaka za kuchukua hatua tunaziomba sisi kama Bunge zichukue hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna fedha hapa za manunuzi ambazo bila kutumia mifumo shilingi bilioni 183, sasa hii ni Serikali au ni kikundi? Maana yake Serikali ina mfumo wake, nami naiamini Serikali yangu ina mifumo mizuri, imepanga utaratibu mzuri ina sheria nzuri. Mimi nashangaa vitu kama hivi vinafanyika, kwa kweli Bunge lichukue maazimio na maazimio haya kwa kweli yaje na utekelezaji, kabla ya utekelezaji wa maazimio haya tupate hasa *live* maazimio yale ambayo tuliyachukua kipindi kile, yamefanyiwa kazi vipi na yamefikia wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakuwa tunacheza *drama* tu humu, tunaonekana kama tunakuja kuchuka posho na mishahara, hawa wanaosema tunachukua posho na mishahara, kazi tunazozifanya ni kubwa ndiyo kama hizi, hatulali tunaishia mahospitali, leo tunakuta hawa watu tunakagua wizi tu, hili jambo halikubaliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niguse hapa Halmashauri inaiba basi hata hizi fedha ambazo tumewatengea hawa vijana, wanawake na wale wenye mahitaji maalum. Ukimuona hapo njiani unampa sadaka, leo tunawatengea fedha Mheshimiwa Rais amekubali pia wanaziiba, aah! jamani mmezidi hili jambo halikubaliki. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale kwetu Pemba tuna msemo unasema *"Ngoja ngoja huumiza matumbo,"* maana yake ni nini? Ukisubiri sana utalala na njaa! Watatuweka na njaa hawa watu, tuchukue hatua, hatua hizi mimi nashauri, Waheshimiwa Wabunge wenzangu wameshauri kunyongwa suala hili la kunyongwa sheria hii ipo, sheria hii ipo lakini hatujawahi kusikia…

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hatujawahi kusikia kwamba kuna…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mohamed kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Ndejembi.

**TAARIFA**

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kumpa taarifa mzungumzaji kwamba Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali na ndiyo maana mpaka hivi tunavyozungumza kuna watu wapo mahakamani kwa makosa ambayo ni ya ubadhirifu wa fedha, kuna watu wameachishwa kazi, kuna watu wametenguliwa teuzi zao kwa sababu ya ubadhirifu wa fedha za umma. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Issa taarifa hiyo unaipokea?

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza hii taarifa ni taarifa hovyo sana kwa sababu huyu ameshasimama mara tatu akisema hiyo hiyo, sasa ya nini tena kunipa taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipo tangu asubuhi hapa nasikiliza Bunge nay eye amesema mara tatu, ananipotezea muda, taarifa hii siichukui na muda wangu naomba ulindwe.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mohamed Issa, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Joseph Musukuma.

**TAARIFA**

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nami naungana na wenzangu kuwaomba Waheshimiwa Mawaziri waache tuzungumze.

Matatizo haya siyo ya Mawaziri ni ya kwetu wote mtupe muda na ninyi tutawapa muda, kama Mwenyekiti ameamua kutengua utaratibu hawatusikilizi utukubalie na sisi kesho wakati wana *wind-up* hapo akidanganya tuchemke nao. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Mohamed taarifa unaipokea.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea sana, naipokea sana ina afya hiyo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa nazungumzia suala la adhabu, hii adhabu ya kunyongwa ipo Waheshimiwa Wabunge, lakini wapo watu ambao wamehukumiwa kunyongwa mpaka sasa hivi wapo magerezani wengine wanakufa huko, ushauri wangu kwa hawa wezi, iletwe sheria hapa mwizi akiiba akatwe mkono, akishakatwa mkono asifukuzwe kazi, kuwe na utaratibu wa kurudisha zile fedha lakini wenzake wakimuona ana mkono kipande pale naamini hawataendelea.*(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni adhabu ambayo inafaa kabisa na wataonyeshana mfano. Iletwe sheria hapa ya kukata mkono wataonyeshana hawa lakini mwisho wa siku atashindwa kuwahudumia hata watoto wake, huo ni ushauri wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana Mbunge wa Sumve hapa Mheshimiwa Kasalali Emmanuel Mageni, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Elimu, Utamaduni, Sanaa na Michezo, lile jambo lilinigusa sana alipozungumzia *sports center*. Mimi nimefuatilia, na jambo hili likiharibika litakuja kwenye Kamati yetu, hatupendi tuwe tunakaa kwenye vikao kwa kujadili upotevu wa fedha ama uharibifu wa fedha. Nimefuatilia sana hili suala mpaka sasa hivi kweli kulikuwa na taarifa hizi za kubadilisha hii *center* kuipeleka kule Ilemela kuitoa Malya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Bunge limeshapitisha mpaka fedha kila kitu kimeshafanyika leo tunakwenda kubadilisha bila Kamati kujua, bila Bunge kujua fedha zimeshatoka hili suala siyo zuri. Kwa kuzuia hili naomba yale malengo tuliyojiwekea ijengwe *sports center* pale Malya bila

kuharibu utaratibu. Hili naliomba sana na Mheshimiwa Waziri wewe ni mpya kwenye Wizara hii pamoja na Naibu wako, nakuomba sana hili suala mlisimamie lisije likaharibika, hawa waliotaka kuharibu Mheshimiwa Rais ameshachukua hatua, kwa hiyo na ninyi msije mkachukuliwa hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea, niguse kidogo kwenye *KADCO,* jambo hili la *KADCO* linakuja mara kwa mara. Tunajua Profesa hapa anafanya kazi nzuri wala hatuwezi kusema anahusika na lolote lakini anaitetea sana na sisi Wabunge humu sote tunasema kwa nini isiende *TAA*? Kwa nini isiende huku? Kwa nini inabakia huku? Mara hii akija aje atupe mfano, hii ina ubora gani zaidi ibakie kuwa yenyewe kuliko viwanja vingine vyote viko kwenye mamlaka; hii tu ndiyo ibakie?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara hii imetumia fedha shilingi bilioni 2.36 pesa ya shilingi lakini pia dola milioni saba ambayo ni sawa sawa na shilingi bilioni 16.8. *CAG* alipouliza wanasema wameruhusiwa kutumia bila utaratibu. Sasa hii ndiyo vipi yaani? Hii siyo sawa. Ndugu yangu Mheshimiwa Profesa Mbarawa naomba hili jambo lisije likalipuka kwako. Hili jambo haraka sana lipeleke huku Waheshimiwa Wabunge wanakoshauri. Eeh, hili mimi ndiyo ushauri wangu.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilindie muda wangu maana yake nina mambo mengi hapa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mohamed kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Anatropia.

**TAARIFA**

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumpa taarifa mzungumzaji kwamba mara ya kwanza Afisa Masuuli alivyokuja kwenye Kamati tukamuuliza kwa nini *KADCO* haikabidhiwi kwa *TAA?* Alisema wanamakubaliano ya kiutendaji *(concession agreement);* alivyorudi juzi mkataba

umeshaisha lakini bado wanaendelea kufanya kazi tena bila mkataba. Kwa hiyo, hilo suala ni jipu na ni jipu na tunataka tujue wanalindwa kwa nini? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mohamed Issa taarifa unaipokea?

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea kwa sababu tunaweka msisitizo ili iondoke *KADCO*. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niguse kidogo suala la *TRA; TRA* wameguswa hapa na *CAG* magari 676 kutoka nje. Haya yamekwisha muda wake ambao wameuruhusu. Hawa *TRA* sijui tuwahesabu kwenye kundi gani? Kwa sababu sisi Wazanzibar tumeomba ruhusa kama hii hakuna mtu ambaye ameruhusiwa kuingiza gari hapa kwa ruhusa kama hii. Inaonekana hii kuna mfumo fulani wanajitengenezea wa wizi, au tuseme sisi Wazanzibari wanatuonea hawa? Kwa nini haturuhusiwi kuleta gari kwa muda mfupi? Watu ambao wanaruhusiwa; aidha awe tajiri tena aweke dhamana lakini mwisho hilo nataka wasituonee *TRA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *point* moja naomba.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa malizia.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nagusa kwenye *TANOIL. TANOIL* hapa mimi nilikuwa Mjumbe wa Kamati ya Nishati na Madini. Hii *TANOIL* imeguswa tu kama taasisi lakini hii Wizara nzima ya Nishati ilikuwa imeoza; imeoza kabisa. Namshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuifumua pale juu. Mheshimiwa Rais amefanya kazi nzuri na mkitaka kujua hii ilikuwa imeoza, wenzangu wamesema hapa, shilingi bilioni 120 walipewa mtaji, mpaka sasa hivi kuna mtaji wa shilingi bilioni 20.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana wameiba shilingi bilioni saba *point something.* Kabla ya kufumuliwa hii Wizara tulitaka kupata mgao wa umeme; uko wapi sasa hivi? Haupo, mafuta yalitaka kupotea; yamepotea? Kuna madudu kule yalifanyika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsantE sana.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ichukuliwe hatua hii Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo atafuatiwa na Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kupata nafasi hii ya kuchangia hoja hii muhimu. Dunia yote sasa hivi inaelekea iko kwenye mwelekeo wa kuwa na Serikali ambazo zinajiendesha kwa uwazi na kwa uwajibikaji wa hali ya juu; ndiyo mwelekeo wa dunia. Kwa hiyo, taarifa kama hii ambayo imekuja ni sehemu ya uwazi huo na uwajibikaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika hatua hii tunapaswa pia kwa kweli kumshukuru Mheshimiwa Rais pamoja na Serikali kwamba angalau ipo nia kwamba Serikali iende kwa uwazi na uwajibikaji. Kwa hiyo, imekuja mbele yetu sasa ni sisi sasa kuichangia na hatua zichukuliwe bila mashaka yoyote kwa sababu ndiyo utaratibu mzuri wa kuendesha Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaungana na wenzangu juu ya suala zima la kuondoa kabisa uvumilivu katika masuala ya uzembe, ubadhirifu na rushwa *(zero tolerance)*. Bila hiyo hakuna nchi duniani ambayo imeweza kuendelea iwe ni Afrika, *Asia,* Marekani au Ulaya kama hawana *zero tolerance* kwenye mambo haya ya uzembe uzembe, rushwa na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa hilo ni lazima tuendelee kuwa wazi kama tulivyo na hatua zichukuliwe kwa mujibu wa sheria tulizonazo kabla hata hatujafikiria kunyonga na kukata mikono, tuweze kwanza kutumia sheria zetu zilizoko kwa ajili ya kufanya mambo yaende sawa sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningetamani na mimi kuongea mambo mengi na kwa hisia kama wenzangu kwa sababu wako sahihi lakini mimi naomba nizungumzie kimsingi suala moja na kama muda utanitosha nitazungumzia lingine. Naomba nizungumzie suala la mradi mkubwa wa maji wa Same – Mwanga – Korogwe katika *context* ya ripoti ambayo imeletwa mbele yetu na wenzetu wa *PAC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ule mradi mimi ninatoka Mwanga ambako ndicho chanzo cha maji kinapoanzia na ndiyo tarajio letu kubwa katika miaka hii mitano ya uongozi wetu kwamba tuta-*deliver* maji kwa wananchi wa Mwanga. Mimi ninauita huu mradi mtihani wangu wa kwanza kwa sababu nilipotoka kuapishwa hapa Bungeni 2020 niliporudi tu Jimboni nikapigiwa simu kwamba kuna watu wanaandamana wanakuja ofisini kwako. Nikauliza wanafuata nini? Nikaambiwa ni wafanyakazi ambao wametelekezwa kule kwenye *site* ya mradi wanafuatilia maisha yao na *future* yao kwa ajili ya ule mradi kuwa umesimama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nikamuuliza yule kiongozi kwamba sasa katika mazingira hayo tunafanya nini? Akaniambia tuwafuate huko huko tusisubiri wakaja. Tukaenda pamoja na Mkuu wangu wa Wilaya na Kamati ya Ulinzi na Usalama. Tumefika pale tulikuta ile *site* imekuwa *abandoned,* mkandarasi alikuwa hayuko *site,* hakuna umeme, hakuna walinzi hakuna chochote. Nilimpigia simu Mheshimiwa Waziri Aweso na kwa kweli *experience* yangu ya kwanza ya Waziri anayefanya kazi vizuri niliipata pale kwa sababu kesho yake alifika *site.* Kwa hilo kwa kweli bado naendelea kumshukuru na ninamkumbuka sana kwa jinsi ambavyo ali-*act* kwa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, alipofika sasa ndiyo tukaanza sasa mchakato wa kufufua upya ile *site* ili iweze kwenda mbele. Mkandarasi wa kwanza alikuwa ameondoka *site* na sasa kwa sababu aliondoka *site* maana yake hiyo ni *repudiation* ya *contract* kwa hiyo ikabidi *termination* ifuate na mkandarasi wa pili siyo katika maana anayefuata ili walikuwa wanawakandarasi wawili kwenye *site,* yeye mkataba wake ukawa *terminated*

akaenda mahakamani na kesi iko mahakamani mapaka leo tunavyozungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tukaanza sasa mchakato wa kuweza kuifufua upya ile *site* na katika hili kwa kweli watu wengi sana walihusika. Wakuu wangu wa mikoa waliokaa kipindi chote hicho, Mkuu wa Wilaya, Kamati zote za Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuja mara nyingi sana kwa ajili ya kushughulikia ku-*restore* ile *site* ifanye kazi lakini kubwa zaidi Mheshimiwa Rais alihusika sana katika kuhakikisha kwamba ule mradi unaanza upya; kwa hiyo, kwa kweli kwenye hilo lazima tumshukuru sana Mheshimiwa Rais, ni mradi ambao nafikiri ana uchungu nao kwa sababu yeye mwenyewe aliweka jiwe la msingi tarehe 28 Novemba, 2018 akiwa Makamu wa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tukapambana ili kuweza kuanzisha upya kurudisha mkandarasi *site* ili mradi uweze kuendelea na katika kuwarudisha *site* wale wakandarasi ilifanyika *special audit* mwaka 2021 na katika kuwarudisha wakandarasi *site,* maelekezo ya *CAG* pamoja na Kamati husika za Bunge yalizingatiwa. Kwa hiyo, mwezi Mei mwaka huu sikumbuki tarehe ndiyo ukasainiwa Mkataba wa kuhuisha ule mradi *(reinstatement agreement)* ambayo ilizingatia maoni ya *CAG* katika *special audit* ambayo ilifanyika. Kwa hiyo, mradi umeanza tena upya mwezi Mei mwaka huu na ni Mkataba wa miezi 14 kwa hiyo, mwezi Mei, mwaka ujao tunategemea maji *tap* ile ifunguliwe ili tuweze kuanza kunywa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hali ilivyo *site* toka tarehe ile wakati tuna *reinstate* mradi mwezi Mei mwaka huu mradi ulikuwa 60% hivi tunavyozungumza mradi uko 83.57%; kwa hiyo, kazi inaendelea vizuri. Sasa kwa nini naelezea yote haya? Naelezea yote haya kwa sababu mradi ule kwetu sisi pale Mwanga, Same na Korogwe ni kila kitu. Yaani tungependa uendelee na usikabiliwe na jambo lolote ambalo litaufanya uingie kigugumizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sipingi kwamba Bunge lisifanye Azimio kama ilivyopendekezwa na Kamati lakini naomba tu tuzingatie mambo kama mawili; la kwanza sina hakika sheria inaweza ikawa inaruhusu kwamba ufanye *special audit,* umeanza

kutekeleza maelekezo ya *CAG* kwenye *special audit* mwezi Mei juzi umekwenda vizuri sasa hivi tuko 83% ufanye tena *special audit* nyingine juu yake. Inawezekana sheria ikaruhusu lakini busara katika maana ya *prudence* siyo *wisdom, prudence* nafikiri ingetaka kwamba ule mradi uendelee bila kusumbuliwa sasa hivi ili haya ambayo yalielekezwa kwenye *special audit* ya 2021 yaendelee kutekelezwa tuweze kukamilisha ule mradi kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Mwanga wanachokitegemea ni kwamba mwezi Mei mwaka ujao wafungue maji wanywe na eneo lile limekaa bila maji kwa muda mrefu sana. Kwa hiyo, kikubwa mimi ambacho ningeomba ni kwamba Azimio lizingatie yaani lije lakini kwa namna yoyote ile lisije likavuruga ile kasi ya mradi ambayo inaendelea sasa hivi na pia *of course* tuzingatie kwamba mkandarasi mmoja yuko mahakamani, sasa sina hakika kama hapo tena napo inakuwaje kama tunaazimia wakati kuna mtu bado yuko mahakamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine tungeomba sana kwamba Wizara ya Fedha waendelee kusukuma fedha kule kwa sababu mimi ni mradi ambao ninalala nao na kuamka nao na nikiwa Jimboni kila wiki nafika *site*. Nilizungumza *personal* na mkandarasi akasema fedha zikija kwa mtiririko zinazokuja sasa hivi, ana uwezo wa kumaliza ule mradi kabla hata ya wakati. Kwa hiyo, tunapoazimia mimi nilikuwa naomba tu kwa kweli tuzingatie hayo kwamba Wananchi wale wanategemea kwamba mwezi Mei wanywe maji tusije tena tukaingia katika mazingira ya kuendelea kuusitisha au kuuchelewesha ule mradi wakati ambapo sasa hivi ndiyo tuko mradi unatekeleza maelekezo ya *CAG* katika *special audit* ile iliyopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba pia ikiwezekana Kamati husika itembelee ule mradi ikiwezekana mara baada ya Bunge hili ili waone kazi jinsi ambavyo inaendelea pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, baada ya kusema hilo kama nimebakiwa na dakika chache ningependa pia nizungumzie suala la *force account.* Suala la *force account* siyo baya kama ambavyo baadhi ya Waheshimiwa Wabunge

wamezungumza na ninafahamu kwamba sheria imerekebishwa mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninachoshauri ni kwamba wakati wa kutengeneza kanuni, Mheshimiwa Waziri anayetengeneza kanuni azingatie ile *good practice* katika tasnia ya ujenzi. Haiwezekani mtu akachora yeye, akafanya *quantities* yeye, akajenga yeye mwenyewe, akajisimamia yeye mwenyewe na yeye mwenyewe akawa mteja. Ukifanya hivyo suala zima la *checks and balances* linaondoka, unaweza ukajenga mradi haraka lakini *quality* ile mradi wenyewe ukajikuta kwamba baada ya muda mfupi unaingia gharama nyingine kwa sababu unajenga mwenyewe, unajisimamia mwenyewe. Mradi unaposimamiwa na *consultant* kwa manufaa ya mteja wake ana uwezo wa kumwambia mkandarasi vunja hapa, vunja kabisa hapa uanze upya kwa sababu kazi imeharibika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili naomba wakati wa kutengeneza kanuni ikumbukwe kwamba Sheria ya Bodi ya Makandarasi inaruhusu *labor contract* yaani mkandarasi kabisa anakuja anapewa mkataba wa kutoa *labor* tu. Mnanunua vifaa nyinyi wenyewe, mnamkabidhi yeye anajenga na anasimamiwa na *consultant* na kukiwa na kosa lolote kuna Bodi za kumuwajibisha na kazi inatoka vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ndiyo ambayo ningependa kuyasema lakini kwa kweli kwa mradi wa maji tunapenda sana kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa sababu ametumia nguvu nyingi sana kutufikisha hapo tulipokuwa mradi ambao wakati mimi naingia madarakani ulikuwa umekwama kabisa na *site* ilikuwa inakaribia kugeuka kichaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu pia tunamshukuru amekuja *site* pale mara nyingi na kuhimiza na bila kumsahau Mheshimiwa Waziri Aweso kwa kweli amefanya kazi nzuri sana mapaka hapo tulipofikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja lakini napendekeza hayo mabadiliko kidogo katika Azimio linalohusiana

na mradi huu wa Same – Mwanga – Korogwe ili mradi uendelee vizuri kama ambavyo umekuwa unaenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tadayo ahsante sana. Mheshimiwa Justin Nyamoga, mchangiaji wetu wa mwisho jioni hii karibu.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa na mimi ya kuchangia. Awali ya yote niseme naunga mkono hoja zote tatu kama zilivyo. Nimesali sana, nimemuomba Mungu anisaidie hata katika kuchagua ni kitu gani cha kuchangia katika hoja zilizoko mbele yetu. Wakati napitia nimegundua kwamba wengi waliitwa kwenye Kamati lakini kuna kundi moja ambalo halina hata uwezo wa kuitwa kwenye Kamati ambalo hela zao pia zimefanyiwa matumizi mabaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma taarifa ya *LAAC* ukurasa wa 42 inazungumzia shilingi bilioni 260 za wastaafu ambazo hazikuwasilishwa kama zilivyokusudiwa. Mimi ni Mkristo na ninaamini wako baadhi viongozi wengi ni Wakristo wengine huwa nawaona kanisani na wapo Waislam nawaona wamevaa kanzu najua wanaenda msikitini na wote tuko humu na tunaamini siku moja huenda tutaenda mahali kwingine na tunategemea tutapokelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi humu ndani tumepigiwa kura, kuna watu ambao wamestaafu walitupigia kura ambao hela zao hazijaenda shilingi bilioni 260. Hawa watu kinachofanyika sasa hivi na mimi sijui kama Mheshimiwa Waziri wa Fedha anafahamu na mimi ninao watu kwa majina ambao baada ya kustaafu imebidi wachukue hela yaani wanaenda kukopa kwenye mikopo umiza ili wachangie kwenye mifuko hizi fedha ambazo hazikupelekwa ndipo sasa walipwe mafao yao na hii mifuko inatabia ya kuwaambia; kwa sababu mwajiri wako hakuleta fedha nenda kalete hizi fedha ukamilishe michango yako ndipo tukulipe hizi fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu mtu amestaafu, mshahara wake tunaujua, walimu tunajua mishahra yao na watumishi wengine wote tunajua mishahara yao. Akishastaafu ndipo anapotakiwa sasa yeye hizi fedha za shilingi bilioni 260 zimetumika vibaya, yeye apeleke hela zake. Kama kweli tuna imani, kama kweli kila mtu anamjua Mungu, tunawezaje kutokufikiria kuzirudisha hizi shilingi bilioni 260 mara moja kwenye hii mifuko ili hawa watu wasiendelee kuumia baada ya kulipwa mishahara midogo, hiyo hiyo imekatwa na hiyo hiyo tena waende wakaongeze kwenye mifuko? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hili ningetamani Wizara husika itoe hizi shilingi bilioni 260 ili hawa watu wasiendelee kusumbuliwa, hawa ambao ni wastaafu. Hata wakati tunaendelea kujadili humu, tutatoka Ijumaa tutaenda misikitini, Jumapili tutaenda makanisani tuwe na kumbukumbu tunafuatiliwa na shilingi bilioni 260 za hawa wazee tutasali, tutaswali? Kwa sababu hawa hawana *forum,* hao wengine wataitwa wajitetee, hao wengine wataitwa kutoa maelezo; hawa wako majumbani wameshastaafu na hawana namna nyingine zaidi ya sisi waliotupigia kura kuwasemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inaonyesha jinsi ambavyo hofu ya watumishi katika halmashauri zetu imepungua. Umeiba za miradi, umeiba na nyingine nyingine zote ukamaliza ukaona bora utamani hata za mstaafu ambaye ni michango yake. Hapa tukifikia hapa maana yake kwanza hofu kwa Serikali imetoka, hofu kwa jeshi imetoka, hofu kwa magereza imetoka, kikubwa zaidi hata hofu kwa Mungu imetoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu watakaoumia ni hawa wastaafu. Ushauri wangu kwenye hili; hii kauli ya mifuko kusema kwamba kalete hela iangaliwe upya. Mimi najua Waziri anayehusika na Utumishi anafahamu hili jambo na viongozi wengine wasaidieni hawa wazee wasirudishwe nyumbani kuambiwa kwamba kalete fedha ndipo ulipwe mafao yao; siyo yeye aliyejikata zile hela, kuna halmashauri ilikata mnaijua. Sasa je, ni mifuko tumeshindwa kweli kuidhibiti mifuko na halmashauri na hizi fedha zinatoka Hazina? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, basi hiyo halmashauri si ikatwe fedha zake nyingine hawa watu wakalipwa fedha zao badala ya yeye kuumia? Shilingi bilioni 260, shilingi bilioni 260 zirudishwe. *(Makofi)*

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nyamoga kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Esther Matiko.

**TAARIFA**

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka nimpe taarifa mchangiaji kwamba wastaafu wanaopata adha hiyo siyo tu wa kwenye halmashauri, wako pia wa Serikali Kuu na taasisi na mashirika mengine. Kwa hiyo, wote hawa waingizwe walipwe hela zao wasidaiwe hela ambazo haikupelekwa pamoja na *penalty* huwa wanaambiwa watoe. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Justin taarifa unaipokea?

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea kwa sababu wote ni wastaafu na wote ni wazee na wote hawa ni ndugu zetu na sisi huku kila siku tunawasumbua Mawaziri, kila siku utaenda unamnong'oneza; Mheshimiwa Waziri kuna huyu anasema hivi, kuna sababu gani ya kufanya kama hivi vitu vinajulikana? Ziagizeni hizo taasisi zote, taasisi yoyote ambayo haikupeleka iagizeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Fedha kama hao wana fedha huko basi peleka moja kwa moja kwenye mifuko ili hawa watu walipwe. Ninatamani mngewaona wanavyozunguka na kutufuata huko na kutuomba ili tuweze kusaidia na hapa ndipo tunapoweza kusema ili nitatue hili tatizo kwa pamoja tusaidie watu wengine. Hawa wastaafu wahudumiwe wasaidiwe waweze kubaki na ustaafu wao vizuri. Hawana kitu kingine wanachotegemea isipokuwa hizo akiba zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu hapa tutawaona sasa ndiyo hao wataenda kwenye hiyo mikopo umiza, riba kubwa na nini kwa sababu bado wana watoto wanasoma wako vyuo vikuu, bado wana mambo ambayo wanataka kuyafanya. Kwa hofu ya Mungu kama hatuna hofu nyingine yoyote kwa hofu ya Mungu tutafute namna bora ya kuhakikisha wastaafu wa Nchi hii hawapati tena adha kwa sababu ya uzembe wa watu wegine iwe kwenye halmashauri, iwe kwenye Serikali za Mitaa, iwe kwenye mashirika ya umma, tuwasaidie hawa hata sisi ni wazee wa kesho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ifike mahali hata kama unataka kuiba basi uchague unaiba wapi. Unaiba kila mahali, kila mahali, mpaka hela za mzee na mwisho wa siku unaiba ni za ndugu zako. Sasa mwisho tumeiba na za kufa na kuzikana. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani tumeiba za waliohai zimeisha, tumeenda hadi kuiba za kufa na kuzikana; tunaanza kujadili hapa za kufa na kuzikana ziliibiwa kiasi gani? Tunakwenda wapi ndugu zangu? Kwa hiyo, mimi ninazungumzia zaidi hili la wastaafu kwa sababu hawa wako hai na wanahitaji hizo hela kwa ajili ya kuendelea kuhudumia familia zao. Hawana mshahara tena, hawana kiinua mgongo kingine isipokuwa hicho walichochangia kwa miaka waliyohudumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeamua kutumia muda wangu wote kuzungumzia hili kwa sababu ninajua jinsi wanavyoumia na ninajua Wabunge wengi hapa wanatembea na bahasha za hao wastaafu ambao taarifa zao tunazikusanya huko kwenu ili tusiwasumbue nyie kuzikusanya litolewe agizo moja hapa hesabu zote za wastaafu ambazo hazijapelekwa kwenye mifuko hiyo fedha ipelekwe walipwe kama walivyostahili na wasisumbuliwe wao kupeleka hela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mifano kwa majina kutoka kwenye Halmashauri yangu ambao wameambiwa kupeleka fedha. Wako waliomudu kupeleka na wako ambao hawajapeleka bado wanatafuta na wengine ndiyo hao watasema Mheshimiwa Mbunge kama unaweza nikopeshe lakini kuna suluhu ya moja kwa moja. Tukumbuke hawa hawaji humu

Bungeni, hawa tayari wamestaafu hawana *forum,* hawana vyama vya Wafanyakazi, tayari wameshaondolewa kwenye vyama vya wafanyakazi lakini tukumbuke hawa ni wazee, ndiyo weanaotumombea, ndiyo wanaosema Mungu tubariki; watasemaje Mungu atubariki na sisi hatujawasaidia kwa jambo lolote? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tunapotaka kufikia kwenye hizi dhuluma za aina hii hazitatufikisha popote na hata hao wanaochukua hizo hela haziwezi kuwa za baraka kwa namna yoyote ile kwa sababu hazitokani na haki yoyote. Mbaya zaidi zinaacha majonzi na manung'uniko na majonzi na machozi ya damu kwa hao ambao wamewadhulumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili lichukuliwe kwa uzito wake na wakati wa kutoa taarifa hapa itoke kauli kutoka kwenye Serikali namna gani wastaafu hawatasumbuliwa tena kuambiwa wapeleke hela ambazo ni hizi hapa zimekatwa na zimeliwa na watu ambazo hazijarejeshwa. Halafu tutakuwa tumewatendea haki halafu tutabarikiwa na Mungu kwa sababu tutakuwa tumewatendea haki wasiokuwa na uwezo wa kujisemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakuwa tumekuwa sauti ya wasiokuwa na sauti, vinginevyo kila mtu nafsi yake imuhukumu kwa namna gani amewahudumia hawa kwa nafasi yako uliyonayo; kama ni Waziri wa Utumishi, kama ni Waziri wa Fedha kama ni Naibu Waziri maana kwamba hawajawahi kuja kuona kama ni Katibu Mkuu huko wa Utumishi au kiongozi yeyote wa mfuko ukumbuke ni wazee wangapi wamekuja pale wamepanga foleni wamekaa siku nzima na wewe bado umewaambia wakatafute hela waje wakulipe ili waje uwalipe mafao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani, haiwezekani, haiwezekani; ifike wakati kitu kieleweke kwamba hawa ni wazee, ni wastaafu. Kwenye matibabu bure tumewasumbua ni shida, kila mahali tumewasumbua; sasa hata hela zao tulizowakata nazo hatutaki kuwalipa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kwa neema ya Mungu wa Mbinguni hili litasikiwa na ninaamini majibu yatakapokuja

hakutakuwa na mstaafu atakayepeleka hela tena Serikalini ili alipwe mafao yake.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Muda wako umeisha.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, muda ulishaisha Mheshimiwa Jesca pole sana.

Waheshimiwa Wabunge nawashukuru sana kwa mjadala uliyo mbele yetu na tumefikia mwisho kwa jioni hii ya leo. Tunawapongeza wote mliopata nafasi ya kuchangia na ninaamini Serikali pia imesikia na itapata nafasi ya kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya maeneo. Baada ya kusema haya naahirisha Shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.42 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumamosi, Tarehe 4 Novemba, 2023 Saa Tatu Asubuhi)*